MADA: "MOFOFONOLOJIA YA KISWAHILI SANIFU NA KIKIKUYU SANIFU; MATHALANI KIKIKUYU CHA KABETE: ULINGANISHI"

NA: MARGARET WANGARI NJUGUNA.

"Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya "Master of Arts: katika Chuo Kikuu cha Nairobi."

June, 1992.

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
0101495 0

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika mahitaji ya Digrii katika Chuo kingine cho-chote.

MARGARET WANGARI NJUGUNA
(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu.

CECILIA M. THANDE

KITHAKA WA MBERIA

PROFESSOR MOHAMED BAKARI
(Wasimamizi)

TABARUKU.

Ni kwa Daktari Charles Irungu, au Baba L.iz; ambaye amegharamia, si masomo tu, bali, na maisha yangu.

Pia ni kwa ndugu wangu wapendwa, George Chege Njuguna na Patrick Kariuki Njuguna,. dada wangu wapendwa; Christine Muthoni Njuguna na Lucy Wanjiru Njuguna.

Mwisho, na kwa tafswili, ni kwa mpwa wangu mpenzi, Elizabeth Wangari Irungu, au Liz.

Sina rafiki kama yeye.

1.

" .......... Ela langu siliwati, nshishiyelo ni lilo."

Abdilatif Abdalla (1976:3)

FIKIRAONO

'Bahati'

Bwana shahabu ndu yangu, hino dunia ya wawi,
Watizame walimwengu, walitendalo haliwi,
Hii kadara ya mungu, viumbe hatuijui,
Bahati hwenda kwa wawi, wema tukalia ngowa.

Bahati zimegeuka, wa tatu hazidishiwi,
Wa moja hufurahika, mbili hazimsumbuwi,
Mkavu hunawirika, mbichi hauchipuwi,
Bahati hwenda kwa wawi, wema wakalia ngowa.

Wenye fahari na sifa, na leo hawasifiwi,
Sasa ni watu dhaifu, shaurini hawatiwi,
Kiwa kimengia ufa, kiana hakitumiwi,
Bahati hwenda kwa wawi, wema wakalia ngowa.

Wa kisambo hula nyama, wa samli hula tuwi,
Simba amekuwa ndama, makucha hayapapuwi,
Kieleacho chazama, shina limekuwa tawi,
Bahati hwenda kwa wawi, wema wakalia ngowa.

Tamati si miujiza, Akhe tu sifanikiwi,
Ilahi ndiye muweza, mara jua halituwi,
Pagumu hupalegeza, maiti akamuhui,
Bahati hwenda kwa wawi, wema wakalia ngowa.

## SHUKRANI

Kwa utafiti ambao si mchango wa mtu mmoja, ninakuwa sina budi kuwashukuru watu kadha ambao wamechangia kwa njia moja au nyingine kuifulia kazi hii dafu.

Kwanza, namshukuru ndugu wangu mpendwa, Daktari Charles Irungu. Ni kwa dhamana yake ambapo nimepata fursa ya kuzingatia masomo haya.

Ninaowashukuru pili, ni wasimamizi wangu Prof. Mohamed Bakari, Cecilia Thande na Kithaka wa mberia. Mawazo yao, yakiwa mengi; yakiwa machache; yamenisaidia kuvyaza kazi bora kuliko ingevyokuwa bila usaidizi wao.

Shukrani zangu pia ni kwa Dkt. Jacqueline Oduol. Alinipa mwanzo mwema, nilipokuwa nimelemewa katika usuli wa utafiti huu.

Ningependa kumshukuru Kyallo W. Wamitilla, kwa kunishajiisha katika nenda rudi za kufa moyo, katika jumla ya mkondo wa masomo haya, nilipomtokezea, wakati wowote. Namwambia : na si chati; "Ahsante".

Shukrani zangu nyingine ni kwa Amir Swaleh na Yang, ambao, pia tulidurusu nao. Akhe wengine ambao nawashukuru sana na kwa dhati, ni Hellen Kitavi, Helle Gesare,Zena, Wasike; kwa moyo wake mkunjufu, Manyora, Sembatya, K. Kimaita, Kabatesi Kibitsu, Jacinta, Kamau wa Mbuguah, Wanjema Kago, Mgullu,Mwaka; kwa kunipa moyo siku zote na Agnes W. Gatehi: kwa sala nyingi alizonisemea.

Maktabani; nitabaki na deni kutomshukuru Ogeto. Pamoja na Njuguna wamenifaa tangu mwanzo.

Iliyopita shukrani : ikapenyeza na tabaruku ni kwa Heneri, au Baba yake Mũmbi. Siwezi kumsahau mwalimu na mwandani wangu Prof. J. Kitsao. Angakuwa mwalimu wangu wa zamani, Prof. L. Omondi amekuwa sahibu.

Shukrani zangu za ziada ni kwa mwalimu wangu mpendwa Prof. Mohamed Bakari, kwa kunipa misingi dhabiti katika somo la fonolojia.

Karidha ilosalia ni kwa: Prof. M. H. Abdulaziz kwa usaidizi wake wa aina moja au nyingine; Njuguna Mutonya, Kineene wa Mutiso na mpendwa ndugu Mutegi Mukobwa.

Pia nawashukuru sana Esther na Patricia kwa masaa yao mengi walio-yatolea kunipigia kazi hii chapa.

Ghayati,ni kwa mpwa wangu mpendwa Liz. Uchache wake wa umri haukupunguza mchango wake hasa kazi iliponiwia nyingi. Wote nawaambia: "Ahsanteni sana".

Ninachosheheni, peke yangu; ni makosa yangu; lakini aliyejaalia yote hayo, ni Rabahu. Tunampa shukrani anazostahiki.

## TANBIHI

1. A. Abdalla. (1976): Sauti ya Dhiki. Oxford University Press. Nairobi. 3.

2. Hatukupata chimbuko asilia la nudhumu hii, lakini si utunzi wetu asilia. Tulilinakili kutoka karatasi ya mtihani wa Kiswahili wa K.C.E. (1984) karatasi nambari 302/1. Kenya Examination Council .

# DHAHANIA

Kazi hii imelenga kulinganisha halia za Kisauti ambazo zipo katika Kiswahili sanifu na Kikikuyu sanifu.

Hata hivyo tumeona umuhimu wa kulinganisha Kikikuyu sanifu, na Kikikuyu cha Kabete.

Lahaja hizi zipo chini ya lahaja ya kusini, kwa mujibu wa Karega (1977). Katika utangulizi, sura ya kwanza, tumepima Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete katika viwango vya fonetiki, na mofolojia na kupata matokeo sawa.

Tukataka basi kuipa uzito kazi hii kwa kulinganisha na Kiswahili sanifu kwani data zile zikitoa mshabaha na pia tukiona uzani zaidi, katika kuchukua data ya lugha ambayo inayo wazungumzaji wazaliwa wake.

Tunasema hivyo kwa sababu hatuwezi kutenga wazungumzaji wazaliwa wa Kikikuyu sanifu, tukasema "Ndio hawa". Hivi ni kutokana na jambo kwamba, lahaja moja huteuliwa iwe, au itumike kama lugha sanifu, ili kukidhi mahitaji rasmi ya uandishi na utangazaji katika muktadha wa lahaja nyingi, au kadha.

Kwa jumla, lipo tatizo la kuweza kupambanua tofauti za kimatamshi kwa kutegemea maandishi ya kawaida au othografia ya lugha ya Kikikuyu. Sauti [b] na [f] huwakilishwa na sauti moja ile [b] Sauti kama vile [s], [š] na [č] huwakilishwa na sauti moja, 's'. Kwa hivyo tulionelea kwamba data ya kimaandishi haitatumulikia sarufi ya Kikikuyu sanifu kikamilifu.

Ndio sababu ya kutumia data inayofanana, ambayo tumeikusanya kutoka rutuba ya uasilia wake: wazungumzaji - wazaliwa hasa wa eneo la Kabete.

Baadaye tumelinganisha halia zile za kifonolojia na kukuta kuwa hata katika kiwango cha fonolojia, Kikikuyu cha Kabete ndicho hicho hicho: Kikikuyu sanifu. Cha Murang'a ndicho sanifu!!

Kisha tumelinganisha lahaja zile mbili sanifu, Kiswahili na Kikikuyu na kuhusisha ulinganifu ule na misingi ya nadharia yetu; fonolojia asilia zalishi, kwa mujibu wa J. B. Hooper, (1976).

Tatizo ambalo tumekabili ni kuhusu istilahi za sifa-bainishi, kama walivyozifasili Chomsky na Halle (1968). Kwa kuwa kufikia sasa ni sifa moja tu; 'sonoranti' ambayo ipo katika Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha (1990), sifa tofautishi, nyinginezo; hazipo.

Kwa sababu hiyo, na bila kutaka kupotosha maana tumeandika sifa zile bainishi, kama zilivyo katika lugha ya Kiingereza; lakini kwa tahajia ya Kiswahili.

Kikikuyu

| Othografia vokali: | Ishara za kifonetiki |
|---|---|
| a | [a] |

Kikuyu Sanifu
Vokali.

| | |
|---|---|
| e | [ɛ] |
| i | [i] |
| o | [ɔ] |
| ũ | [o] |
| u | [u] |
| ĩ | [e] |
| a | |

Konsonanti

| | |
|---|---|
| b | [b] [β] |
| t | [t] |
| d | [d] |
| nj | [j] |
| k | [k] |
| g | [g] [ɣ] |
| th | [ð] |
| ch | [š] |
| h | [h] |
| m | [m] |
| n | [n] |
| ny | [ɲ] |
| ng' | [ŋ] |
| r | [r] |
| y | [j] |
| w | [w] |

Kiswahili Sanifu:
Vokali.

| Herufi za kawaida | Ishara za kifonetiki |
|---|---|
| a | [a] |
| e | [ɛ] |
| i | [i] |
| o | [ɔ] |
| u | [u] |

Konsonanti

| | |
|---|---|
| p | [p] |
| b | [b] |
| t | [t] |
| d | [d] |
| ch | [č] |
| j | [ǰ] [ɟ] |
| k | [k] |

| | |
|---|---|
| g | [g] |
| f | [f] |
| v | [v] |
| th | [θ] |
| dh | [ð] |
| s | [s] |
| z | [z] |
| sh | [š] |
| gh | [ɣ] |
| h | [h] |
| m | [m] |
| n | [n] |
| ng' | [ŋ] |
| ny | [ɲ] |
| l | [l] |
| r | [r] |
| y | [j] |
| w | [w] |

# FAHARISI


Orodha ya Yaliyomo .......... (xi)

Ungamo .......... (i)

Tabaruku .......... (ii)

Nukulu .......... (iii)

Fikiraono .......... (iv)

Shukrani .......... (v)

Tanbihi .......... (vii)

Dhahania .......... (viii)

SURA YA KWANZA

1.0.0 Utangulizi .......... 1

1.1.0 Kiswahili sanifu .......... 4

1.2.0 Tatizo .......... 4

1.3.0 Upeo na mpaka .......... 5

1.4.0 Madhumuni au lengo .......... 5

1.5.0 Haipothesia .......... 6

1.6.0 Mapitio ya vitabu .......... 6

1.7.0 Msingi wa nadharia .......... 7

1.8.0 Umuhimu wa somo hili .......... 8

1.9.0 Methodolojia .......... 9

Tanbihi .......... 10

SURA YA PILI
KISWAHILI SANIFU

2.0.0 Utangulizi .......... 11

2.1.0 SHERIA ZA MUUNDO WA SILABI UNAOPENDEKEZWA... 12

2.1.1 Kuundwa kwa nusu - vokali .......... 13

2.1.2 Ukakaaishaji .......... 18

2.1.3 Kudondoshwa kwa vokali .......... 19

2.2.0 SHERIA ZA UWIANO .................................... 28

2.2.1 Mvutano wa vokali .................................... 28

2.2.2 Mkubaliano wa vokali .................................... 30

2.2.3 Kuathiriwa kwa nasali kuhusu mahali pa kutamkia ......... 32

2.3.0 SHERIA ZA KUDHOOFIKA KWA SAUTI .................... 32

2.4.0 SHERIA ZA KUKAZANA KWA SAUTI .................... 37

2.5.0 Hitimisho .................................... 38

Tanbihi .................................... 39

SURA YA TATU

KIKIKUYU SANIFU & KIKIKUYU CHA KABETE

3.0.0 Utangulizi .................................... 40

3.1.0 SHERIA ZA MUUNDO WA SILABI UNAOPENDEKEZWA ..... 40

3.1.1 Kuundwa kwa nusu-vokali .................................... 40

3.1.2 Kudondoshwa kwa vokali .................................... 44

3.1.3 Kudondoshwa kwakonsonanti .................................... 47

3.1.4 Kudondoshwa kwa nasali .................................... 47

3.1.5 Kudondoshwa kwa vilainisho .................................... 48

3.1.6 Ukakaaishaji .................................... 49

3.2.0 SHERIA ZA UWIANO .................................... 50

3.2.1 Kuathiriwa kwa nasali kuhusu mahali pa kutamkia ........ 50

3.2.2 Sifa ya ughuna .................................... 52

3.2.3 Sifa : Iso - ghuna .................................... 53

3.2.4 Uwiano wa vokali .................................... 55

3.3.0 KUKAZANA KWA SAUTI .................................... 58

3.4.0 Hitimisho .................................... 62

Tanbihi .................................... 63

## SURA YA NNE

## ULINGANISHI


4.0.0 Utangulizi .................................... 64

4.1.0 SHERIA ZA MUUNDO WA SILABI UNAOPENDEKEZWA ...... 64

4.1.1 Kuundwa kwa nusu-vokali .............................. 64

4.1.2 Kudondoshwa kwa vokali .............................. 66

4.1.3 Kudondoshwa kwa konsonanti .......................... 67

4.1.4 Ukakaaishaji .................................... 68

4.2.0 SHERIA ZA UWIANO .................................... 69

4.2.1 Kuathiriwa kwa nasali kuhusu mahali pa kutamkia ........ 69

4.2.2 Sifa ya ughuna .................................... 70

4.2.3 Sifa : Iso - ghuna.................................... 71

4.2.4 Uwiano wa vokali .................................... 71

4.3.0 KUDHOOFIKA KWA SAUTI .............................. 73

4.4.0 KUKAZANA KWA SAUTI .............................. 73

4.5.0 Hitimisho .................................... 76


## SURA YA TANO


5.0.0 Utangulizi .................................... 79

5.1.0 Jukumu la Fonolojia asilia zalishi ...................... 79

5.1.1 Dhana ya Uasilia .................................... 81

5.2.0 HALIA ZA KISAUTI .................................... 82

5.3.0 MABADILIKO YANAYOHUSU KONSONANTI.............. 84

5.3.1 Ukakaaishaji .................................... 84

5.3.2 Kudondoshwa kwa konsonanti .......................... 85

5.3.3 Kuathiriwa kwa nasali kuhusu mahali pa kutamkia ....... 86

5.3.4 Sifa ya Ughuna .................................... 86

5.3.5 Sheria ya Dahl .................................... 86

5.3.6 Kukazana kwa sauti .................................... 87

5.3.7 Kudhoofika kwa sauti .................................... 88

5.4.0 MABADILIKO YANAYOHUSU VOKALI .................. 89

5.4.1 Kuundwa kwa nusu - vokali .......................... 89

5.4.2 Kudondoshwa kwa vokali ............................ 90

5.4.3 Mvutano wa vokali ................................... 91

5.4.4 Mkubaliano wa vokali ............................... 91

5.5.0 Hitimisho ................................................ 92

Tanbihi ................................................... 94

SURA YA SITA - HITIMISHO

6.0.0 Utangulizi ............................................... 95

6.1.0 Ulinganishi ............................................. 96

6.2.0 Hitimisho ................................................ 97

6.2.1 Pendekezo .............................................. 98

Tanbihi ................................................... 99

MAREJELEO .............................................. 100

Ziada ....................................................... 103

## 1.0.0 SURA YA KWANZA.

## UTANGULIZ I .

Lengo letu la kimsingi katika utafiti huu ni kulinganisha mifanyiko ya kifonolojia, inayopatikana katika Kiswahili sanifu, na Kikikuyu sanifu.

Pamoja na kutekeleza lengo hilo, tumetaka kuipa uzito kazi hii kwa kulinganisha pia na lahaja ambayo inafasiliwa kimaeneo, Kikikuyu cha Kabete.

Usanifishaji ni jambo ambalo hufanywa, kwa minajili ya kuchagua lahaja rasmi, miongoni mwa lahaja kadha, katika mazingira ya lugha, yaliyo na wingi wa lahaja.

Lahaja moja huteuliwa ili iweze kutumiwa katika shughuli rasmi za uchapishaji na utangazaji.

Kiswahlili sanifu kilisanifishwa tokana na lahaja ya Ki-unguja.

Mpaka leo kimekidhia mahitaji rasmi ya mawasiliano, uandishi na utangazaji.

Kuhusu Kikikuyu sanifu, Karega (1977) na Mukuriah (1987) wanakubaliana kimaoni, kuhusu ukweli kuwa lahaja waiitayo ya kusini, ndiyo inayotumika kama Kikikuyu sanifu.

Ni vigumu kusema wazungumzaji-wazaliwa wa lugha sanifu "ni hawa".

Na kwa hivyo, tunaleta katika mandhari, lahaja nyingineyo yenye fasili ya kimaeneo na ambayo inao wazungumzaji-wazaliwa wake, ambao wamejulikana na wazungmzaji-wazaliwa wengine kama "AKabete"; mmoja "MoKabete".

Tumeeleza eneo la Kabete kama lililopo katika wilaya ya Nairobi katika sehemu moja, na wilaya ya Kiambu; katika kufuata mipaka ya kisiasa.

Sehemu ambazo zipo chini ya kule tulikokufasili kama Kabete ni maeneo ya Kangemi, Kabete, Uthiru, Ndumbu-ini, Eni, Gatina, Kinoo, na sehemu ya Gitaru.

Tumethibitisha kwa faridi za kiismu, kuwa Iugha inayozungumzwa katika eneo lile, ambalo linajulikana kama Kabete kwa jumla inafanana.

Tutaonyesha hivi punde faridi zile za kiismu ambazo tumetumia kuipima kama lahaja.

Almuradi sababu ya kuitalii ni kuongeza utafiti wetu uzito, tutajishughulisha na Kiswahili sanifu dhidi ya Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete.

Karega (1977;96) anasema kuwa lahaja ya kusini ya Kikikuyu ni ile iliyokaribiana na lahaja ya kaskazini lakini badala ya sauti /f/ ambayo inatumiwa katika lahaja ya kaskazini inatumia sauti ya /β/. Anasema:

> "Lahaja hizi mbili ni karibu sawa. Tofauti kati ya lahaja ya kaskazini na lahaja ya kusini ni kuwa wakati ambapo lahaja ya kaskazini inashabihiana na Kimathira kwa kuwa na sauti ya /f/ < * B lahaja ya kusini ina /β/ < * B. Katika mabadiliko mengine yote lahaja hizi mbili zinamithiliana".[1]

Akieleza kuwa lahaja ya kusini ni ile iliyoenea kutoka mto wa Mathioya hadi

.../2

mji wa Nairobi, na tukijua kuwa lugha sanifu ni ile inayotumiwa kwa shughuli rasmi za uandishi na utangazaji, tunachukulia zote: Kiswahili sanifu na Kikikuyu cha Kabete kuwa chini ya lahaja ya kusini.

Vikiwepo vigezo vinginevyo vya kupimia lugha, tutatumia vigezo vya kisauti na kimofolojia, kuonyesha kuwa isipokuwa majina yake, Kikikuyu sanifu hakitofautiani kamwe na Kikikuyu cha Kabete. Kwa hivyo, lakabu ya "Kikikuyu cha Kabete" katika kazi hii itakuwa ni istilahi ambayo inatumiwa pia na wazungumzaji - wazaliwa wengine kuashiria Kikikuyu cha eneo fulani, Kabete.

Baadaye tutaeleza ni kwa nini tumechagua kulinganisha Kiswahili sanifu na Kikikuyu sanifu na nyongeza ya lahaja nyingineyo: Kikikuyu cha Kabete.

Tumeonyesha chati za vokali na konsonanti, na baadaye mofimu za ngeli zinazopatikana katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete, ambazo: zimelingana. Hiyo inathibitisha kuwa data: au ya Kikikuyu sanifu, ama ya Kikikuyu cha Kabete ni sawa, katika utafiti huu.

VOKALI

| Kikikuyu Sanifu | Kikikuyu cha Kabete |
|---|---|
| [a] | [a] |
| [ɛ] | [ɛ] |
| [e] | [e] |
| [i] | [i] |
| [o] | [o] |
| [u] | [u] |

Konsonanti

| | |
|---|---|
| [b] | [b] |
| [β] | [β] |
| [t] | [t] |
| [d] | [d] |
| [ǰ] | [ǰ] |
| [k] | [k] |
| [g] | [g] |
| [ð] | [ð] |
| [ɣ] | [ɣ] |
| [š] | [š] |
| [h] | [h] |
| [m] | [m] |
| [n] | [n] |
| [ɲ] | [ɲ] |
| [ŋ] | [ŋ] |

[r] [r]

[j] [j]

[w] [w]

Tunatoa pia makundi ya ngeli ya Kikikuyu sanifu kwa mujibu wa Mukuriah (1987 ). Kwa kuwa hakuna utafiti wo-wote uliofanywa kuhusu Kikikuyu cha Kabete, imetuwajibikia kurejelea data ya lugha hiyo, kama inavyozungumzwa hivi leo, ili kuweza kuthibitisha mofimu za makundi ya ngeli.

<u>NGELI</u>

| | Kikikuyu Sanifu | | Kikikuyu cha Kabete |
|---|---|---|---|
| 1 | {mo} | 1 | {mo-} |
| 2 | {a-} | 2 | {a-} |
| 3 | {mo-} | 3 | {mo-} |
| 4 | {me-} | 4 | {me-} |
| 5 | {re-} au{i-} | 5 | {re-}au{i-} |
| 6 | {ma-} | 6 | {ma-} |
| 7 | {ke-} | 7 | {ke-} |
| 8 | {i-} | 8 | {i-} |
| 9 | {n}au{ϕ} | 9 | {n-}au{ϕ-} |
| 10 | wingi wa ngeli ya 9 | 10 | wingi wa ngeli ya 9 |
| 11 | {ro-} | 11 | {ro-} |
| 12 | {ka-} | 12 | {ka-} |
| 13 | {to-} | 13 | {to-} |
| 14 | {o-} | 14 | {o-} |
| 15 | {ko-} | 15 | {ko-} |
| 16 | {ha-} | 16 | {ha-} |
| 17 | {ko-} | 17 | {ko-} |

Ikiwa hakuna tofauti kati ya lahaja hizi mbili; tofauti ni ya vijelezi tu, kuwa Kiswahili sanifu ni jina la lahaja inayokidhi mahitaji rasmi kama vile uandishi na utangazaji. Karega (1977) na Mukuriah (1987) wanaelekea kukubaliana kimaoni kuhusu dai hili .

"Kikikuyu cha Kabete" kwa upande wake ni lahaja ambayo ina lakabu ya lahaja lakini kwa msingi wa kimaeneo, au kijografia. Kwa kuwa data yake imechukuliwa katika uasilia wa mazingira yake, tunanuia kuipa kazi yetu uzito zaidi kwa kuhimili data ya Kikikuyu sanifu, ambayo tumeitoa kutoka vipindi vya matangazo, vya redio.

Tunaona data hiyo kama ya "kidhahania" kwa kiasi kidogo. Sababu ni kuwa data yake ya kimaandishi haionyeshi tofauti za matamshi. kwa mfano:

| ,Kikikuyu | Kikikuyu | Maana katika Kiswahili |
|---|---|---|
| 'baba' | [βaβa] | "baba" |
| 'cumbi' | [šu:be] | "chumvi" |
| 'cucu' | [šo:šǒ] | "nyanya" |

Inahitaji ujuzi wa sauti ipi inawakilishwa na ishara ipi kifonetiki. Lugha kimatendo inatuonyesha wazi-wazi tofauti za kimatamshi. Ndipo tukatumia data -pacha: Kikikuyu cha Kabete na Kikikuyu sanifu, na kulinganisha na Kiswahili sanifu.

## 1.1.0 KISWAHILI SANIFU

Kiswahili ni lugha ambayo imenea katika matumizi na si ajabu basi, kuwa kinaendelea kufanyiwa utafiti.

Anavyosema Bakari (1982: 5) ni kuwa:-

> "Kiswahili ni mojawapo ya lugha za kiafrika ambazo zimeenea sana barani Afrika."[2]

Ni lugha ambayo inazungumzwa na wakazi wa mwambao wa Afrika mashariki. Eneo lake, chambilecho Bakari (1982) ni, kaskazini kutoka nchi ya Somalia, hadi visiwa vya Komoro, kusini.

Tunapozungumza kuhusu Kiswahili sanifu, tuna maana ya, lugha ambayo iliteuliwa kwa matumizi rasmi ya uandishi na utangazaji.

Kama inavyojulikana tayari, msingi ambao Kiswahili sanifu kilitokana nao ni lahaja ya Unguja au Zanzibar.

Mukuriah (1987: 1) anaelekea kusema kuwa:

> "Lakini kwa vile Kiswahili sanifu kinatumiwa na watu wengi wenye tofauti za kitamaduni kiuchumi na kisiasa kimeathiriwa sana na msamiati kutoka lugha mbalimbali."[3]

Si rahisi, kwa hivyo, kufahamu idadi kamili ya watu wanaozungumza Kiswahili sanifu. Sababu ni kwamba wazungumzaji hao wametapakaa, wengi wao wakiwa na lugha za kwanza tofauti tofauti.

Watu hama hao: Mukuriah (1987:1): "hukitumia Kiswahili kama lugha sambazi"[4]

## 1.2.0 TATIZO.

Utafiti wetu haujashughulikiwa katika kiwango cha fonolojia. Tunamaanisha

kuwa katika kiwango cha fonolojia, Kiswahili sanifu hakijalinganishwa na Kikikuyu sanifu.

Lakini kimewahi kulinganishwa na lugha na lahaja zinginezo za Kiswahili kama Kitumbatu, Ki pemba na Kimakunduchi.

Katika kiwango cha mofolojia, Mukuriah (1987) amekilinganisha na Kikikuyu sanifu , ambacho alichagua kukiita Kikikuyu cha Kiambu.

## 1.2.1 UPEO NA MPAKA:

Si lengo letu kuingilia kiwango cha fonolojia kiarudhi.

Nia yetu ni kutalii mabadiliko ya kifonolojia, yanayohusu vokali , konsonanti, mofimu , hata mipaka ya maneno.

Ni dhamira yetu kuchangia katika kuandika sarufi ya Lugha zile mbili. Sababu ya kusema hivi ni kuwa kila mwana-isimu anapofanya utafiti wa lugha fulani, katika kiwango cho-chote kile, huwa anachangia katika kuandika sarufi ya Lugha ile. Viwango hivyo vinaweza kuwa ni vya kifonetiki, kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia au kisemantiki.

Kwa hivyo upana wa data yetu ni mapana ya kuwakilisha umilisi wa wazungumzaji wa lugha hizi, katika kiwango cha fonolojia.

Chomsky (1965: 8) anatuonya kuwa tatizo la sarufi zalishi ni kuwa inazingatia masiala ambayo yana msingi wake katika mifanyiko ya kiakili, au kisaikolojia.

Anatueleza kuwa jukumu la mwana-isimu ni kuelezea umilisi wa mzungumzaji-mzaliwa, na wala sio maoni yake kuhusu umilisi wa lugha yake. Anasema: (1965:8)

> "Kwa sababu hiyo, sarufi- zalishi inajaribu kuonyesha kile ambacho mzungumzaji anajua wala sio maoni ambayo angeyatoa, kuhusu ujuzi wake huo."[5]

Utafiti wetu ni wa kiwakati sio wa kimapisi.

Isipobidi, hatuna nia ya kuingilia kwa kina, isimu-historia au lugha kimapisi, Msingi wetu wa nadharia ni fonolojia zalishi kwa mujibu wa Hooper (1976).

## 1.4.0 MADHUMUNI AU LENGO LA SOMO HILI

Kwa kuwa nadharia yetu: fonolojia zalishi ni nadharia bia ya kuandikia umilisi wa lugha za kibinadamu, tunadhamiria kulinganisha mabadililiko ya kimofofonolojia kati ya Kiswahili sanifu kwa upande mmoja; na Kikikuyu sanifu pamoja na Kikikuyu cha Kabete, kwa upande wa pili.

Kwa upande wake, kwa kulinganisha pia, fonolojia ya Kikikuyu sanifu na halia za kisauti katika Kikikuyu cha Kabete, tungependa kuchunguza kama ipo tofauti kati ya lahaja mbili hizi.

Si nia yetu kuingilia isimu-historia kwa undani, kwani somo hili likiegemea lugha kiwakati. Itakapobidi, tutarejelea misingi ya kihistoria.

Kazi yetu haitavuka mipaka ya fonolojia-kiarudhi.

Itajikita katika kiwango cha sauti tu.

## 1.5.0 HAIPOTHESIA

Somo hili lina haipothesia nne:

i) Halia za kisauti, za kimofofonolojia zipo, katika lahaja zote tatu.

ii) Kikikuyu sanifu hakithibiti tofauti yo-yote kuhusu halia hizi, kutokana na Kikikuyu cha Kabete.

iii) Upo ulinganifu wa aina fulani katika kiwango cha kisauti; hususan: kimofofonolojia, kati ya Kiswahili sanifu kwa upande mmoja; na Kikikuyu sanifu, mathalani, Kikikuyu cha Kabete; kwa upande mwingine

iv) Uasilia wa halia zote zile una nguzo katika nadharia ya fonolojia asilia zalishi: Mintaraf Hooper (1976).

## 1.6.0. MAPITIO YA VITABU

Utafiti uliofanywa kuhusu Kiswahili sanifu na Kikikuyu sanifu si mwingi.

Kama tulivyotaja tayari, katika sehemu ya 1.0.0, hakuna utafiti uliofanywa kuhusu Kikikuyu cha Kabete. Huo ni mchango ambao tumeutoa tu, tukinuia kuongeza kazi yetu uzito.

Katika kiwango cha fonolojia, C. Maganga (1990) ameandika kuhusu mofofonolojia ya Kiswahili sanifu, Kitumbatu na Kimakunduchi, na Kipemba.

Kazi yake imetufaa sana kwa sababu imetuangazia mifanyiko ya kisauti, ambayo ipo katika lahaja sanifu ya Kiswahili .

Pia imekuwa msingi mwema wa data, kwa utafiti wetu.

Maringah (1987) amelinganisha mifanyiko ya kifonolojia katika kunyambua vitenzi, kati ya Kiswahili sanifu na Kimbeere.

Kazi yake inajihusisha na mifanyiko katika mnyambuliko wa vitenzi tu. Haiingilii mazingira kama vile ya uundaji wa nomino. Utafiti wake umetufaa pia, kwa kuwa kiunzi chake cha nadharia ni fonolojia zalishi.

Bakari M. (1982) ni kazi nyingine ambayo imetupa mwongozo, kwa kuwa, hata kama utafiti huo umehusu lahaja za Kiswahili za mwambao wa Kenya, ametumia nadharia ile ile ya fonolojia-zalishi kwa mujibu wa Hooper (1973).

Kazi hii imetufaa tena, kwa kulinganisha mifanyiko kadha wa kadha kati ya lahaja tulizozishughulikia na lahaja nyinginezo za Kiswahili.

D. Muthondu (1987) ni kazi nyingine ambayo imekuwa mhimili imara, kwa utafiti wetu. Tunasema hivi kwa sababu kazi hii imeainisha ngeli za Kiswahili

sanifu, na Kikikuyu sanifu.

Kazi yetu ikihusisha viwango viwili, fonolojia na mofolojia, imekuwa haina budi kuegemea utafiti huo. Nadharia yetu inadhihirisha, viwango hivi, anaposema Hooper (1976:xi):

> "Matokeo yamekuwa nadharia mpya kabisa ambayo inaambatanisha mofolojia na fonolojia". [6]

Utafiti wake P.R. Bennet (1969) umekuwa msingi wa data ya Kikikuyu. Kinachotupa kusema hivyo ni kwa kuwa ameshughulikia unyambishi wa vitenzi, katika Kikikuyu. Data yake imetufaidi, hasa kwa upande wa halia za kisauti kama uwiano wa vokali katika viambishi mbalimbali vya vitenzi, katika lugha ya Kikikuyu. Karega (1977) ni kazi nyingine ambayo imekuwa msingi imara kwetu hasa panapohusu uainishaji wa lahaja.

Anatoa misingi thabiti ya kiismu kuonyesha vijopo vya lahaja zile, nayo imetusaidia kuelewa pale ambapo tutaratibu Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete pia. Anasema, kuhusu Kikikuyu cha Kabete (1977:8):

> "Watu wa Gichugu wanadai ya kuwa wanatofautiana sana kiismu na kuwa mtu ye-yote anayezungumza lahaja iliyo kusini mwa Ndia, ni MoKabete". [7]

Zipo kazi nyinginezo zilizoshughulikia Kikikuyu kama vile Ford (1974). Lakini hazihusiani na utafiti wetu, kwa kuwa ameshughulikia fonolojia-kiarudhi, ambayo ipo nje wa mpaka wa somo letu.

Katika upande wa nadharia, zipo kazi nyingine ambazo au zimehusiana na msingi wa nadharia tuliyoitumia, au zimefafanua kiunzi cha nadharia yetu.

Kazi zote hizo zimetusaidia katika somo letu.

Chomsky, (1965) amekuwa wa manufaa kwetu, kwani akifafanua dhana za kimsingi za isimu, kama vile umilisi na utendaji na baadhi ya majukumu ya mwana-isimu elezi.

L. M Hyman (1975) ni kazi iliyotufaa pia. Mjadala wake wa vikundi asilia na hatimaye sifa bainifu, au sifa-tofautishi zinaelekea kulingana na zile zilizopendekezwa na Chomsky na Halle, (1968); ambazo tumetumia kuelezea mifanyiko ya kifonolojia katika Kiswahili sanifu, na Kikikuyu sanifu.

Schane (1973) ndicho msingi wa mpango wetu wa mabadiliko katika makundi asilia, au katika uasilia wake.

Schane (1973) pia kimetufaa katika kuandikia sheria za fonolojia.

Msingi wa nadharia yetu ni J.B. Hooper, (1976). Ni nadharia ambayo inahusisha viwango vya fonolojia na mofolojia. Nadharia hii ina misingi yake katika dhana ya uzalishi ambao ulianzisha katika miaka ya hamsini.

Tutaifafanua zaidi katika 1.7.0, katika msingi wa nadharia.

## 1.7.0. MSINGI WA NADHARIA

Nadharia ambayo tunaitumia ni fonolojia zalishi: Hooper (1976). Nadharia hii, kwa upande mmoja, ina misingi yake katika nadharia zalishi, geuzamaumbo ambayo imekuzwa tangu miaka ya hamsini .

Theo Vennemann amechangia nadharia hii ya fonolojia zalishi hasa kuhusu tatizo la udhahania.

Kwa mapendekezo yaliyotolewa na wana-isimu wengine, imekuja kuhusisha viwango viwili, mofolojia na fonolojia.

Inahusisha maumbo ndani na maumbo nje kwa kutumia sheria za kifonolojia. Uhusiano huo ni uhusiano ambao unawez a kuthibitishwa.

Fonolojia - zalishi ni nadharia ambayo ina zaidi ya aina nne za sheria.

Zipo sheria ambazo huwa na msingi wake katika sifa za kifonetiki. Sheria hizi zinatekelezwa katika mipaka ya kifonolojia , ambayo ndiyo mipaka ya silabi, na mipaka ya vipumuo. Mipaka hii miwili ina misingi yake katika sifa za kifonetiki.

Hata hivyo, sheria inaweza kuwa ya kifonetiki, lakini ikose kutekelezwa kwa sababu ya vikwazo vya kijamii, kimofolojia au kisintaksia.

Aina ya pili ya sheria ni sheria za kimofonolojia. Sheria hizi, au za aina hii zinabadilisha sifa za kifonolojia katika mazingira ya kimofolojia au ya kisintaksia; kama vile wingi, njeo, nomino, na kitenzi.

Ipo aina ya tatu ya sheria, ambazo Hooper (1976) anaita sheria za via. Sheria hizi hutoa maelezo kama vile ya kileksia, kama vile, nomino, vitenzi na sifa nyinginezo za kileksia, au zinazohusiana na leksia.

Sheria za sandhi, nazo ni aina ya sheria ambazo hutoa maelezo ambayo hayatolewi na au sheria za kifonetiki ama za kimofofonolojia.

Maelezo haya ni kama vile mipaka ya maneno, ambayo inachukuliwa kuwa ya kisintaksia, na kisemantiki, kwa kuwa haina msingi wake katika fonolojia.

Pamoja na aina hizo nne za sheria, zipo sheria ambazo hupatikana pia, katika nadhar ia nyinginezo za kimofofonolojia.

Sheria za tahajia huzipa mofimu maumbo halisi, ilhali sheria za uundaji wa maneno huonyesha ni mofimu zipi zinafaa kufuatana na zipi, na vipi.

Za mwisho ni sheria za silabi, nazo zinahusu aina za miundo ya silabi na nafasi mbalimbali za silabi katika miundo yake.

Almuradi nadharia yetu inaturudisha katika kuandika sarufi ya lugha, ambayo ni wakilisho la umilisi wa mzungumzaji - mzaliwa unaomwezesha kuelewa sentensi ziso-ukomo, katika lugha yake.

Tukarudi kwa jukumu la kimsingi la lugha, kuwasiliana.

## 1.8.0. UMUHIMU WA SOMO HILI

Ni matumaini yetu kuwa somo, au utafiti wetu utakuwa mchango kwa utafiti wa lugha za Kibantu.

Kazi yetu inaelekea kuthibitisha dai la Hooper (1976:4) kuwa nadharia asilia

zalishi ni nadharia bia, na kuwa inaweza kutumiwa kutafitia halia za kisauti katika lugha nyingi za kibinadamu.

Tunapotalii mifanyiko ya kisauti katika Kiswahili sanifu, Kikikuyu sanifu na kikikuyu cha Kabete tunakuwa katika harakati ya kuchangia kuandika sarufi ya lugha hizi.

Tukirejelea tena anavyosema Hooper (1976:3):

"Katika nadharia zalishi, lengo la utafiti wa kimaelezi wa lugha, ni kuunda sarufi".[8]

Hatimaye, hamu yetu ni kugundua ni halia zipi za kisauti zipo katika lahaja hizi za Kikikuyu kwa kuwa hazijafanyiwa utafiti na kuona vile zilivyolingana na zile za Kiswahili sanifu.

## 1.9.0 METHODOLOJIA

Kwa upande mmoja tutakusanya data kutoka kwa maktaba.

Tunasema hivyo kwa kuwa, kwa upande mmoja tutarejelea kazi ambazo zimefanywa tayari, ambazo zinahusiana na mada hii.

Maswali ya kinadharia ni mojawapo, pamoja na utafiti uliofanywa kuhusu Kiswahili sanifu, kwani upo.

Nikiwa mzungumzaji - mzaliwa wa Kikikuyu cha Kabete, ni dhamira yetu kuchota data kutoka umilisi wetu wa lugha hiyo, na ambayo imemithili usawa na Kikikuyu sanifu, kama itakavyobainika katika kazi hii.

Hata hivyo, tunazingatia onyo la Chomsky (1965:9) anaposema:

> "Sarufi - zalishi inajaribu kueleza, bila kuingiza hisia za ubinafsi, ujuzi wa lugha kimatumizi, na mzungumzaji - msikilizaji"[9]

Ili kuepusha data yetu na ubinafsi, tutathibitisha maumbo yetu na maumbo ya wazungumzaji - wazaliwa wengineo.

Chomsky (1965:8) analalamika:

> "Imejitokeza kwa uwazi kuwa taarifa; na maoni ya mzungumzaji - kuhusu hulka na umilisi wake huweza kuwa na makosa"[10]

Kwa sababu hiyo, hatutategemea umilisi wetu tisti, ila tutahimili taswishi yo-yote na wazungumzaji - wazaliwa wengineo.

Tutatumia ishara za kifonetiki katika kuvyaza maumbo ya ndani; maumbo ya kati, pale yanapopatikana; na hatimaye, maumbo ya nje.

TANBIHI

1. E..K. Karega, (1977): Sound change and classification of the Dialects of Southern Mt. Kenya. Ph.D Thesis. University of Nairobi. 96

2. M. Bakari, (1982): The Morphophonology of the Kenyan Swahili Dialects. Ph.D Thesis. University of Nairobi. 5

3. D.M. Mukuriah, (1987): Mpangilio wa Ngeli: Ulinganishi wa Ngeli za Kiswahili sanifu na Kikikuyu cha Kiambu. M.A. Thesis. University of Nairobi. 1

4. ————————,(opp.cit). 1

5. N. Chomsky, (1965): Aspects of the Theory of Syntax. Cambridge, Mass: M.I.T. Press. 8.

6. J.B. Hooper, (1976): An Introduction to Natural Generative Phonology. New York Academic Press. xi.

7. E.K. Karega, (opp.cit). 8.

8. J.B. Hooper, (opp.cit). 3.

9. N. Chomsky, (opp.cit). 9

10. ————————,(opp.cit). 8

## 2.0.0 SURA YA PILI

Katika sura hii; madhumuni yetu ni kuratibu mabadiliko ya kifonolojia ambayo yapatikana katika Kiswahili sanifu.

Mifanyiko hii ni ya kifonolojia, na kimofofonolojia.

Hii inamaanisha kuwa zipo halia za kisauti, ambazo zina msingi wake katika sifa za kifonetiki, ilhali halia za kimofofonolojia zina misingi yake katika mofimu, au viambishi vya kimofolojia, sintaksia na hata leksia.

Muradi mifanyiko ile imejikita kwingineko, wala si misingi ya kifonetiki, hususan.

Hooper (1976:3) anaelekea kueleza kuwa jukumu la isimu - elezi ni kuandika sarufi ya lugha ile, ambayo inakuwa ni wakilisho la umilisi wa mzungumzaji - mzaliwa ambao unamwezesha kufasiri idadi iso - ukomo ya sentensi katika lugha yake. Anasema:

> "Katika nadharia zalishi, lengo la utafiti - elezi wa lugha ni kuunda sarufi ya lugha. Sarufi hii ni wakilisho la ujuzi ambao mzungumzaji - mzaliwa anao, na ambao unamwezesha kuelewa idadi iso - ukomo ya sentensi."[1]

Anasema kuhusu nadharia zalishi:

Hooper (1976:ix)

> "Nadharia hii inahitaji kuwa sheria za kifonolojia na maumbo ambayo zinawakilisha yahusianishwe kwa njia ya moja kwa moja, na maumbo ya nje."[2]

Hivi ni kama kusema kuwa, katika kuratibu seti ya sheria zinazowakilisha umilisi wa mzungumzaji - mzaliwa, tunaandika sarufi ya Kiswahili sanifu, na kwamba ni lazima tuwe na maumbo ya ndani, na maumbo ya nje ambayo yanastahili kuhusianishwa, kwa sheria za kifonolojia.

Lakini kabla hatujafanya hivyo, tunahiari kuonyesha viambishi vile vya ngeli katika Kiswahili sanifu, kwani tumezitumia.

Hatutatoa mifano katika orodha hii, au maelezo, ila tutaonyesha viambishi vile, au mofimu zinazowakilisha vikundi vile, vyenyewe, na ngeli zenyewe.

| Ngeli | Mofimu au kiambishi |
| --- | --- |
| 1 | {m-} |
| 2 | {wa-} |

3 {mu-}
4 {mi-}
5 (ki-}
6 {vi-}
7 {ji-}
8 {ma-}
9 {n-}
10 wingi wa majina katika ngeli ya tisa.
11 Imeungana na ya 14
14 {u-}
15 {ku-}
16 {pa-}
17 {ku-}
18 {ku-}

Yapo mambo mengi ambayo yanajadiliwa kuhusu ngeli hizi, sana sana zile alomofu, na kundi la 11 na 14.

Lakini hatutaingia katika mjadala huu kwa kuwa upo nje ya upeo na mpaka.

Kwa sababu hiyo, tutarejelea maelezo yetu ya awali, kuhusu yale ambayo tumeshughulikia:kwa mujibu wa Schane (1973) kulingana na uasilia wake, wala hatukugawanya halia zile, kulingana na kama ni za konsonanti, au vokali.

Msingi wa jinsi yetu ya kuratibu mabadiliko ni uasilia wa sheria zenyewe, kama anavyosema Schane (1973:207):

> "Hebu basi tuangalie kategoria tatu zile za sheria asilia ambazo tumeshughulikia zaidi katika mjadala wetu. Nitaziita sheria za uwiano, sheria za muundo wa silabi unaopendekezwa na sheria za kutofautisha sauti mbali iwezakanavyo"[3]

Lakini zipo sheria ambazo , bila shaka, hazionyeshi uasilia wo-wote. Anasema Schane (1973:206):

> "Mtu anaweza kufikiria mifanyiko ya kifonolojia isiyo asilia, ambayo haionyeshi kutokana na ile iliyo asilia."[4]

## <u>(iii) 2.1.0 SHERIA ZA MUUNDO WA SILABI UANOPENDEKEZWA</u>

Katika isimu, au katika mfululizo bia wa lugha, muundo wa silabi wa KVKV (konsonanti vokali, konsonanti vokali) unachukuliwa kuwa ndio muundo sahili zaidi wa silabi.

Muundo huu ndio unaopatikana katika lugha nyingi za Kibantu.

Kwa kusema hivyo, hatudai au hatumaanishi kuwa hakuna miundo ya aina nyingine ya silabi.

Ni kama anavyosema Hooper (1976:195) anapokuwa akieleza kuhusu masharti ya miundo ya silabi. Anasema:

> "Kufikia hapa nimejadilia muundo ulio sahili zaidi wa silabi, katika masharti ya miundo ya silabi; ule wa lugha ambayo ina miundo ya KVKV."[5]

Ni kuwa muundo huu ndio unaochukuliwa kuwa sahili kabisa, miongoni mwa miundo mingineyo.

Kuna halia za kisauti ambazo hufanyika ili kuleta muundo wa KvKv wa silabi, katika lugha.

Aina zile, mbalimbali, zimejadiliwa katika vijisehemu vya sura hii.

## 2.1.1 KUUNDWA KWA NUSU-VOKALI

Nusu-vokali imedhihiri kuundwa katika mazingira mbalimbali.

Katika viambishi vya pronomino {tu-}, {ku-} na {u-}, vinapotangulia mashina yanyoanza kwa vokali za mbele, au, zenye sifa ya [+mbele], nusu-vokali huundwa.

Ni kama anvyosema Hooper (1976), kuwa mabadiliko ya kifonolojia yanafuata ruwaza, toka umbo ndani, hadi umbo nje.

Kwa sababu hiyo, katika kudhihirisha fenomena zote za kisauti, tumeonyesha maumbo yale mawili. Umbo la ndani, na umbo la nje, pamoja na mabadiliko ya kati, ikiwa yapo.

Tunaanza kwa mazingira ambayo yanathibiti kuundwa kwa nusu-vokali au kutoundwa. Kwa kusema hivi tunamaanisha kuwa katika umbo nje, nusu-vokali huweza kuundwa, au isiundwe. Mifano inayofuatia inathibitisha.

| Umbo ndani | | umbo kati | | umbo nje | othografia |
|---|---|---|---|---|---|
| /u + amkɛ/ | ⟶ | [uamkɛ] | ~ | [wamkɛ] | 'uamke' |
| /u+ɛndɛ+ɛ/ | ⟶ | [uɛndɛ] | ~ | [wɛndɛ] | 'uende' |
| /u+imb+ɛ/ | ⟶ | [uimbɛ] | ~ | [wimbɛ] | 'uimbe' |
| /a+ku +amš +ɛ/ | ⟶ | [akuamšɛ] | ~ | akwamšɛ] | 'akuamshe' |
| /a+ku+imb + i +ɛ/ | ⟶ | [akuimbiɛ] | ~ | [akwimbiɛ] | 'akuimbie' |
| /a+ku+ɛnd+ɛ+ɛ/ | ⟶ | [akuɛndɛ:] | ~ | [akwɛndɛ:] | 'akuendee' |
| /tu+amk+ɛ/ | ⟶ | [tuamke ] | ~ | [twamkɛ] | 'tuamke' |

/tu+ɛnd +ɛ/ ⟶ [tuɛndɛ] ~ [twɛndɛ] ‘twende'

Tukizingatia sheria ya kifonolojia, tutasema:

$$\begin{bmatrix} +\text{ silabi} \\ -\text{konsonanti} \end{bmatrix} \rightarrow [-\text{silabi}] \;/\; __ \left\{ \begin{matrix} \begin{bmatrix} +\text{ juu} \\ +\text{ mbele} \end{bmatrix} \\ \\ \begin{bmatrix} -\text{ juu} \\ -\text{ chini} \\ +\text{ mbele} \end{bmatrix} \\ \\ [+\text{ chini}] \end{matrix} \right\}$$

Mazingira mengine ambapo nusu-vokali inaundwa ni wakati ambapo pronomino {mu} inafuatia mashina yanayoanzia kwa vokali za [a], [ɛ], [i], [ɔ] hata [u]. Mifano ni:

| umbo ndani | | umbo nje | othografia |
|---|---|---|---|
| /mu + amk +ɛ/ | — | [mwa mkɛ] | ‘mwamke' |
| /mu +ɛnd +ɛ/ | — | [mwɛndɛ] | ‘mwende' |
| /mu + imb +ɛ/ | — | [mwi mbɛ] | ‘muimbe' |

| umbo ndani | | umbo nje | othografia |
|---|---|---|---|
| /mu +ɔn +ɛ/ | ⟶ | [mwɔ nɛ] | ‘muone' |
| /mu +uliz + ɛ/ | ⟶ | [mwu.lizɛ] | ‘muulize' |
| /mu +ɛlɛk +ɛ/ | ⟶ | mwɛlɛkɛ] | ‘mueleke' |
| /mu + inam +ɛ/ | ⟶ | [mwinamɛ] | ‘muiname' |
| /mu +ɔgɛ/ | ⟶ | [mwɔgɛ] | ‘muoge' |
| /mu +ɛpuk +ɛ/ | ⟶ | [mwɛpukɛ] | ‘muepuke' |
| /mu +ɛ+ lɛ+ɛ/ | ⟶ | [mwɛlɛ:] | ‘muelee' |
| /mu + itiš +ɛ/ | ⟶ | [mwitišɛ] | ‘mwitishe' |
| /mu + inu +ɛ/ | ⟶ | [mwinuɛ] | ‘mwinue' |
| /mu + izɛ/ | ⟶ | [mwizɛ] | ‘mwize' |
| /mu + iŋgine/ | ⟶ | [mwiŋginɛ] | ‘mwingine' |

Viambisho vya ngeli za 1, 3, 11, 15, 17 na 18 vinapotangulia mashina yanayoanza kwa vokali za [a], [ɛ], [i], nusu-vokali inaundwa. Mifano ni:

| umbo ndani | | umbo nje | othografia |
|---|---|---|---|
| 1. /mu + alimu/ | → | [mwalimu] | 'mwalimu' |
| /mu +ɛnzi/ | → | [mwɛnzi] | 'mwenzi' |
| /mu + izi/ | → | [mwizi] | 'mwizi' |
| /mu +ɔkɔzi/ | → | [mwɔkɔzi] | 'mwokozi' |
| 3. /mu +ɛzi/ | → | [mwɛzi] | 'mwezi' |
| /mu + aka/ | → | [mwaka] | 'mwaka' |
| /mu + ili/ | → | [mwili] | 'mwili' |
| 11. /u + ajɔ/ | → | [wajɔ] | 'wayo' |
| /u +ɛmbɛ/ | → | [wɛmbɛ] | 'wembe' |
| /u + imbɛ/ | → | [wimbɛ] | 'wimbo' |
| /u +ɔrɔrɔ/ | → | [wɔrɔrɔ] | 'wororo' |
| 15./ku + aŋguka/ | → | [kwaŋguka] | 'kuanguka' |
| /ku +ɛnda/ | → | [kwɛnda] | 'kwenda' |
| /ku + imba/ | → | [kwimba] | 'kuimba' |
| 17. /ku + aŋgavu/ | → | [kwaŋgavu] | 'kuangavu' |
| /ku +ɛmbamba/ | → | [kwɛmbamba] | 'kwembamba' |
| /ku + iŋgi/ | → | [kwiŋgi] | 'kwingi' |
| 18.. /mu + aŋgavu/ | → | [mwaŋgavu] | 'mwangavu' |
| /mu +ɛmbamba/ | → | [mwɛmbamba] | 'mwembamba' |
| /mu + iŋgi/ | → | [mwiŋgi] | 'mwingi' |

Sheria za kifonolojia ni:

$$[+\text{silabi}] \longrightarrow [-\text{silabi}] \,/\, __ \left\{ \begin{array}{l} \overset{V}{\begin{bmatrix} +\text{juu} \\ +\text{mbele} \end{bmatrix}} \\ \overset{V}{\begin{bmatrix} -\text{juu} \\ -\text{chini} \\ +\text{mbele} \end{bmatrix}} \; \varepsilon \\ \overset{V}{\begin{bmatrix} -\text{juu} \\ -\text{chini} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix}} \; ɔ \\ \overset{V}{\begin{bmatrix} +\text{chini} \end{bmatrix}} \; a \end{array} \right\}$$

Sio mazingira yote hudhibiti kuundwa kwa nusu-vokali. Mifano ifuatayo inaonyesha, ama kuundwa, au kutoundwa kwa nusu-vokali.

Mifano ni kama vile:

| Umbo ndani | | umbo nje | | umbo nje | othografia |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. /mu + umba/ | → | [mu:mba] | ~ | [mwumba] | 'muumba' |
| 3./mu +ujiza/ | → | [mu:jiza] | ~ | [mwujiza] | 'muujiza' |
| 18./mu + uŋ guamo/ | → | [muŋ guamo] | ~ | [mwuŋguamɔ] | 'muuguamo |
| 11../u+guzi/ | → | [u:guzi] | ~ | [wuguzi] | 'uuguzi' |
| 17. /ku + uŋ guakɔ/ | → | [kuŋguakɔ] | ~ | [kwuŋ guakɔ] | 'kuunguako' |

Ngeli za 8 na 9 na pronomino za nafsi ya pili, umoja na wingi, {u-} na {wa-} ni mazingira mengine ambayo yanaipa nusu-vokali kuundwa.

Mifano ni :

| Umbo ndani | | Umbo nje | othografia |
|---|---|---|---|
| /vi+a+uŋgua/ | → | [vjauŋgua] | 'vyaungua' |
| /vi + uŋgu/ | → | [vjuŋgu] | 'vyungu' |
| /vi + ura/ | → | [vju ra] | 'vyura' |
| /i + aŋguka/ | → | [jaŋguka] | 'yaanguka' |
| /mu + a + inuka/ | → | [mwainuka] | 'mwainuka' |

Viambishi vya umilikaji huonyesha kuundwa kwa nusu-vokali, kabla ya mashina yanayoanza kwa vokali ya [a], ama [ɛ]. Mifano ni kama katika

| Umbo ndani | | Umbo nje | othografia |
|---|---|---|---|
| 1. /u + aŋgu/ | → | [waŋgu] | 'wangu' |
| /u +ɛtu/ | → | [wɛtu] | 'wetu' |
| 15. /ku + akɔ/ | → | [kwa:kɔ] | 'kwako' |
| /ku +ɛnu/ | → | [kwɛnu] | 'kwenu' |
| 18. /mu + akɛ/ | → | [mwakɛ] | 'mwake' |
| /mu +ɛtu/ | → | [mwɛtu] | 'mwetu' |

Baada ya nusu-vokali kuundwa, vokali inayofuatia inarefushwa.

Viambishi vinginevyo vya umilikaji, vyenye muundo wa /(k) i vinathibiti kuundwa kwa nusu-vokali. /K/ inasimamia konsonanti. Mifano ifuatayo inaonyesha fenomena hii.

| Umbo ndani | | Umbo nje | othografia |
|---|---|---|---|
| /i + aŋgu/ | ⟶ | [jaŋgu] | 'yangu' |
| /i +ɛtu/ | ⟶ | [jɛtu] | 'yetu' |
| /vi + akɔ/ | ⟶ | [vja:kɔ] | 'vyako' |
| /vi +ɛnu/ | ⟶ | [vjɛ:nu] | 'vyenu' |

{ni-} ni kiambishi cha pronomino ya nafsi ya kwanza umoja. Mofimu hii inapotangulia kiambishi cha pronomino ya nafsi ya kwanza wingi {mu-} kisha ikafuatia shina la kitenzi ambalo linaanza kwa mojawapo ya vokali, [a], [ɛ], [i], [ɔ], na [u], moja kwa moja nusu-vokali huundwa. Ni kama katika:

| Umbo ndani | | umbo nje | othografia |
|---|---|---|---|
| /ni + mu + andaɛ/ | ⟶ | [nimwandaɛ] | 'nimuandae' |
| /ni + mu +ɛnd + ɛ+ ɛ/ | ⟶ | [nimwɛndɛ: ] | 'nimwendee' |
| /ni + mu + inuɛ/ | ⟶ | [nimwinuɛ] | 'nimwinue' |
| /ni + muɔndoɛ/ | ⟶ | [nimwɔndɔɛ] | 'nimwondoe' |
| /ni + mu + uguzɛ/ | ⟶ | [nimwuŋguzɛ] | 'nimuuguze' |

Wakati mwingine, kutegemea mazingira, nusu-vokali au huundwa, au isiundwe, kama mifano inavyoonyesha.

| Umbo ndani | | umbo nje | | umbo nje | othografia |
|---|---|---|---|---|---|
| /u + anzɛ/ | ⟶ | [uanzɛ] | ~ | [wanzɛ] | uanze' |
| /u +ɛnɛ+ɛ/ | ⟶ | [uɛnɛ:] | ~ | [wɛnɛ:] | uenee' |
| /u + inukɛ/ | ⟶ | [uinukɛ] | ~ | [winukɛ] | uinuke' |
| /u + ɔkɔtwɛ/ | ⟶ | [uɔkɔtwɛ] | ~ | [wɔkwɔtwɛ] | uokotwe |
| /ku + anza/ | ⟶ | [kuanza] | ~ | [kwanza] | kuanza' |

Sheria tuliyoiandika mwisho inaelekea kuafiki, hata mazingira haya. Kwa hivyo hatukuiandika upya.

Nusu-vokali [j], nayo inaelekea kuundwa katika ngeli ya 4 na ya 8. Mifano ni kama vile:

| Umbo ndani | | umbo nje | othografia |
|---|---|---|---|
| 4. /mi + aka/ | ⟶ | [mja:ka] | 'miaka' |

/mi +: ɛzi / ⟶ [mj ɛzi ] 'miezi'
8. /vi + akula./ ⟶ [vja kula] vyakula'
/vi +ɔɔ/ ⟶ [vjɔ:] vyoo'

Sheria ya kisauti itakuwa:

$$\begin{bmatrix} +\text{ vokali} \\ -\text{ konsonanti} \\ +\text{ silabi} \\ +\text{juu} \end{bmatrix} \rightarrow [-\text{ silabi}] \;/\; \# \begin{bmatrix} +\text{ konsonanti} \\ -\text{ silabi} \end{bmatrix} \text{—+} \begin{bmatrix} \text{V} \\ -\text{juu} \end{bmatrix}$$

2.1.2 UKAKAAISHAJI

Hii ni halia ambayo inaathiri nafasi ya mahali pa kutamkia.

Hii ina maana ya kwamba sauti ambayo katika kutamkwa, inatamkiwa sehemu za nyuma katika mfululizo wa mwahala pa kutamkia, kama vile kaakaa laini; inavutwa mbele zaidi katika mfululizo ule.

Mfano ni kama vile wa K→K^y /-[i], katika lahaja ya Kiswahili ya chijomvu. Bakari (1982:127).

Halia hii si geni katika Kiswahili sanifu. Mfanyiko huu unajitokeza katika ngeli ya 7. Mifano ni kama vile:

| Umbo ndani | umbo kati | umbo nje | othografia |
|---|---|---|---|
| /ki + akula/ ⟶ | /kjakula/ ⟶ | [čakula] | 'chakula' |
| /ki +ɔmbɔ/ ⟶ | /kjɔmbɔ/ ⟶ | [čɔmbɔ] | 'chombo' |
| /ki+ ɛtɛzɔ/ ⟶ | /kjɛtɛzɔ/ ⟶ | [čɛtɛzɔ] | 'chetezo' |
| /ki +ɛti/ ⟶ | /kjɛti/ ⟶ | [čɛti] | 'cheti' |
| /ki + ura/ ⟶ | /kjura/ ⟶ | [čura] | 'chura' |
| /ki + andalua/ ⟶ | /kjandalua ⟶ | [čandalua] | 'chandalua' |

Katika mofimu za umilikaji na vionyeshi vile vile mabadiliko haya yanapatikana. Ni kama vile:

| umbo ndani | umbo kati | umbo nje | othografia |
|---|---|---|---|
| /ki + akɔ/ / ⟶ | /kjakɔ/ ⟶ | [čakɔ] | 'chako' |
| /hi + ki +ɔ/ ⟶ | /hi + kj+ ɔ/ ⟶ | [hičɔ] | 'hicho' |

Katika kueleza mabadiliko hayo kwa kuandika sheria ya kifonolojia, tutasema:

[+nyuma] ⟶ [-nyuma]/ – [-nyuma]

## 2.1.3 KUONDOSHWA KWA VOKALI

Kulingana na Schane (1973), kudondoshwa kwa vokali pia ni katika jumla ya sheria zinazosahilisha muundo wa silabi, au sheria za muundo wa silabi unaopendekezwa.

Mazingira ambayo tunatalii kwanza, ni kuondoshwa kwa vokali kabla ya shina linaloanza kwa konsonanti.

Vokali zinaelekea kudondoshwa wakati ambapo kiambishi cha pronomino ya nafsi ya pili wingi {mu-} inapotangulia mashina yaliyoanza kwa konsonanti.

Katika mazingira haya, vokali inadondoshwa, kisha nasali kupokezwa mkazo. Mifano ambayo tumetoa inathibitisha dai hili, na vile vile kuonyesha vile halia hizi zinavyostahili kufuatana.

| Halia | umbo ndani | umbo nje |
|---|---|---|
| | /mu + gawɛ/ | |
| kudondoshwa kwa vokali | ↓<br>/m + gawɛ/ | |
| Nasali kupokezwa mkazo | ↓<br>/m̩ + gawɛ/ → | [m̩gawɛ<br>mgawe' |
| | /a + mu + hɔŋgɛ/ | |
| kudondoshwa kwa vokali | ↓<br>/a + m + hɔŋgɛ/ | |
| Nasali kupokezwa | \|<br>/a + m̩ + hɔŋgɛ/ → | [am̩hɔŋgɛ]<br>amhonge' |

Kabla hatujaiandika sheria yetu ya kifonolojia, ni muhimu tutaje umuhimu wa jinsi ambayo sheria zinastahili kufuatana, na umuhimu wa sheria zenyewe, kufuatana vile ambavyo zinafuatana. Hooper (1976:53) anasema:

> "Mojawapo ya kaida za kimsingi za fonolojia - zalishi ni kaida ya mpangilio maalum wa sheria za sarufi".6

Tunaweza kuangalia mfano wa kuonyesha umuhimu wa mfuatano wa sheria za kifonolojia. Mfano wenyewe unahusu nasali kupokeza vokali ya /ɔ/, sifa fulani na kisha kudondoshwa.

Schane (1968) anatoa mfano wa aina hii, katika lugha ya Kifaransa. Tunahiari kuonyesha maumbo ya halia hii, kabla hatujaeleza kikamilifu, umuhimu wa mifanyiko kufuatana kwa namna moja, wala si nyingine.

| umbo ndani | umbo nje | maana |
|---|---|---|
| /bɔn/ | | - zuri' |
| ↓ | | |
| /bɔ̃n/ | | |
| ↓ | | |
| /bɔ̃/ ⟶ | [bɔ̃] | |

Kwanza nasali ile [n] inaathiri vokali na kuipa sifa ya aini hii: [~]

(i) $V \rightarrow [+\text{nasali}] \;/\; \underline{\quad} \; [+\text{nasali}]$

Kisha nasali ile inaondoshwa. Ndivyo vile:

(ii) $[+\text{nasali}] \rightarrow \phi \;/\; \underline{\quad} \; [+\text{nasali}]$

Tunachojaribu kusema ni kuwa, sheria (ii), haiwezi kuja, au kutekelezwa, kabla ya sheria (i).

Sababu ni kwamba, ikiwa vokali itakuwa na sifa ile ya [+ nasali], au ya kipua, ni lazima itatokana na athari ya nasali. Kwa hivyo, iwapo sheria (ii) itatangulia sheria (i), nasali itakapodondoshwa, haitakuwa na nafasi ya kuathiri vokali ile, na kwa hivyo, umbo la nje litakuwa si [bɔ̃] kama ilivyo bali [bɔ] na tutakuwa tumepotosha sarufi ya lugha ya Kifaransa; kwa mfuatano wa sheria tu.

Tukirejelea Kiswahili sanifu, katika mifano ile, [mgawɛ.] na [amhɔŋgɛ] ili nasali hizi zipate jukumu la kubeba mkazo, sauti iliyobeba mkazo, hapo awali; ikiwa ni vokali, itastahili idondoshwe kwanza ili nasali zile [m], katika /mgawɛ/ na /amhɔŋgɛ/ ziweze kupokea mkazo na kuwa [m̩].

Sheria za kifonolojia zitashabihiana na hizo za kifaransa. Zikawa:

(i) $\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{konsonanti} \\ +\text{juu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix} \rightarrow \phi \;/\; \begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \\ -\text{silabi} \\ +\text{nasali} \\ +\text{nyuma} \\ +\text{korono} \end{bmatrix} \underline{\qquad} + \begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \\ -\text{silabi} \end{bmatrix}$

(ii) $\begin{bmatrix} +\text{nasali} \\ -\text{silabi} \end{bmatrix} \rightarrow [+\text{silabi}] \;/\; \underline{\quad} + \begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \\ -\text{silabi} \end{bmatrix}$

Kuhusu jumla ya mabadiliko ambayo yanahusu kudondoshwa kwa vokali, kuna mazingira yasiothibiti halia hii, kwa kuwa ya lazima.

Kwa kusema hivi tunamaanisha kwamba vokali huenda ikadondoshwa, au isidondoshwe. Mifano ni kama vile:

| umbo ndani | | umbo nje | | Umbo nje |
|---|---|---|---|---|
| /mu + hɔgɔ/ | ⟶ | [m̩hɔgɔ] | ~ | [muhogo] |
| /mu + hindi/ | ⟶ | [m̩hindi] | ~ | [muhindi] |

Kabla ya viambishi vya kiima, {ni-}, {a-} na {wa-} ambazo ni pronomino za nafsi za; kwanza umoja, nafsi ya tatu umoja na nafsi ya tatu wingi, vokali huelekea kudondoshwa :

| umbo ndani | umbo nje | othografia |
|---|---|---|
| /ni + a + amk + a/ | [na:mka] | 'namka' |
| /a + a + amka/ | [a:mka] | 'aamka' |
| /wa + a + amk + a/ | [wa:mka] | 'waamka' |

Katika ngeli za 3,5 na 18 vokali pia ~~vokali~~ inapotea :

| umbo ndani | umbo nje | othografia |
|---|---|---|
| /mu +ɔ j ɔ/ | [m ɔːjɔ] | 'moyo' |
| /ku + ɔ t ɛ/ | [K ɔːtɛ] | 'kote' |
| /mu +ɔ t ɛ/ | [m ɔːt ɛ] | 'mote' |

Tofauti ambayo inajitokeza katika mazingira haya tuliyoyataja, na mazingira mengineyo ni kwamba baada ya vokali kudondoshwa, vokali inayobakia inarefushwa. Bakari (1982) anapendekeza kwamba kurefushwa huku kwa vokali ni kama aina ya kufidia vokali ile iliyopotea.

Tumeunganisha sheria hizi mbili za kifonolojia, kwa sababu hiyo; tukaziandika kwa pamoja. Inakuwa:

$$\begin{bmatrix} +\text{ silabi} \\ -\text{ konsonanti} \\ +\text{ juu} \\ \alpha\text{ nyuma} \end{bmatrix} \rightarrow \phi \Big/ \# \begin{bmatrix} +\text{ konsonanti} \\ -\text{ silabi} \end{bmatrix} \text{——} + \qquad \begin{bmatrix} +\text{ silabi} \\ -\text{ juu} \\ -\text{ chini} \\ +\text{ nyuma} \\ +\text{ urefu} \end{bmatrix}$$

Tunanuia kutalii vitenzi katika hali ya kukanusha, kama mazingira mengine yanayoipa vokali kudondoshwa. Halia hii inajitokeza kabla ya mofimu ya kukanusha, {ha-}, inapofuatiwa na mashina ya kitenzi yaliyoanza kwa [i], [ɔ], [a] na [ɛ]. Ni kama vile:

/ha + a + imbi/ ⟶ [haimbi] 'haimbi'
/ha + a + ɔni/ ⟶ [haɔni] 'haoni'
/ha + u + amk + i/ ⟶ [huamki] 'huamki'
/ha + u + ɛnd + i/ ⟶ [huɛndi] 'huendi'

Tunaweza kwa kifupi, kusema kuwa vokali za chini zindondoshwa; kabla ya, au zinapotangulia vokali nyinginezo za chini, au za juu. Sifa - bainishi zinaeleza vyema zaidi, kile kinachofanyika. Kwa hivyo tutasema:

$$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{konsonanti} \\ +\text{chini} \end{bmatrix} \longrightarrow \phi \;/\; __ + \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{konsonanti} \\ +\text{chini} \end{bmatrix}$$

na

$$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{konsonanti} \\ +\text{chini} \end{bmatrix} \longrightarrow \phi \;/\; \# \begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \\ -\text{sauti} \\ +\text{mfululizo} \\ +\text{chini} \end{bmatrix} __ + \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{konsonanti} \\ +\text{juu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix}$$

Katika ngeli ya 5, vokali zinadondoshwa kabla ya mashina yanayoanza kwa [a], na [ɛ]. ]. Mifano ni kama:

/ǰi + ambo/ ⟶ [ǰambo] 'jambo'
/ǰi + ɛma/ ⟶ [ǰɛma] 'jema'

Mabadiliko haya yanaonyeshwa na sheria ifuatayo:

$$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ +\text{juu} \\ +\text{mbele} \end{bmatrix} \longrightarrow \phi \;/\; __ + \left\{ \begin{matrix} \underset{[+\text{chini}]}{V} \\ \\ \underset{\begin{bmatrix} -\text{juu} \\ -\text{chini} \\ +\text{mbele} \end{bmatrix}}{V} \end{matrix} \right\}$$

Kuna mazingira ambayo yamethibiti halia - pacha. Kwa maana ya kwamba, vokali haidondoshwi tu, bali inafuatiwa na mabadiliko ya kisauti. Mabadiliko haya si mengine ila kuundwa kwa nusu-vokali.

Mazingira haya ambayo yanaonyesha halia hizi, ni wakati ambapo {ha-}; mofimu ya kukanusha, na {ku-}; mofimu ya kitenzi katika hali iso-ukomo: zinapotangulia mashina ya vitenzi yanayoanzia kwa vokali za [a], [ɛ] na [i].

Mifano ni kama vile:

| umbo ndani | umbo nje | | othografia |
|---|---|---|---|
| /ha + a + ku + amka/→ | [hakuamka] | - [hakwamka] | 'hakuamka' |
| /ha + a + ku + ɛ nda/→ | [hakuɛ nda] | - [hakwenda] | 'hakuenda' |
| /ha + a + ku + iŋgia/→ | [hakuiŋ gia] | - [hakuwiŋ gia] | 'hakuingia' |

Sheria ya kifonolojia ielezayo mabadiliko haya ni:

$$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{konsonanti} \\ +\text{chini} \end{bmatrix} \longrightarrow \phi \;/\; \text{——} \quad \begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ +\text{chini} \end{bmatrix}$$

Kwa hivyo, mazingira yale tuliyoyataja, ya [a], [ɛ], na [i] yanahusu pale nusu-vokali; ikiwa ndicho kiini cha sehemu hii, katika sura hii.

Katika ngeli za 1, 3 na 18, vokali inadondoshwa kabla ya mashina ya maneno yanayoanza kwa konsonanti. Mifano ni kama vile:

(i) /mu + pisi/
(ii) /m + pisi/
(iii) /m̩pisi/ ⟶ [m̩pisi]

(i) /mu + fukɔ /
(ii) /m + fukɔ /
(iii) /m̩fukɔ / ⟶ [m̩fukɔ ]

(i) /mu + lɛ/
↓
(ii) /m + lɛ/
↓
(iii) /m̩ + lɛ/ ⟶ [m̩lɛ]

Katika (i) vokali inadondoshwa, na katika (ii) nasali ikapokezwa mkazo.

Kama tulivyokwishaeleza, mabadiliko haya ni lazima yafuate ruwaza hii, (i) kisha (ii), au tusipate maumbo nje sahihi.

Tukieleza mabadiliko yale kwa sifa za kisauti, tutasema:

$$\begin{bmatrix} +\text{silabi} \\ -\text{konsonanti} \\ +\text{juu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix} \longrightarrow \phi \Big/ __ + \left\{ \begin{matrix} \begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \\ -\text{silabi} \\ -\text{mfululizo} \\ +\text{mbele} \\ -\text{sauti} \end{bmatrix} \\ \begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \\ -\text{silabi} \\ +\text{mfululizo} \\ -\text{stridenti} \\ -\text{sauti} \end{bmatrix} \\ \begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \\ -\text{silabi} \\ -\text{mfululizo} \\ +\text{mbele} \\ +\text{korono} \end{bmatrix} \end{matrix} \right\}$$

$$\begin{bmatrix} +\text{nasali} \\ -\text{silabi} \end{bmatrix} \longrightarrow [+\text{silabi}] \Big/ __ + \left\{ \begin{matrix} \begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \\ -\text{silabi} \\ -\text{mfululizo} \\ +\text{mbele} \\ -\text{sauti} \end{bmatrix} \\ \begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \\ -\text{silabi} \\ +\text{mfululizo} \\ -\text{stridenti} \\ -\text{sauti} \end{bmatrix} \\ \begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \\ -\text{silabi} \\ -\text{mfululizo} \\ +\text{mbele} \\ +\text{korono} \end{bmatrix} \end{matrix} \right\}$$

Mifano mingine katika ngeli ya kwanza ni:

| umbo ndani | | umbo nje | othografia |
|---|---|---|---|
| /mu + sɔ m + aǰi/ | ___ | [m̩sɔ maǰi] | 'msomaji' |
| /mu + sɔ m + i/ | ___ | [m̩sɔmi] | 'msomi' |
| /mu + kal + i/ | ___ | [m̩kazi] | 'mkazi' |
| /mu + zal + i/ | ___ | [m̩zazi] | 'mzazi' |
| /mu + ǰɛŋg + i/ | ___ | [m̩ǰɛnzi] | 'mjenzi' |

Kwa kuwa nadharia ya fonolojia asilia zalishi inatakia maumbo yadhihirishwe, toka umbo ndani, hadi umbo nje, inalazimu kuonyesha mabadiliko muhimu ya kati, yanayopitikia data hii.

| Halia | Umbo ndani | | Umbo nje |
|---|---|---|---|
| | /mu + sɔm + aǰi / | | |
| Kudondoshwa kwa vokali | /m + sɔm + aǰi / | | |
| Nasali kupokezwa mkazo | /m̩ + sɔm + aǰi / | ⟶ | [m̩sɔ maji] 'msomaji' |
| | /mu + sɔm + i / | | |
| Kudondoshwa kwa vokali | /m + sɔm + i / | | |
| Nasali kupokezwa mkazo | /m̩ + sɔm + i / | ⟶ | [m̩sɔmi] 'msomi' |
| | /mu + kal + i / | | |
| Kudondoshwa kwa vokali | /m + kal + i / | | |
| Nasali kupokezwa mkazo | /m̩ + kal + i / | | |
| Kukazana kwa sauti | /m̩ + kaz + i / | ⟶ | [m̩kazi] 'mkazi' |

account for & explain

| | | | |
|---|---|---|---|
| | /mu + zal + i / | | |
| Kudondoshwa kwa vokali | /m + zal + i / | | |
| Nasali kupokezwa mkazo | /m̩ + zal + i / | | |
| Kukazana kwa sauti | /m̩ + zaz + i / | ⟶ | [m̩zazi] 'mzazi' |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | /mu + ǰεŋgi / | | |
| Kudondoshwa kwa vokali | /m + ǰεŋgi / | | |
| Nasali kupokezwa mkazo | /m̩ + ǰεŋgi / | | |
| Kukazana kwa sauti | /m̩ + ǰε nz + i / | ⟶ | [m̩ǰε nzi] 'mjenzi' |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | /mu + + čεk + i / | | |
| Kudondoshwa kwa vokali | /m + + čεk + i / | | |
| Nasali kupokezwa mkazo | /m̩ + + čεk + i / | | |
| Kukazana kwa sauti | /m̩ + čεš + i / | ⟶ | [m̩čεši] 'mcheshi' |

Mtaala wa halia hii hautupi kuepuka kueleza dhana za sheria ambazo ni lazima zifuatane kwa ruwaza fulani, na zile ambazo si lazima zifuatane kwa ruwaza maalum.

Kama inavyoonekana, ni lazima vokali idondoshwe kwanza, ili pawe na haja ya sauti nyingineyo kubeba mkazo ule uliokuwa umebebwa na vokali.

Hatuwezi kupokeza nasali mkazo ambao umebebwa na vokali, kwani haijadondoshwa.

Lakini, halia kama kukazana na kudhoofika kwa sauti, katika [m̩kazi], [m̩zazi], na [m̩jεnzi]; na kwa upande wake,[msɔmi]au zaweza kuja mwanzo wa mabadiliko yale, kabla ya kudondoshwa kwa vokali na kupokezwa mkazo; ama yaje mwisho baada ya kudondoshwa kwa vokali na nasali kupokezwa mkazo bila ya kuathiri umbo sahihi la nje, hata kidogo.

Miktadha hii inaelekea kuafiki yale anayosema Hooper (1976:54) na (1976:55), kuhusu mfuatano wa sheria za kifonolojia.

Anasema:

> "Mpangilio wa kuelekezana ni mpangilio maalum. Sheria ya A, inasemekana kuelekeza sheria ya B, katika uwezekano wa sheria ya A kuundia sheria ya B mazingira ya kutekelezwa."[7]

Anaeleza zaidi katika (1976:55):

> "Katika sheria ambazo zinatekelezwa kwa pamoja, sheria zote hutekelezwa kwa maumbo ya ndani, kwa njia ya moja kwa moja. Lakini katika aina ya sheria ambazo zinatekelezwa kwa ruwaza (au mfuatano) maalum, sheria moja hutekelezwa kwa matokeo ya umbo nje la sheria nyingine."8
>
> (mabano ni yetu).

Vokali hudondoshwa pia katika mazingira ya mofimu za vionyeshi, katika ngeli za1, 2, 5, 6, 10, 15, 16, 17, na 18. Tumetoa mifano kuthibiti maoni haya.

| umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| 1. /hu+jɔ/ | ⟶ | [hujɔ] | 'huyo' |
| 2. /ha+ɔ/ | ⟶ | [haɔ] | 'hao' |
| 3. /hu+ɔ/ | ⟶ | [huɔ] | 'huo' |
| 11. /hu+ɔ/ | ⟶ | [huɔ] | 'huo' |
| 5. /hilɔ/ | ⟶ | [hilɔ] | 'hilo' |
| 6. /hajɔ/ | ⟶ | [hajɔ] | 'hayo' |
| 10. /hizɔ/ | ⟶ | [hizɔ] | 'hizo' |
| 15. /hukɔ/ | ⟶ | [hukɔ] | 'huko' |
| 17. /hu+kɔ/ | ⟶ | [hukɔ] | 'huko' |
| 16. /hapɔ/ | ⟶ | [hapɔ] | 'hapo' |
| 18. /hu+mɔ/ | ⟶ | [humɔ] | 'humo' |

Tunapata vokali zikidondoshwa katika mazingira ya kiambisho cha kiima, mofimu ya aspekti, na shina la kitenzi. Mifano ni kama vile:

| umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /mu+ na+ɔta / | ⟶ | [m̩naɔta ] | 'mnaota' |
| /mu+ na+čɛza / | ⟶ | [m̩načɛ:za ] | 'mnacheza' |
| /mu+ŋgɛ+ɛ:nda / | ⟶ | [m̩ŋgɛ:nda ] | 'mngeenda' |
| /mu+ ta + ɔna / | ⟶ | [m̩taɔna ] | 'mtaona' |
| /mu+ ta+sɔma / | ⟶ | [m̩tasɔ: ma ] | 'mtasoma' |

Tunashuhudia vokali ikipotea pia kabla ya mofimu ya wakati uliopo, katika ngeli za 5, na 10. Mifano ni kama vile:

| | | |
|---|---|---|
| /mu + čɛz + a#ŋgɔma/ → [m̩čɛzaŋgɔma] | | 'mcheza ngoma' |
| /mu + čɛz + a#baɔ/ → [m̩čɛzabao ] | | 'mcheza bao' |

Ngeli

| | | |
|---|---|---|
| 5. /li + a+inama / → | [lainama] | 'lainama' |
| 10./zi + a+ɛnɛa / → | [zaɛnɛa] | 'zaenea' |

## 2.2.0 SHERIA ZA UWIANO.

Katika sheria za aina hii, sauti moja huathiri sauti nyingine kwa sifa fulani. Huenda ikawa ni urefu, au sifa ya [+] ama ya [-] mbele, kwa vokali.

Aidha, halia za uwiano ni nyingi. Chambilecho Schane (1973:207):

> "Zipo sheria nyingi asilia za uwiano. Vokali huathiriwa kwa sifa ya kipua zinapopakana na konsonanti ambazo ni za kipua; sauti za mtuo zinakubaliana kwa sifa ya ughuna na sauti zilizopakana nazo za mtuo; sauti za mtuo zinakuwa ghuna ziwapo katikati ya vokali kwani vokali huwa ghuna kwa jumla; nasali zinaathiriwa kuhusu mahali pa kutamkia na sauti za mtuo zinazozifuatia; konsonanti zinazotamkiwa kaakaa laini zinavutwa, kutamkiwa katika kaakaa ngumu kabla ya vokali za sifa ya umbele; vokali zinavutwa mbele na vokali ya sifa ya umbele; vokali zinakubaliana kiurefu, unyuma, au umviringo na vokali nyinginezo (mifano ya mkubaliano wa vokali), na kadhalika."[9]

## 2.2.1 MVUTANO WA VOKALI


Vokali zinapoathiriana kwa sifa ya urefu, zinasemekana kuwa zimevutana.

Mabadiliko yanapatikana wakati ambapo vokali za kiambishi cha ngeli /a/ zinavutana kiurefu na vokali za sifa ya shina la nomino.

Mifano ya mabadiliko haya yanapatikana katika ngeli za 2, 6 na 16. Kama vile:

| umbo ndani | umbo nje | othografia |
|---|---|---|
| /wa + ɛŋgi / → | [wɛŋgi ] | 'wengi' |
| /wa + ɛzi / → | [wɛzi ] | 'wezi' |
| /ma + ikɔ / → | [mɛkɔ ] | 'meko' |
| /ma + inɔ / → | [mɛnɔ ] | 'meno' |
| /ma + iŋginɛ / → | [mɛŋginɛ ] | 'mengine' |
| /pa + iŋginɛ/ → | [pɛŋginɛ ] | 'pengine' |
| /pa + iŋgi / → | [pɛŋgi ] | 'pengi' |

Bakari (1982:73) anaelekea kueleza mantiki ya kudai kuwa vokali hizi zinavutana. Mchoro unaofuatia ni mwangwi wa yale aliyoyatoa kimaelezo.




Vokali ambayo ni ya chini [a], na [i], ikiwa ni vokali ya juu, huathiriana, au huvutana, matokeo yakawa vokali ya kati au :

| V | | V | | V |
|---|---|---|---|---|
| [+ juu, + mbele] | + | [+ chini] | ⟶ | [- juu, - chini] |

Sheria ya kisauti itakuwa:

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| [+ silabi, - konsonanti, + chini] | + | [+ vokali, - konsonanti, + juu, - chini] | → | [- juu, - chini] | / # | [+ konsonanti, - vokali] ——— . |

Mifano mingine inayohusu vokali tofauti, [a] na [ɛ] ni kama vile:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /wa + ɛnzi:/ | ⟶ | [wɛnzi:] | 'wenzi' |
| /wa + ɛɲɛwɛ/ | ⟶ | [wɛɲɛwɛ] | 'wenyewe' |
| /ma + ɛma/ | ⟶ | [mɛma] | 'mema' |
| /pa + ɛmbamba/ | ⟶ | [wɛmbamba] | 'wembamba' |

Mofimu hizi zinajitokeza kuwa 2, 6, na 16.
Sheria ya kifonolojia ambayo inaelezea halia hii ni:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| [+ usilabi, α chini, - nyuma] | ⟶ | [- juu, α- nyuma] | / —+ | [+ usilabi, α juu, - chini, α nyuma] |

## 2.2.2 MKUBALIANO WA VOKALI

Kwa kawaida, au katika lahaja nyingi za Kiswahili kama vile Chichifundi, Chijomvu, Kisiu na Kimvita, katika kunyambua vitenzi vokali ambayo ipo katika mzizi, ndiyo inayoathiri vokali iliyo katika kiambishi cha kunyambua.

Katika Kiswahili sanifu vile vile, vokali ambayo inapatikana katika mzizi wa kitenzi ndiyo inayoathiri vokali iliyo katika kiambishi cha kunyambua kitenzi kile.

Kwa hivyo, vokali ambazo zinakubaliana; au kwa sifa ya urefu, au kuwa mbele, au nyuma ni zile za mzizi wa kitenzi na za kiambishi.

Mifano ni kama vile:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ib + i + a / | ⟶ | [ibia] | 'ibia' |
| /um + i + a / | ⟶ | [umia] | 'umia' |
| /kat + i + a / | ⟶ | [katia] | 'katia' |
| /sɔm + ɛ + a / | ⟶ | [sɔmɛa] | 'somea' |
| /ɛnd + ɛ + a / | ⟶ | [ɛndɛa] | 'endea' |

Katika hali ya kufanyisha, tunapata :

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ib + iš + a / | ⟶ | [ibiša] | 'ibisha' |
| /um + iš + a / | ⟶ | [umiša] | 'umisha' |
| /kat + iš + a / | ⟶ | [katiša] | 'katisha' |
| /sɔm + ɛš + a / | ⟶ | [sɔmɛša] | 'somesha' |
| /ɛnd + ɛš + a / | ⟶ | [ɛndɛša] | 'endesha' |

Vitenzi vinanyambuliwa pia, katika hali ya kufanyika. Mifano ni kama vile:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ib + ik + a / | ⟶ | [ibika] | 'ibika' |
| /um + ik + a / | ⟶ | [umika] | 'umika' |
| /kat + ik + a / | ⟶ | [katika] | 'katika' |
| /sɔm + ɛk + a / | ⟶ | [sɔmɛka | 'someka' |
| /ɛnd + ɛk + a / | ⟶ | [ɛndɛka] | 'endeka' |

Katika sheria za kifonolojia, tunaweza kusema kuwa:

$$\begin{bmatrix}-\text{ chini}\end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix}\alpha\text{ juu}\end{bmatrix} \Big/ \begin{bmatrix}[\alpha\text{ juu}] \\ -\text{ chini}\end{bmatrix} K ____$$

mnyambuliko [mzizi]

Mifano mingineyo inajitokeza katika hali ya kutendeana {an-} kama vile

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ib + an + a / | ⟶ | [ibiana] | 'ibiana' |
| /um + i + an + a/ | ⟶ | [umiana] | 'umiana' |
| /sɔm + ɛ + an + a/ | ⟶ | [sɔmɛana] | 'someana' |

Jinsi ya kutendana pia yatupa mifano. Ni kama vile:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ib + an + a / | ⟶ | [ibana] | 'ibana' |
| /um + an + a / | ⟶ | [umana] | 'umana' |
| /sɔm + an + a / | ⟶ | [sɔmana] | 'somana' |

Tunapochanganya hali ya kusababisha na hali ya kutendana tunapata:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ib + iš + an + a / | ⟶ | [ibišana] | 'ibishana' |
| /um + iš + an + a / | ⟶ | [umišana] | 'umishana' |
| /sɔm + ɛš + an + a / | ⟶ | [sɔmɛšana] | 'someshana' |

Katika kauli ya kufanyia, na ya kutendewa, vipo vitenzi:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ib + i + w + a / | ⟶ | [ibiwa ] | 'ibiwa' |
| /um + i + w + a / | ⟶ | [umiwa ] | 'umiwa' |
| /sɔm + ɛ + w + a / | ⟶ | [sɔmɛwa] | 'somewa' |

Tunaweza pia kuchanganya hali ya kusababisha, na kauli ya kutendewa. Mifano kama vile:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ib + iš + w + a / | ⟶ | [ibišwa ] | 'ibishwa' |
| /sɔm + ɛš + w + a / | ⟶ | [sɔmɛšwa] | 'someshwa' |

Katika hali ya kufanyua, pamoja na hali ya kufanyika, tunapata mifano kama vile

| | | | |
|---|---|---|---|
| /lipu + k + a/ | ⟶ | [lipuka] | 'lipuka' |
| /čɔm + ok + a/ | ⟶ | [čomoka] | 'chomoka' |
| /šik + am + a/ | ⟶ | [šikama] | 'shikama' |
| /fuŋg + am + a/ | ⟶ | [fuŋ gama] | 'fungama' |

## 2.2..3 KUATHIRIWA KWA NASALI KUHUSU MAHALI PA KUTAMKIA

Katika Kiswahili sanifu, kunayo majina katika ngeli ya tisa, ambayo yanaonyesha athari fulani katika mofimu inayowakilisha ngeli ya 9 nayo ni fonimu jumuishi /N-/.

Mofimu hii, ambayo ni nasali bila shaka, inaathiriwa na sauti iliyoanzia shina la jina, hasa konsonanti ghuna, na zisizo - ghuna. Mifano ambayo tumeitoa inathibiti hali hii ya mambo.

| | | |
|---|---|---|
| /n + bɛgu/ | [mbɛgu] | 'mbegu' |
| /n + vua/ | [ɱvua] | 'mvua' |
| /n + dɔgɔ/ | [ndɔgɔ] | 'ndogo' |
| /n + ǰia/ | [ɲǰia] | 'njia' |
| /n + gumu/ | [ŋgumu] | 'ngumu' |
| /n + vi/ | [ɱvi] | 'mvi' |
| /n + ta/ | [nta] | 'nta' |
| /n + či/ | [n̪či] | 'nchi' |
| /n + gwɛ/ | [ŋgwɛ] | 'ngwe' |

Sheria ya kisauti ambayo inaonyesha hali hii ni:

$$[+\text{nasali}] \longrightarrow [\alpha\ \text{mahali}] \ / \ \# ___ + \begin{bmatrix} +\ \text{konsonanti} \\ -\ \text{silabi} \\ \alpha\ \text{mahali} \end{bmatrix}$$

## 2.3.0 SHERIA ZA KUDHOOFIKA KWA SAUTI

Katika isimu sauti husemekana kuwa dhaifu, au dhabiti, kulingana na ruwaza bia ya udhabiti wa sauti.

Hooper (1976:206) anatoa mfuatano wa sauti, kuanzia na zile dhaifu, kuelekea upande mmoja, kulingana na vile zinaendelea kukazana.

Mfuatano huu ni:

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
|---|---|---|---|---|---|
| [nusu - vokali] | [vilainisho] | [nasali] | [+ mfululizo, + sauti] | [+ mfululizo, - sauti] | [+ mtuo, - sauti] |

1 - [nusu vokali]
2 - [vilainisho]
3 - [nasali]
4 - [+ mfululizo / + sauti]
5 - [+ mfululizo / - sauti]
6 - [+ mtuo / - sauti]

Kutoka 1 kuelekea 6, ni kukazana kwa sauti. Kutoka 6 kuteremka hadi 1, ni kudhoofika kwa sauti.

Tukizingatia mazingira mbalimbali ya nomino, katika Kiswahili sanifu, tunapata mifano ya kudhoofika kwa sauti. Mifano ni kama vile:

(i) /mu + ǰɛŋg + i /
(ii) /m + ǰɛŋg + i /
(iii) /m̩ + ǰɛŋg + i /
(iv) /m̩ + ǰɛnz + i /
(v) /m̩ + ǰɛnz + i / ⟶ [m̩jɛnzi] 'mjenzi'

/mu + fuat + i /
/m + fuat + i /
/m̩ + fuat + i /
/m̩ + fuas + i /
/m̩ + fuas + i / ⟶ [m̩fuasi] 'mfuasi'

Katika mifano yote hii, (i) ni umbo la ndani. (ii) ni kukazana kwa sauti; (iii) ni kudondoshwa kwa vokali, (iv); nasali inapokezwa sifa ya [+ silabi].

Kabla hatujaendelea na mifano, tunataka tueleze kuwa mifano yote ya (i) nomino, zimetokana na vitenzi. `mjenzi' linatokana na kitenzi cha `kujenga'; `mfuasi' linatokana na kitenzi cha `kufuata'; `mcheshi' na `kucheka'; `mpishi' linatokana na `kupika' na `mpenzi' linatokana na `kupenda'.

Tunaendelea na mifano ile ya kudhoofika kwa sauti, ambapo tunapata;

/mu + čɛk + i /

| | | | |
|---|---|---|---|
| /m + č ɛ k + i / | | | |
| /m̩ + č ɛ k + i / | | | |
| /m̩ + č ɛ š + i / | | | |
| /m̩ + č ɛ š + i / | ⟶ | [m̩ č ɛ š i ] | 'mcheshi' |
| /mu + p i k + i / | | | |
| /m + p i k + i / | | | |
| /m̩ + p i k + i / | | | |
| /m̩ + p i š + i / | | | |
| /m̩ + p i š + i / | ⟶ | [m̩ p i š i ] | 'mpishi' |
| /mu + ǰ ɛ ŋ g + i / | | | |
| /m + ǰ ɛ ŋ g + i / | | | |
| /m̩ + ǰ ɛ ŋ g + i / | | | |
| /m̩ + ǰ ɛ n z + i / | | | |
| /m̩ + ǰ ɛ n z + i / | ⟶ | [m̩ǰ ɛ nzi] | 'mjenzi' |
| /mu + p ɛ n d + i / | | | |
| /m + p ɛ n d + i / | | | |
| /m̩ + p ɛ n d + i / | | | |
| /m̩ + p ɛ n z + i / | | | |
| /m̩ + p ɛ n z + i / | ⟶ | [m̩p ɛ nzi] | 'mpenzi' |

Kwa muhtasari, kabla hatujaandika sheria ya kifonolojia tunaweza kusema kuwa:

/k/ ⟶ [š]
/ǰ/ ⟶ [z] au
/d/ ⟶ [z]

$$\begin{bmatrix} k \\ \check{j} \\ d \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} \check{s} \\ z \\ z \end{bmatrix} \Big/ \; - \; v$$

katika mazingira ambayo tutaeleza vyema.

Kabla ya kufanya hivyo, jambo la kuvutia sana ni jinsi maumbo hayo ya ndani yanavyoibuka hadi maumbo hayo ya nje. Inaonekana wazi kabisa kuwa mpangilio wa halia za kifonolojia ambazo zinajitokeza zina mfuatano maalum. Kwanza ni sauti ya mtuo ambayo inabadilika na kuwa ya mkwaruzo. Kisha vokali ya kiambisho ikapotea, ndipo nasali ipokezwe mkazo.

Ikiwa tutamnukuu Bakari (1982:14) anaelekea kueleza:

"Sheria za mabadiliko ya kati zinatuwezesha kuhusisha faridi za kileksia ambazo zingejitokeza kwa njia tofauti kwa sababu ya maumbo yake ya nje."[11]

Sheria hizi ni muhimu kwa mifano kuliyoitoa katika ngeli ya 1, katika kuzipa mofimu maumbo yake kamili, katika umbo ndani ili kuweza kuelewa vile inavyokuwa, hata yakafikiwa matokeo ya umbo nje. Ni kama anavyosema Hooper (1976:54) kuwa:

"Sheria zinafuata mpangilio maalum ikiwa cha kufikiriwa tu katika kuamua zitafuatana lini na wapi ni miundo ya umbo nje."[12]

Sheria za mabadiliko haya ni:

$$[-\text{mfululizo}] \longrightarrow [+\text{mfululizo}] \quad \text{v} __ \text{v}$$

$$\begin{bmatrix}-\text{konsonanti}\\+\text{vokali}\end{bmatrix} \longrightarrow \phi \ / \ __ \begin{bmatrix}+\text{nasali}\\-\text{koroni}\\+\text{antiria}\end{bmatrix}$$

$$\begin{bmatrix}+\text{nasali}\\-\text{silabi}\end{bmatrix} \longrightarrow [+\text{silabi}] \ / \ __ + \begin{bmatrix}+\text{juu}\\+\text{mbele}\end{bmatrix}$$

Sheria hizi zinafuatana kwa mpangilio huu.

Katika kundi hili la mabadiliko ya kudhoofika kwa sauti, kuna halia ya kisauti, ya /j/ [š]. Mifano ifuatayo inaonyesha tukio hili.

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ruk + j + a/ | ⟶ | [ruša] | 'rusha' |
| /čɛk + j + a/ | ⟶ | [čɛša] | 'chesha' |
| /pit + j + a/ | ⟶ | [piša] | 'pisha' |

Pia /g/ ⟶ [ž] kama katika:

/mu + lim + ag + i/
/mu + lim + aǰ + i/
/m + lim + aǰ + i/
/m̩ + lim + aǰ + i/ ⟶ [m̩limaǰi] 'mlimaji'

/mu + ɟug + agi/
/mu + ɟug + aǰi/

/m + ɸug + aɟi /

/m̩ + ɸug + aɟi / ⟶ [m̩fugaji] 'mfugaji'

Sauti ya mtuo ya /k/ pia huwa [f] ambayo ni sauti ya mkwaruzo.

/u + tukut + u/

/u + tukuɸ + u/ ⟶ [utukuɸu]

Sheria ya kisauti ya kuonyesha halia hii ni:

$$\begin{bmatrix} + \text{ konsonanti} \\ - \text{ silabi} \\ + \text{ juu} \\ - \text{ mfululizo} \\ - \text{ antiria} \\ - \text{ korono} \\ - \text{ sauti} \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} - \text{ juu} \\ - \text{ nyuma} \\ + \text{ mfululizo} \\ + \text{ mbele} \\ + \text{ stridenti} \end{bmatrix} / __ + \begin{bmatrix} + \text{ silabi} \\ - \text{ konsonanti} \\ + \text{ juu} \\ + \text{ nyuma} \end{bmatrix}$$

strengthening

## 2.4.0 SHERIA ZA KUKAZANA KWA SAUTI

Kinyume cha kudhoofika kwa sauti katika isimu: sauti ya kilainisho inapobadilika na kuwa ya mkwaruzo, sauti hiyo husemekana kuwa imekazana. Tunaweza kuzingatia mifano kadha, kuuthibiti ukweli huu.

| | | | |
|---|---|---|---|
| /m + kaz + i / | ⟶ | [m̩kazi] | 'mkazi' |
| /m + lɛl + i / | ⟶ | [m̩lɛzi] | 'mlezi' |
| /ɸ + val + i / | ⟶ | [vazi] | 'vazi' |
| /m + zal + i / | ⟶ | [m̩zazi] | 'mzazi' |
| /ma + lal + i / | ⟶ | [malazi] | 'malazi' |

Kwa hivyo, katika /l/→[z] tunaweza kuandika sheria ya kifonolojia:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| + konsonanti<br>- silabi<br>+ sonoranti<br>- latero<br>- korono | ⟶ | [+ mfululizo] | / — + | + silabi<br>- konsonanti<br>+ juu<br>- nyuma |

Sauti hiyo hiyo ya /l/ huweza pia kuwa [v], katika mazingira tofauti. Mifano ni kama vile:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /u + tulil + u / | ⟶ | [utulivu] | 'utulivu' |
| /u + ɔkɔl + u / | ⟶ | [wɔkɔvu] | 'wokovu' |

Sheria inayoeleza halia hii ni: ↗ hakuna sheria?

| | | | |
|---|---|---|---|
| /n + limi / | ⟶ | [ndimi] | 'ndimi' |
| /n + rɛfu/ | ⟶ | [ndɛfu] | 'ndefu' |
| /n + lɔa / | ⟶ | [ndɔa ] | 'ndoa' |
| /n + wili / | ⟶ | [mbili ] | 'mbili' |
| /n + wati/ | ⟶ | [mbati ] | 'mbati' |
| /n + lɔta/ | ⟶ | [ndɔtɔ] | 'ndoto' |

/l/ pia huwa [d]. Mazingira yanayoonyesha kutokea kwa halia hii ni :

| Umbo ndani | | Umbo nje | othografia |
|---|---|---|---|
| /N + limi/ | ⟶ | [ndimi] | 'ndimi' |
| /N + refu/ | ⟶ | [ndefu] | 'ndefu' |
| /N + loa/ | ⟶ | [ndɔa] | 'ndoa' |
| /N + wili/ | ⟶ | [mbili] | 'mbili' |
| /N + wati/ | ⟶ | [mbati] | 'mbati' |
| /N + lota/ | ⟶ | [ndɔtɔ] | 'ndoto' |

Tukijumisha hali hizi, tutasema;

$$\begin{bmatrix} l \\ l \\ r \\ w \\ l \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} z \\ d \\ d \\ b \\ v \end{bmatrix}$$

Kuhusu /r/→[d] na /w/→ [b], tunaweza kusema, katika sheria ya kifonolojia:

$$\begin{bmatrix} + \text{ konsonanti} \\ - \text{ silabi} \end{bmatrix} \longrightarrow [- \text{ mfululizo}] \quad / \; \text{—} + \begin{bmatrix} + \text{ silabi} \\ - \text{ konsonanti} \\ + \text{ juu} \\ - \text{ nyuma} \end{bmatrix}$$

## 2.5.0 HITIMISHO

Tunaweza kusema kuwa Kiswahili sanifu kimethibiti rutuba yake, panapohusu halia za kifonolojia.

Chini ya sehemu za 2.1.0, 2.1.1., 2.1.2, 2.1.3; 2.2.0, 2.2.1, 2.2.2; 2.3.0 na 2.4.0 tumeyaonyesha haya, pamoja na kuyatolea mifano.

Isipokuwa halia ya kuathirika kwa nasali, ambayo imejitokeza kama sheria ya kifonolojia, halia za; kuundwa kwa nusu-vokali, kudondoshwa kwa vokali, ukaaishaji, uwiano kwa urefu, mkubaliano wa vokali, kudhoofika, na kukazana kwa sauti, zote zimejitokeza kuwa halia za kimofofonolojia.

Ithibati hizi, zimethibitisha haipothesia yetu, kuwa mabadiliko haya ya kisauti yanapatikana katika Kiswahili sanifu, kwani yakiwa bia na yakipatikana katika lugha nyingine za kibinadam, kama vile Kikikuyu.

TANBIHI

1. J.B. Hooper, (1976): An Introduction to Natural Generative Phonology. New York Academic Press. 3.
2. ——————————, (opp., cit): ix
3. S.A. Schane, (1973): "Natural Rules in Phonology", katika Robert P. Stockwell and Ronald K.S. Macaulay, (eds) Linguistic change and Generative Theory. Bloomington. Indiana University Press. 207
4. (opp. cit). 206
5. J.B. Hooper, (opp cit). 195
6. ————————, (opp. cit). 53
7. ————————, (opp cit). 54
8. ————————, (opp.cit). 55
9. S.A. Schane, (opp. cit). 207
10. J. B. Hooper, (opp. cit). 206
11. M. Bakari, (1982) The Morphophonology of the Kenyan Swahili Dialects. Ph.D Thesis. University of Nairobi. 14.

12. J.B. Hooper, (opp. cit). 54

## SURA YA TATU

## UTANGULIZI

Ni madhumuni yetu kuonyesha halia au mifanyiko ya kisauti, ambayo inadhihirika katika Kikikuyu sanifu katika sura hii.

Mifanyiko hiyo haijajitokeza kuwa tofauti na ile iliyopo katika Kikikuyu cha Kabete.

Kwa hivyo tutaonyesha pia katika kiwango cha fonolojia, kuwa Kikikuyu cha Kabete ni sawa na Kikikuyu sanifu.

### 3.1.0. SHERIA ZA MUUNDO WA SILABI UNAOPENDEKEZWA

Kama tulivyoeleza katika 2.0.0, sheria za muundo wa silabi unaopendekezwa ni katika sheria za kisauti ambazo husahilisha muundo wa silabi katika lugha. Ijapokuwa,tunakumbushwa kuwa sio halia zote za kisauti huleta muundo sahili zaidi wa silabi. Kama anavyosema Schane (1973: 208):

> "Sio sheria zote asilia za muundo wa silabi unaopendekezwa huleta muundo wa konsonanti vokali: konsonanti vokali"[1]

Kinaya chake ni kuwa mifanyiko fulani ya kisauti huweza kuleta miundo changamano zaidi ya silabi, katika lugha.

### 3.1.1. KUUNDWA KWA NUSU-VOKALI

Nusu-vokali inathibiti kuundwa katika mazingira mbali mbali katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete.

Katika ngeli ya 1 {mo}, mifano kadha ya kuundwa kwa [w] inajitokeza.

| Umbo ndani | | Umbo nje | Maana |
|---|---|---|---|
| /mo + ana/ | ⟶ | [mwana] | Mtoto |
| /mo + ere/ | ⟶ | [mwere] | Mwili |
| /mo + ɛnɛ/ | ⟶ | [mwene] | Mwenyewe |
| /mo + isi/ | ⟶ | [mwoisi] | Mwizi |
| /mo + iru/ | ⟶ | [mwoiru] | 'mke- mwenza' |
| /mo + ehia/ | ⟶ | [mwehia] | mwenye-dhambi |
| /mo + ɔi/ | ⟶ | [mwoi] | mwenye kuchukua |
| /mo + itani/ | ⟶ | [mwoitani] | anayenyonga |

| | | | |
|---|---|---|---|
| /mo + ini/ | ⟶ | [mwoini] | mwimbaji |
| /mo + iretu/ | ⟶ | [mwoiretu] | msichana |
| /mo + anake/ | ⟶ | [mwanake] | mvulana |

[ + silabi ] ⟶ [ - silabi ] / v - v.

au

[ + silabi ] ⟶ [ - silabi ] / — [+ kinsonanti, - vokali]

Katika ngeli ya 3 ambayo ni {mu-} ama {mo-}, na ngeli ya 4, {me-} nusu-vokali, [j], inaundwa. Mifano ni kama vile:-

| Umbo ndani | | Umbo nje | Maana |
|---|---|---|---|
| /mu +ɔjɔ/ | ⟶ | [mwɔjɔ] | 'roho' |
| /mo + eri/ | ⟶ | [mweri] | mwezi |
| /me +ɔjɔ/ | ⟶ | [mjɔjɔ] | mioyo |
| /me + eri/ | ⟶ | [mjeri] | 'miezi' |

Hali ya kurefushwa kwa vokali inyofuatia nusu-vokali ni jambo ambalo linajitokeza sio tu katika Kikikuyu cha Kabete, bali pia katika Kikikuyu sanifu, na lahaja nyinginezo zaKiswahili.

Mazingira mengineyo yanayothibiti kuundwa kwa nusu-vokali ni katika ngeli ya 14 {ko-}. Mifano ni kama vile:

| Umbo ndani | | Umbo nje | Maana |
|---|---|---|---|
| /ko +ɔhɔra/ | ⟶ | [kwɔhɔra] | kufungua |
| /ko +ɔja/ | ⟶ | [kwɔja] | kuchukua |
| /ko + aɣera/ | ⟶ | [kwaɣera] | 'kuwa |
| /ko +ɔhɔra/ | ⟶ | [kwɔhɔra] | kuondoka |
| /ko + aria/ | ⟶ | [kwaria] | kuongea |

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ko + e + ita/ | ⟶ | [kweita] | kujinyonga |
| /ko + e + -h-ria/ | ⟶ | [kwe:jɛhɛria] lawama' | kujiepushia lawama |
| /ko + e + adeka/ | ⟶ | [kwe:ja:deka] | kujiandika |
| /ko + e + ru-e:ra/ | ⟶ | [kwe:ru:ɣe:ra] | kujipikia |
| /ko + e + -a:era/ | ⟶ | [kweɣa:era] | kujipakulia |

Kuna mfanyiko mwingine ambao unajitokeza katika ngeli hii hii ya 14, pamoja na nusu-vokali ile kuundwa,. Iwapo kiima cha kitenzi ni pronomino ya nafsi ya kwanza umoja: {e-}, konsonanti moja ya mofimu ya ngeli ya 14, {ko-} inapata sifa ya kuwa [+ ghuna]. Mifano ni kama vile:

| Umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /ko + e + tea/ | ⟶ | [gwetea] | kujishaua' |
| /ko + e + tɛma/ | ⟶ | [gwetɛma] | kujikata' |
| /ko +e + šɔkia/ | ⟶ | [gwešɔkia] | kujilalamikia' |
| /ko + e tu:era/ | ⟶ | [gwetwera] | kujiamulia' |
| /ko + e +ɣo:kia/ | ⟶ | [gweɣokia] | kujiharibu' |

Lakini, mazingira ambayo yanafanya /k/ kuwa /g/ yamejipekeesha. Tunasema hivyo kwa sababu ipo mifano isiyoonyesha fenomena hii kutokea. Ni kama vile:

| (iv) umbo ndani | umbo nje | maana |
|---|---|---|
| /ko + e + ita/ | [kwe :ita] | kujinyonga' |
| /ko + e + gaera | [kwe:gaera] | kujigawia' |

Sheria zetu za kuundwa kwa nusu - vokali, na kupata sifa ya ughuna zitakuwa:

(i)[+ silabi] ⟶ [-silabi] / — [+ mbele, − juu, − chini]

(ii) [− ughuna] ⟶ [+ ughuna]

Kuundwa kwa nusu-vokali kunaelekea kutaladhadhi katika mazingira fulani, ambapo nusu-vokali zote mbili, [w], na [j] zinaundwa sawia, au, pamoja katika ngeli ya 14. Lakini katika mazingira ambayo mofimu ya kiima ni pronomino ya nafsi ya kwanza umoja {e-}, na

inapotangulia kiini cha kitenzi.- Mifano yetu inaonyesha kwa uwazi zaidi, halia hizi za pamoja.

| umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /ko + e + eɔhɔra/ | → | [kwejɔhɔra] | kujitanzua |
| /ko + e + ɛhɛria/ | → | [kwejɛhɛria] | kujiondolea lawama |
| /ko + e + adeka/ | → | [kweadeka] | kujiajiri |
| /ko + e + oria/ | → | [kwejoria] | kujiuliza |
| /ko + e + tea/ | → | [gwetea] | kuringa |
| /ko + e + ɔnɛra/ | → | [kwejɔnera] | kujionea |
| /ko + e + +aɣa/ | → | [kwejaɣa] | kujikosea thamani |
| /ko + e + ɛda/ | → | [kwejɛda] | kujipenda |
| /ko + e + ɣeria/ | → | [kwejaɣeria] | kujifanya mzuri |
| /ko + e + tua/ | → | [gwetua] | kujitanya |
| /ko + e + uga / | → | [kwejuɣa] | kujisema |
| /ko + e + a rera / | → | [kwejarwa] [kwejarera] | kujitandika |

Inatubidi kutaja kuwa nusu-vokali hizi haziundwi kila mara katika mazingira yale. Wakati mwingine, katika mazingira ambapo kiini cha kitenzi kinaanzia kwa [i], nusu-vokali ya pili, [j] haielekei kuundwa. Mifano ni kama katika:

| Umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /ko + e + inera/ | → | [kweinera] | kujiimbia' |
| /ko + e + igera/ | → | [kweiɣera] | kujiwekea' |
| /kp + e + ita/ | → | [kweita] | kujinyonga' |
| /ko + e + iniɣia/ | → | [kweiniɣia] | kujifanya unaimba |
| /ko + e + i ania/ | → | [kweiɣania] | kujitosheleza |
| /ko + e + i e: re :ra/ | → | [kweiɣerera] | kujiwekelea' |

Vile ilivyodhihirika, kufikia hapa ni kuwa [w] inaundwa katika mazingira mapana zaidikuliko[j], katika Kikikuyu cha Kabete, pamoja na Kikikuyu sanifu.

Katika mofimu za umilikaji pia [w] inaelekea kuundwa. Mifano ni kama vile:

| Umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /ro + akwa/ | → | [rwakwa] | yangu' |
| /ro + ake/ | → | [rwake] | yake' |
| /ro + aɔ/ | → | [rwaɔ] | yao' |
| /ro + ajɔ/ | → | [rwaɔ] | yake' |
| /ro + ašiɔ/ | → | [rwasiɔ] | yao' |
| /ro + akɛ / | → | [rwakɛ] | yake |
| /o + akwa/ | → | [wakwa] | wangu |

| | | |
|---|---|---|
| /o + aku/ → | [waku] | yako' |
| /o + ake/ → | [wakɛ] | wake' |
| /o + ito/ → | [wito] | wetu' |
| /o +aɲʊ/ → | [waɲ ʊ] | wenu' |
| /o + a / → | [waɔ] | wao' |

Tunaweza kueleza katika sheria ya kifonolojia, kuwa:

$$[+\text{silabi}] \rightarrow [-\text{silabi}] \Big/ __ \left\{ \begin{matrix} \overset{V}{[+\text{chini}]} \\ \overset{V}{\begin{bmatrix} +\text{mbele} \\ -\text{juu} \\ -\text{chini} \end{bmatrix}} \\ \overset{V}{\begin{bmatrix} +\text{mbele} \\ +\text{juu} \end{bmatrix}} \\ \overset{V}{\begin{bmatrix} +\text{nyuma} \\ -\text{juu} \\ -\text{chini} \end{bmatrix}} \end{matrix} \right\}$$

Nusu-vokali [j] inaundwa katika mazingira ya mofimu ya umilikaji. Ni kama katika:

| umbo ndani | umbo nje | maana |
|---|---|---|
| /e + akwa/ → | [ja:kwa] | yangu' |
| /e + aku/ → | [ja:ku] | yako' |
| /e + aɲu/ → | [ja:ɲu] | yenu' |
| /e + ake/ → | [ja:ke] | yake' |
| /e + aɔ/ → | [ja:ɔ] | yao' |

Sheria ya kifonolojia ni :

$$[+\text{silabi}] \rightarrow [-\text{silabi}] \Big/ __ \overset{V}{\begin{bmatrix} -\text{juu} \\ -\text{chini} \\ +\text{mbele} \end{bmatrix}}$$

### 3.1.2 KUDONDOSHWA KWA VOKALI

Mabadiliko mengine ambayo yanaratibiwa chini ya sheria za muundo wa silabi unaopendekezwa ni kudondoshwa kwa vokali.

Halia hii ikatika Kikikuyu cha Kabete, kama ilivyojitokeza katika Kikikuyu sanifu, Kiswahili sanifu, Kipemba, Kimakunduchi na Kitumbatu.

Maganga (1990) anaonyesha vile ilivyo katika lahaja za mwisho nne.

Kudondoshwa kwa vokali ni jambo lisilo geni pia, katika lahaja nyingine za Kiswahili kama Chijomvu, Chichifundi, Kimvita, Kitikuu na Kisiu.

Katika Kikikuyu cha Kabete na Kikikuyu sanifu, pronomino ya nafsi ya kwanza umoja inapokuwa kiima, katika kitenzi, huku ikifuatiwa na yambwa ya pronomino ya nafsi ya tatu wingi, {ma-} vokali inaelekea kudondoshwa. Mifano ni kama vile:

| umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /a+ ma+ ɔɛ / | → | [amɔɛ ] | 'awachukue |
| /a+ ma+ erɛ / | → | [ame re: ] | 'awaambie' |
| /a+ ma+ ɔɛrɛ/ | → | [amɔɛrɛ] | 'awachukulie' |
| /a+ ma+ ɔnɛ / | → | [amɔnɛ] | 'awaone' |
| /a+ ma+ ɛhɛriɛ/ | → | [amɛhɛriɛ] | 'awaondoe' |
| /a+ ma+ etɛ / | → | [amɛtɛ] | 'awaite' |
| /a+ ma+ ɛdɛ / | → | [amɛdɛ] | ~~'awauzie'~~ "awapende" |

Sheria ya kifonolojia inayoonyesha kudondoshwa kwa vokali zile ni:

[+ vokali, - konsonanti] → ɸ / — [- juu, - chini, + nyuma] ∨ [- juu, - chini, + mbele]

Hata hivyo, sio mazingira yote yanaipa vokali kupotea. Katika mashina ya vitenzi yanayoanza kwa [a] au [i], vokali hazidondoshwi. Mifano ni:

| umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /a + ma + ɣɛ / | → | [ama: ɣɛ ] | awakose' |
| /a + ma + aɣɛ / | → | [ama: ɣɛ ] | awatawale |
| /a + ma +ije/ | → | [ama: ije] | awaibie |
| /a + ma + iɣɛ / | → | [ama: iɣɛ] | awasalimishe |
| /a + ma +ije:rɛ/ | → | [ama: ije:rɛ] | awaibie |

Katika kitenzi, iwapo nafsi ya pili wingi {ma-} ndio kiima, na mofimu ya na mofimu ya nafsi ya pili, wingi {ma-} vile vile ndiyo yambwa, vokali inadhihirisha:

| umbo ndani | umbo nje | maana |
|---|---|---|
| /ma + ma + ɔ ɛ / → | [mamɔ:ɛ] | wawachukue |
| /ma + ma + inerɛ/ → | [mamainɛrɛ] | wawaimbie |
| /ma + ma + ɔere/ → | [mamɔ ɛrɛ] | wawachukulie |
| /ma + ma + ɔnɛ/ → | [mamɔnɛ] | wawaone |
| /ma + ma + ɛhɛriɛ/ → | [mamɛhɛriɛ] | wawaondoe |
| /ma + ma + etɛ/ → | [mamɛtɛ] | wawaite |
| /ma + ma + ɛderiɛ/ → | [mamɛdɛriɛ] | wawauzie |

Sheria ya kuonyesha fenomena hii ni kama ile tuliyoiandika katika mazingira yale ya kwanza lakini tutaiandika tena kwa kutaka kurahisisha urejelezi.

$$\begin{bmatrix}+\text{vokali}\\-\text{konsonanti}\end{bmatrix} \rightarrow \phi \Big/ - \left\{\begin{array}{c}\begin{bmatrix}-\text{juu}\\-\text{chini}\\+\text{nyuma}\end{bmatrix}\\ \begin{bmatrix}-\text{juu}\\-\text{chini}\\+\text{mbele}\end{bmatrix}\end{array}\right\}$$

Kama ilivyo katika nafsi ya kwanza umoja, {a-}, mofimu ya nafsi ya pili wingi {wi-} inapotangulia kiini cha kitenzi ambacho kinaanzia kwa [a] au [i], vokali haielekei kudondoshwa. Ni kama vile katika:

| Umbo ndani | umbo nje | maana |
|---|---|---|
| /ma + ma + aorɛ / → | [mama: orɛ] | wawatue mzigo |
| /ma + ma + areriɛ/ → | [mama: reriɛ] | wawazugumzie |
| /ma + ma + arerɛ / → | [mama:rɛrɛ] | wawatandikie |
| /ma + ma + iɣererɛ/ → | [mamaiɣererɛ] | wawawekelee |
| /ma + ma + iterɛ / → | [mama iterɛ] | wawamwagie |
| /ma + ma +ike: iriɛ/ → | [mama ike:riɛ] | wawarushie |

Jambo ambalo hatujalitaja kufikia hapo, na ambalo hutendeka vokali inapodondoshwa ni kurefushwa kwa vokali inayobakia. Mazingira yote yaliyothibiti kudondoshwa kwa vokali yameonyesha kurefushwa kwa vokali inayobakia. Jambo hili linajitokeza hata katika lugha nyingine za Kibantu kama vile Wanga, Logooli, na Bukusu; zote ambazo ni lahaja za Kiluhya. Mifano michache inayofuatia inathibitisha dai letu:

| | Umbo ndani | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| Wanga - | /a + la + ora/ → | [alo:ra] | ataota moto |
| Lagooli - | /a + ma + uru/→ | [amu:ru] | pua' |
| Bukusu - | /a + la + oma/ → | [alo:ma] | atakausha |

### 3.1.3 KUDONDOSHWA KWA KONSONANTI

Bakari (1982) na Hooper (1976) wanaelekea kukubaliana kimaoni, kuwa iwapo sauti fulani mbili zimepakana, na zina sifa fulani zilizoshabihiana, mojawapo ya sauti zile ina uwezekano wa kudondoshwa.

Lahaja za Kiswahili, kama vile Chi -chifundi na Kivumba zinaelekea kuwa na fenomena ya kuingizwa kwa konsonanti, katika sarufi ya lugha hizi.

Kwa upande wake, Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete, zinaelekea kuthibiti halia ya konsonanti kudondoshwa, badala yake. Hyman (1975:163) anasema:

> "Kwa jumla, konsonanti zinadondoshwa; na vokali kuingizwa; ili kuleta muundo asilia wa silabi"[3]

Anaendelea kueleza, (1975:164):

> "Kwa hivyo sheria za kuingiza au kudondoshwa sauti zina uasilia kwa kiasi kuwa zinajenga miundo asilia zaidi ya silabi"[4]

### 3.1.4 KUDONDOSHWA KWA [n]

Schane, naye (1973:207) anaeleza namna ambavyo konsonanti hudondoshwa katika lugha ya Kifaransa. Kulingana na maelezo yake, ni kuwa; pawapo na konsonanti moja katika mwisho wa neno moja, na pawe na konsonanti nyingine katika mwanzo wa neno linalofuatia, moja katika konsonanti zile, ni lazima idondoshwe.

Katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete, nasali [n] inadondoshwa katika baadhi ya mazingira, ikiwa inafuatiwa na nasali nyingine, hususan katika mpaka wa mofimu ya shina la kitenzi na mofimu ya Kiima.

Tumeitoa mifano ili kuonyesha vile halia hii inavyotekelezwa.

| Umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /n + nuŋ gɛ/ | → | [nuŋ gɛ] | 'ninuke' |
| /n + ariɛ/ | → | [ŋ ariɛ] | 'niudhi ' |
| /n + a: riɛ/ | → | [ŋa:r'ɛ] | 'niinamishe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| /n+oroɾiɛ/ | ⟶ | [ɲororiɛ] | nisimange |
| /n+ɲitɛ/ | ⟶ | [ɲitɛ] | nishike |
| /n+ɲitiɛ/ | ⟶ | [ɲitiɛ] | nikaze |
| /n+ɲɔtɛ/ | ⟶ | [ɲɔtɛ] | nione kiu |
| /n+makiɛ/ | ⟶ | [makiɛ] | nishtue' |
| /n+madɛ/ | ⟶ | [madɛ] | nibonde |
| /n+mɔdɛ/ | ⟶ | [mɔdɛ] | nifinye |
| /n+morekɛ/ | ⟶ | [morekɛ] | niangazie |
| /n+mi:ɾɛ/ | ⟶ | [mi:rɛ] | nifinye |
| /n+miɾɛ/ | ⟶ | [mirɛ] | nipenge makamasi |
| /n+miⁿjiɛ/ | ⟶ | [miⁿjiɛ] | nirashie |
| /n+nɔɾɛ/ | ⟶ | [nɔrɛ] | ninone |
| /n+nɔ:ɾɛ/ | ⟶ | [nɔ:rɛ] | nitie makali |

Vile inavyoonekana ni kuwa nasali inadondoshwa katika mazingira ambapo nafsi ya kwanza umoja, {n-} inakuwa kiima cha kitenzi.Kinapotanguliwa na viima vinginevyo, nasali haionekani kudondoshwa. Mifano ni kama vile:

| Umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /ma + ŋga:riɛ/ | ⟶ | [maŋa:riɛ] | wainamishe' |
| /ma + ŋgariɛ/ | ⟶ | [maŋariɛ] | waudhi' |
| /ma + makiɛ/ | ⟶ | [mamakiɛ] | washtue' |
| /ma + i: tɛ/ | ⟶ | [maɲi:tɛ] | washike' |

Sheria ya kifonolojia inayoonyesha kupotea kwa nasali hizi ni:

[+ nasali] ⟶ ɸ / — [+ nasali]

[ngeli ya I].

## 3.1.5 KUDONDOSHWA KWA [ɾ]

Licha ya nasali [n] kupotea, sauti nyingine ambayo inaelekea kupotea ni kilainisho, [r].

Mazingira ambayo halia hii inaelekea kuthibitika ni kama yale ya kudondoshwa kwa [n]. Mifano ni kama vile:

| Umbo ndani | umbo nje | maana |
|---|---|---|
| /n + remɛ/ | [ne.mɛ] | nilime |
| /n + riŋgɛ/ | [niŋ gɛ] | nigonge |
| /n + ro.mɛ/ | [no mɛ] | niume' |

Hata hivyo, si kila mara ambapo mfuatano wa [n] na [r] unaonyesha kupotea kwa [r]. Katika mazingira mengineyo sauti hiyo inaonyesha mabadiliko tofauti kabisa. Ni kama vile:

| Umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /n + raihɛ/ | → | [ⁿdaihɛ] | nirefuke' |
| /n + roɛ/ | → | [ⁿdoɛ] | nipigane' |

Hatunuii kuingilia mifano ya aina hii kwa undani, kwa kuwa tutaishughulikia kwa kina zaidi, katika sehemu ya kukazana kwa sauti.

Sheria ya kudondoshwa kwa [r] ni:

$$\begin{bmatrix} + \text{konsonanti} \\ + \text{vokali} \end{bmatrix} \rightarrow \phi \; / \; __ \; \begin{bmatrix} + \text{nasali} \\ + \text{korono} \end{bmatrix}$$

[ngeli ya 1]

## 3.1.6 UKAKAAISHAJI

Katika Kikikuyu cha Kabete, na Kikikuyu sanifu ukakaaishaji unashuhudiwa katika mazingira ya nafsi ya kwanza umoja, {n -}, kutangulia vitenzi ambavyo vina mashina yanayoanza kwa vokali [a], [ɛ] [ɪ], [i], [ɔ] na [u]. Mifano ni kama vile.

| Umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /n + aɤimorɛ / | → | [ⁿɟaɤimorɛ] | nipige chafya |
| /n + anorɛ/ | → | [ɲanorɛ] | nianue' |
| /n + ane: re:rɛ/ | → | [ɲane:re:rɛ] | nipase sauti |
| /n + ɛⁿdɛ / | → | [ɲɛⁿdɛ | nipende |
| /n + ɛⁿdi:ɛ/ | → | [ɲɛⁿdiɛ ] | niuze |
| /n + ɛⁿɟɛ/ | → | [ɲɛⁿɟɛ ] | ninyoe |
| /n + ɛhɛrɛ/ | → | [ⁿɟɛhɛrɛ] | niondoke |
| /n + inɛ / | → | [ɲinɛ ] | niimbe |
| /n + iŋgɛrɛ/ | → | [ɲiŋgɛrɛ] | niingie |
| /n + imɛ / | → | [ɲimɛ ] | ninyime |
| /n + ɔnɛ / | → | [ɲɔnɛ ] | nione |
| /n + omɛ/ | → | [ɲomɛ] | nikauke |
| /n + ɔnɛ / | → | [ɲɔnɛkɛ] | nipatikane |
| /n + umɛ/ | → | [ɲumɛ] | nitoke |

Nasali hii ambayo inawakilisha pronomino ya nafsi ya kwanza umoja, {n-} inaelekea kufifia, katika umbo la nje. Haijapotea

kabisa, wala si dhabiti kabisa kuwakilishwa kama konsonanti nzima. Tumetumia [ⁿ -] kuonyesha kufifia huku.
Sheria ya kifonolojia ya ukakaaishaji itakuwa:

$$\begin{bmatrix} +\text{ nasali} \\ +\text{ mbele} \\ +\text{ korono} \end{bmatrix} \longrightarrow [+\text{ nyuma}] \Big/ ___ \begin{Bmatrix} \vee \\ \begin{bmatrix} +\text{ juu} \\ +\text{ nyuma} \end{bmatrix} \\ \vee \\ \begin{bmatrix} +\text{ juu} \\ +\text{ mbele} \end{bmatrix} \\ \vee \\ \begin{bmatrix} -\text{ juu} \\ -\text{ chini} \\ +\text{ mbele} \end{bmatrix} \\ \vee \\ \begin{bmatrix} -\text{ juu} \\ -\text{ chini} \\ +\text{ nyuma} \end{bmatrix} \\ \vee \\ [+\text{ chini}] \end{Bmatrix}$$

## 3.2.0. SHERIA ZA UWIANO

Katika sehemu hii tutazingatia halia za kisauti ambapo konsonanti zinaathiri konsonanti, konsonanti zinaathiri vokali, au pia, vokali zinaathiri vokali nyenzake. Schane (1973) anaelekea kufasili sheria hizi kama aina ambayo hufanya sauti fulani zifanane na nyingine kwa sifa fulani.

## 3.2.1 KUATHIRIWA KWA NASALI KUHUSU MAHALI PA KUTAMKIA

Tumeona kuwa fenomena ya nasali kuathiriwa kuhusu mahali pa kutamkia ni ya kifonolojia katika Kiswahili sanifu. Hivi ni kusema kuwa nasali huathiriwa katika mahali pa kutamkia, kote kote katika ngeli ya 9, au mazingira yake.

Kuhusu Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete nasali inaelekea kuwa [ɖ mahali ]/ - [ɖ mahali], lakini katika mazingira tofauti. Pamoja na mazingira mengine na mengine katika ngeli ya 9, kuna nomino ambazo zinaonyesha kubadilika kwa nasali, na nyingine ambazo hazithibiti ukweli huu. Mifano ni kama vile:

| Umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /N + ama/ | ⟶ | [ ɲama ] | nyama' |
| /N +ɛki/ | ⟶ | [ ɲɛki' ] | nyasi' |
| /N + gɔdu/ | ⟶ | [ ŋɔdu ] | kondoo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| /N +ɔka/ | ⟶ | [ ɲɔka ] | nyoka |
| /N + gui/ | ⟶ | [ ŋgui ] | mbwa |
| /N + gɔbɛ/ | ⟶ | [ ŋɔbɛ ] | ngombe' |

Nomino ambazo hazionyeshi athari hii ni zile ambazo mofimu ya ngeli ya 9 ni {ϕ}. Ni kama vile:

| Umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /N + bɔga/ | ⟶ | [ⁿbo ga] | mboga' |
| /N + jera/ | ⟶ | [ⁿǰera] | njia' |

Kwa hivyo tutasema:

[ + nasali] ⟶ [d mahali] /___ [d mahali]

Mazingira mengineyo ambayo yanadhihirisha kuathiriwa kwa nasali ni mofimu ya nafsi ya kwanza umoja {n-}, inapotangulia shina la kitenzi. Mifano ni:

| Umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /n + ɣerɛ / | ⟶ | [ŋgerɛ] | nikachukue |
| /n + ɣɔmɛ / | ⟶ | [ŋɔmɛ] | nigome |
| /n + ɣadɛ / | ⟶ | [ŋadɛ] | nife-ganza |
| /n + kerɛ / | ⟶ | [ŋgerɛ] | nivuke |
| /n + ɣorɛ / | ⟶ | [ŋgorɛ] | ninunue |
| /n + kimɛ / | ⟶ | [ŋgimɛ] | niponde |
| /n + kerɛ / | ⟶ | [ŋgerɛ] | nipite |
| /n + ɣiɛ / | ⟶ | [ŋgiɛ ] | nisumbue |
| /n + ɣaɛ / | ⟶ | [ŋgaɛ] | nigawe |
| /n + ɣiriɛ / | ⟶ | [ŋgiriɛ] | nikataze |
| /n + ɣarorɛ / | ⟶ | [ŋgarorɛ] | nigeuze |
| /n + karɔrɛ / | ⟶ | [ŋgarɔrɛ] | nikaangalie |
| /n + karariɛ / | ⟶ | [ŋgarariɛ] | nitoe ubishi |
| /n + ɣimarɛ / | ⟶ | [ŋimarɛ] | niwe mkubwa |

Katika mazingira haya, kuna halia ambayo inajitokeza sawia, na kuathiriwa kwa nasali.

Japo tutaiingilia kwa undani wake, katika sehemu ya 3.2.2, tutatoa mifano michache ya sauti ambayo ni [- ghuna] kuwa [+ ghuna]. Mifano ni:

| Umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /n + kimɛ/ | ⟶ | [ŋgimɛ] | niponde' |
| /n + kɔmɛ/ | ⟶ | [ŋgɔmɛ] | nilale |
| /n + kerɛ/ | ⟶ | [ŋgerɛ] | nivuke' |

| | | |
|---|---|---|
| /n + kamɛ/ | [ŋgamɛ] | nikamue' |
| /n + keɣɛ | [ŋgeɣɛ] | niwe mjinga' |
| /n + kɛrɛ/ | [ŋgɛrɛ] | nikata- kate |
| /n + kuɛ/ | [ŋguɛ] | nibebe |

## 3.2.2 SIFA YA UGHUNA

Katika mazingira fulani, sauti ambazo si ghuna, zinakuwa ghuna. Halia hii inajitokeza wakati mofimu ya nafsi ya kwanza, {n-} inatangulia mashina ya vitenzi ambayo yanaanza kwa [k]. Mifano ni kama vile:

| Umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /n + kimɛ / | ⟶ | [ŋgimɛ] | niponde |
| /n + kɔmɛ/ | ⟶ | [ŋgomɛ] | nilale |
| /n + kerɛ/ | ⟶ | [ŋge:rɛ ] | nivuke |
| /n + kirɛ/ | ⟶ | [ŋgirɛ ] | ninyamaze |
| /n + kamɛ / | ⟶ | [ŋgamɛ] | nikamue |
| /n +kegɛ/ | ⟶ | [ŋgegɛ] | niwe mjinga |
| /n + kuɲɛ | ⟶ | [ŋguɲɛ] | nifinye |
| /n + kedɛ/ | ⟶ | [ŋgedɛ] | nisuke |
| /n + twarɛ/ | ⟶ | [ⁿdwarɛ] | nipeleke |
| /n + to:rɛ/ | ⟶ | [ⁿdo:rɛ] | niishi milele |
| /n + torɛ/ | ⟶ | [ⁿdorɛ] | nitoboe shimo |
| /n + te:rɛ/ | ⟶ | [ⁿde:rɛ] | nikose kuhudhuria |
| /n + tuɛ/ | ⟶ | [ⁿduɲɛ | ninyang'anye |
| /n + tigɛ/ | ⟶ | [ⁿdiɣɛ] | niache |
| /n + tɛiɣiɛ/ | ⟶ | [ⁿdɛiɣiɛ] | nisaidie |

Ngeli ya 14 pia inathibiti halia hii ya sauti ambayo ni [-ghuna] ⟶ [+ ghuna]. Lakini ni wakati ambapo yambwa ni pronomino ya nafsi ya kwanza, umoja, {e-} na inapofuatiwa na shina la kitenzi. Mifano ni kama:

| Umbo ndani | umbo nje | maana |
|---|---|---|
| /ko + e + tea / ⟶ | [gwe tea ] | kujinata' |
| /ko + e + tɛma / ⟶ | [gwetɛma] | kujikata' |
| /ko + e + šɔkia / ⟶ | [gwe šɔkia] | kunugunika' |
| /ko + e + tuera / ⟶ | [gwet uera] | kujiamulia' |
| /ko + e + ɣokia / ⟶ | [gweɣokia] | kujiharibu' |

Katika kuandika sheria ya kifonolojia, tutasema:

[-ghuna] ⟶ [+ ghuna] / — V.

## 3.2.3. SIFA: ISO GHUNA

Kabla ya kutoa data ya kuthibitisha halia hii, ambapo sauti ghuna inapoteza ughuna wake, tunalo jambo ambalo tungependa kueleza, kwanza.

Na haya ni mabadiliko ambayo yanajitokeza katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete, Mathalani.

Kuwa: zipo sauti ambazo zinapata ughuna, ilhali nyinginezo, katika neno moja lile zinapoteza ughuna.

Karega (1977:154) anaelekea kueleza kuwa mabadiliko haya, ama, ya aina hii, ni mfano wa athari kwa mbali, katika silabi zinazopakana.

Kiini cha mabadiliko, kikielezwa kwa sifa - tofautishi itakuwa ni kama vile:

$$\begin{bmatrix} +\text{nyuma} \\ +\text{juu} \\ -\text{sauti} \\ +\text{mtuo} \\ -\text{sauti} \end{bmatrix} \longrightarrow [+\text{sauti}] \; / \; \# V \;\text{---}\; +\begin{bmatrix} K \\ +\text{sauti} \end{bmatrix}$$

K inasimamia konsonanti. Halia hii inajulikana kama sheria ya Dahl, na inapatikana katika lugha nyingi za Kibantu.

Mifano katika Kikikuyu sanifu, mathalani Kikikuyu cha Kabete ni kama:

| Umbo ndani | umbo kati | umbo nje | |
|---|---|---|---|
| /Ka + N + kari / → | /Ka # gari/ → | [gakari] | kijigari |
| /Ka + N + ɣiβitare/ → | /ka # ɣiβitare/ → | [gaɣiβitare] | kijihospitali |
| /Ka + N + kɔma / → | /ka # ŋgɔma/ → | [gakɔma] | 'kijishetani' |
| /Ka + N + kema / → | /ka # ŋ gema / → | [gakema] | kijinyani |
| /Ka + N + kwar / → | /ka # ŋgwarɛ/ → | [gakwarɛ] | 'kijikware |
| /Ka + N + toiɣa/ → | /ka # ⁿdoiɣa/ → | [gatoiɣa] | kijitwiga |

Tukimrejelea Karega tena (1977:154) anaeleza kwamba tunaweza kuwakilisha mabadiliko haya, kwa kutumia [ɣ] badala ya [g]. Sauti hizi kwa maoni yetu, hazileti tofauti ya maana.

Matamshi yanaipa kuwa [ɣ] au [g], katika umbo la nje; kwa hivyo tukaweza kusema:

[ɣakari]
[ɣaterɛβa]
[ɣakɔma]
[ɣakema]
[ɣakwarɛ]
[ɣatoiɣa]

Ilmuradi, maana haibadiliki kwa kutumia moja au nyingine.

Jambo ambalo ni lazima tutaje, na tukikubaliana tena na Karega (1977:154) ni kwamba [g] inaafiki sheria ya kifonolojia, ambayo tuliitoa, nayo ndiyo:

$$\begin{bmatrix} +\text{ nyuma} \\ +\text{ juu} \\ +\text{ mtuo} \\ -\text{ sauti} \end{bmatrix} \longrightarrow [+\text{ sauti}] \;/\; \#\ V \;___\; \overset{K}{+[+\text{ sauti}]}$$

Iwapo tutatumia [ɣ], katika umbo la nje, ili tusizoroteshe sarufi ya lugha tunayoielezea, inatubidi kutaja kwamba si sifa ya [sauti] tu ambayo inabadilika, bali pia sifa ya [mtuo]. Kwa hivyo ukawa pia ni mfano wa kudhoofika kwa sauti. Halia hii inajitokeza katika ngeli ya 12.

Kama tulivyotaja, sauti ambazo si ghuna katika mofimu ya ngeli ya 12 zinakuwa ghuna, katika mwanzo wa majina hayo. Nazo zile ghuna, katika nafasi ya katikati ya majina zinabadilika na kuwa ziso-ghuna. Ikiwa tutafuatanisha sheria hizi mbili, tutasema:

(i) $$\begin{bmatrix} +\text{ konsonanti} \\ +\text{ vokali} \\ +\text{ mfululizo} \\ +\text{ korono} \\ -\text{ sauti} \end{bmatrix} \longrightarrow [+\text{ sauti}] \quad \#\,___\ [\text{ngeli ya 12}]$$

(ii) $$[+\text{ ghuna}] \longrightarrow [-\text{ ghuna}] \quad \underset{[\text{ngeli ya 12}]}{\#\,___\,\#}$$

Lakini yapo majina katika ngeli hii hii ambayo hayadhihirishi hali hiyo ya mambo. Mazingira yenyewe ni wakati ambapo mofimu ya ngeli ya 12, {ka-} inatangulia mashina ya vitenzi yanayoanzia, au kwa nasali [n], ama kilainisho [ɾ]. Mifano ni kama vile:

| Umbo ndani | umbo nje | maana |
|---|---|---|
| /Ka + roreme/ | [karoreme] | kilimi' |
| /Ka + roswere/ | [karošwere] | kijinywele |
| /Ka + roe/ | [karo:ɛ] | kijimto' |

| | | |
|---|---|---|
| /Ka + roɛ / ⟶ | [karo:ɛ] | kijimto' |

Katika mazingira ya mofimu inayoonyesha ukubwa {ke-} ama mofimu ambayo inapotangulizwa majina ya ngeli mbalimbali huleta dhana ya ukubwa, sauti ambazo ni ghuna hupoteza ughuna wake. Mifano ni kama vile:

| Umbo ndani | umbo nje | maana |
|---|---|---|
| /Ke + dɛrɛβa/ ⟶ | [ge:tɛrɛβa] | jidereva' |
| /Ke + doiga/ ⟶ | [ge toiga] | jitwiga |
| /Ke + dira/ ⟶ | [geti:ra] | jisigino |

Inadhihirika kwamba fonimu ambazo ni ghuna zinapoteza sifa hiyo, katikati ya neno.

Kwa hivyo, katika kuandika sheria ya kifonolojia tutasema:

[+ ghuna] ⟶ [- ghuna] / ## ——— #.

Tumetanguliza maelezo juu ya kupoteza ughuna, kwa sauti. Lakini hatuwezi kukosa kueleza kuwa, kama ilivyo katika ngeli ya 12, {ka -} kuwa sauti zilizo katika mwanzo wa nomino zinapata sifa ya ughuna, inakuwa vivyo hivyo katika mazingira haya ya mofimu ya {ke -}. Mofimu hii ni kama tulivyoeleza; kuwa inaleta dhana ya ukubwa, inapotangulia nomino mbalimbali. Kwa hivyo, wakati ambapo sauti za mwanzo zinapata sifa ya ughuna, sauti nyinginezo katikati mwa nomino hizi, katika hali ya ukubwa zinapoteza ughuna na kuwa [ - ghuna].

Tukifuatisha sheria zote mbili, kwa kuwa halia hizo ni za pamoja, tutasema:

(i) [+ konsonanti, - vokali, - mfululizo, + mbele, - ghuna] ⟶ [+ ghuna] / # # ———

(ii) [+ ghuna] ⟶ [- ghuna] / # # ——— #

## 3.2.4 . UWIANO WA VOKALI

Uwiano wa vokali unajitokeza katika lahaja sanifu ya Kiswahili.

Katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete kuna uwiano wa vokali, wa mbali na wa karibu.

Schane (1973:207) anaeleza:

> "Vokali zinaweza kuvutwa mbele na vokali ya mbele; vokali ziathiriane kwa kuwa za mbele, au nyuma, au kwa sifa ya kuviringa".[5]

Mifano ambapo vokali zinaathiri vokali nyinginezo kwa mbali ni kama vile:

| Umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /kim + Vra/ | ⟶ | [kimera] | pondea |
| /ug + Vra/ | ⟶ | [ugera] | semea' |
| /oker + Vra/ | ⟶ | [okerera] | amkia' |
| /roŋ + Vra/ | ⟶ | [roŋgera] | nyoshea' |
| /ken + Vra/ | ⟶ | [kenera] | furahia' |
| /rɔg + Vra/ | ⟶ | [rɔgɛra] | rogea' |

V inasimamia vokali. Kulingana na data hii:

[+ vokali, - konsonanti] ⟶ [- juu, - chini, + mbele] / [+ vokali, - juu, - chini] K ______ .

[Kiambishi]

K inasimamia konsonanti. Hii ni mifano ya uwiano wa mbele.

Tofauti kati ya jumla ya Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete kwa upande wake, na baadhi ya lahaja za Kiswahili ni kuwa uwiano wa vokali unathibitika katika mazingira ya kuundwa kwa nomino kutokana na vitenzi.

Kabla hatujaingilia mifano yenyewe, inatubidi kueleza kwa kifupi, namna mbalimbali za kuundia nomino, kutokana na vitenzi katika Kikikuyu, ili data yetu iwe bayana.

Njia kadha za kuundia nomino, kutoka kwa kitenzi ni kuongeza vokali ya {-i} katika shina la nomino. Kisha kuongeza, pale mwanzo, mofimu, au viambishi mbalimbali, ili kuyapa majina yale ngeli. Viambishi hivi ni kama vile {o-},{ɣɛ},{u -}, {mwe-} na {o-}..

Vokali zile za mwisho ni {- i -}, {ɔ} na {-o}.

Tunaorodhesha mifano yenyewe, ambapo vokali iliyopo katika mofimu ya ngeli inaathiri vokali ya mwisho, ya nomino. Athari hizi zinahusu sifa za [urefu] na [mbele], au [nyuma].

Katika athari ya urefu, tunapata:

| Kitenzi | | Nomino | maana |
|---|---|---|---|
| /go + ki ɲa/ | ⟶ | [mokiɲɛrɛ] | jinsi ya kutembea' |
| /go + kiːɲa/ | ⟶ | [mokiɲeːrɛ] | jinsi ya kusugua meno |
| /ko + i a/ | ⟶ | [moiʤerɛ] | jinsi ya kuweka' |
| /ko + ira/ | ⟶ | [oːiro] | weusi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| /go + ɣɔrita/ | ⟶ | [moɣɔrɛriɛ] | jinsi ya kuchokoza' |
| /ku +ɔha/ | ⟶ | [keɔhɔ] | kifungo' |
| /go + taŋga / | ⟶ | [getaŋgɔ] | usumbufu |
| /go + tuma/ | ⟶ | [getumɩ] | mahali pa kushonea' |
| /ko + uma/ | ⟶ | [umiɣiɔ] | jambo lililo la fanaka' |
| /ko + era/ | ⟶ | [mwe:rɔ] | hiari' |
| /ko + etea/ | ⟶ | [mweteɔ] | maringo' |
| /ko + eata/ | ⟶ | [mwe:jatɔ] | maringo' |

Katika sheria ya kifonolojia tutasema kuwa:

[+ vokali] ⟶ [d urefu] / —[d urefu] K ——— .
[tamati] [ngeli]

Katika mazingira mengine, vokali ile tamati inaathiriwa na vokali ya mofimu ya ngeli, kuwa [+ mbele] au [- mbele]. Mifano ya athari ya [+ mbele] ni:

| <u>Kitenzi</u> | | <u>Nomino</u> | <u>maana</u> |
|---|---|---|---|
| /ko +ɛtɛrɛr + a/ | ⟶ | [wɛtɛrɛri] | subira' |
| /ko +ɛⁿda / | ⟶ | [ wɛdi] | hiari' |

Sheria ya kifonolojia itakuwa:

[+ vokali] ⟶ [d mbele] / —[d mbele] K ——— .
[ngeli]

Sarufi ya lugha hii, Kikikuyu, inaonyesha rutuba na ladha, katika fenomena hii, hususan. Kwamba, vokali ile tamati inaathiriwa kwa sifa mbili pamoja, [d urefu] na [d -mbele].
Mifano ni kama vile:

| <u>Kitenzi</u> | | <u>Nomino</u> | <u>Maana</u> |
|---|---|---|---|
| /Ku +ɔrɔrɔ+ a/ | ⟶ | [wɔrɔrɔ ] | ulainifu' |
| /ko + oma/ | ⟶ | [o :mo] | ugumu' |
| /ko + iɣuana/ | ⟶ | [oiguano] | masikizano' |
| /ko + ira/ | ⟶ | [o:iranɔ] | kutoheshimiana' |
| /ko + ira/ | ⟶ | [oiro] | weusi' |

Katika kuandika sheria ya kisauti, tutasema kuwa:

$$[+\text{vokali}] \longrightarrow \begin{bmatrix} \alpha \text{ urefu} \\ \beta \text{ nyuma} \end{bmatrix} \Big/ \; — \; \begin{bmatrix} \alpha \text{ urefu} \\ \beta \text{ nyuma} \end{bmatrix}, \; \kappa \; \underset{[\text{ngeli}]}{____}$$
[tamati]

Ipo mifano ya uwiano kamili, kama vile katika nomino [ɯɔrɔro] [o:mo], ambazo zina maana ya `ulainifu' na `ugumu', kama zinavyofuatana.

## 3.3.0 KUKAZANA KWA SAUTI

Kama tulivyoeleza katika 2.3.0., sauti zimepangwa, katika isimu, kulingana na udhabiti wake, na udhaifu wake. Hivi kwamba, kulingana na mabadiliko yenyewe, toka kikundi kimoja hadi kingine, sauti husemekana kuwa imekazana, au ikadhoofika. Hooper (1976:201) anasema:

> "Sifa ya kukazana inalingana kwa kiasi na sifa ya kifonetiki ya usonoranti, kwa makisio"[6]

Katika kueleza ruwaza ya sauti, kulingana na viwango vya udhaifu, kuelekea udhabiti, anaeleza:

> "Tutautoa ushuhuda wa kifonolojia katika kueleza ruwaza ya kukazana, ambayo imejitenga kabisa na muundo wa silabi. Ushuhuda huu unaonyesha kuwa konsonanti ziso-ghuna zinatangulia katika sifa au ruwaza ya kukazana; sauti za mtuo zikatangulia sauti za mkwaruzo, ziso-nasali zikitangulia nasali, nazo nasali zikitangulia vilainisho na nusu-vokali".[7]

Nukuu hii ni kwa mujibu wa Hooper (1976:203).

Katika Kikikuyu sanifu, na Kikikuyu cha Kabete, vilainisho vinabadilika na kuwa sauti ya mtuo ilhali sauti za mkwaruzo zinabadilika na kuwa za mtuo. Tukianzia kwa vilainisho, tunapata mifano kama:

| Umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /n + rugɛ/ | ⟶ | [ⁿdugɛ] | nipike' |
| /n + re:rɛ/ | ⟶ | [ⁿderɛ] | nilie' |
| /n + rɔrɛ/ | ⟶ | [ⁿderɛ] | nilee' |
| /n + rɛgɛ/ | ⟶ | [ⁿdɛgɛ] | nikatae' |
| /n + rɔrɛ/ | ⟶ | [ⁿdɔrɛ] | niangalie |

| | | | |
|---|---|---|---|
| /n + rasiɛ/ | ⟶ | [$^{n}$da:siɛ] | nitoe mahari' |
| /n + roɛ/ | ⟶ | [$^{n}$doɛ] | nipigane' |
| /n + rɛhɛ/ | ⟶ | [$^{n}$dɛ:hɛ] | nilete' |
| /n + rogamɛ/ | ⟶ | [$^{n}$doɣamɛ] | nisimame' |

Inavyoonekana ni kuwa, pamoja na /r/ kuwa [d], nasali ile, /n/ inadodondoshwa, katika umbo la ndani. Kwa sababu hiyo, inatosha kusema kuwa /r/ inabadilika, na kuwa [d].

Sheria ya kifonolojia itakuwa:

[+ vokali, + konsonati, - latero] ⟶ [- vokali] / — { [+ juu, + nyuma] ∨ [+ nyuma, - juu, - chini] ∨ [+ mbele, - juu, - chini] ∨ [+ chini] }

Hiyo haina maana kuwa kila mara [r] itanguliapo vokali zile, {a, e, ɔ, o, u} kuwa inabadilika na kuwa [d].

Katika mazingira mengine, kilainisho hicho kinathibiti mabadiliko mengine kabisa. Mifano ni kama vile:

| Umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /n + riŋgɛ/ | ⟶ | [niŋgɛ] | nigonge' |
| /n + raŋgɛ/ | ⟶ | [naŋ gɛ] | nikanyange |
| /n + romɛ/ | ⟶ | [nomɛ] | niume' |

Katika mazingira haya, [r] inaelekea kupotea.

Sauti ya /β/ vile vile, huweza kubadilika na kuwa [b]. Ni mfano mwingine wa kukazana kwa sauti. Mifano ni:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /n +βerɛ/ | ⟶ | [$b^{h}$erɛ] | nilainishe supu |
| n +βu tɛ/ | ⟶ | [$b^{h}$utɛ] | nitoe manyoya |
| /n +β urɛ/ | ⟶ | [$b^{h}$urɛ] | aina fulani ya kulainisha kitu |

Kama inavyojitokeza, kiambishi hichi cha nafsi ya kwanza, {n-} kinapodondoshwa, ile sifa ya mpumuo, [$^{h}$], , inabakia katika sauti inayofuata, [b]. Ni ishara ya kuonyesha kuwa mofimu fulani imepotea.

Sifa hii si geni katika lugha nyinginezo za Kibantu kama vile Kimvita, ambayo ni mojawapo ya lahaja za Kiswahili. Katika lugha hii (Kimvita) sifa ya mpumuo hutofautisha maana ya maneno kama vile:

| | | |
|---|---|---|
| [ka:] | - | la kupikia' |
| [k$^{h}$a:] | - | mnyama mdogo wa baharini' |
| [pa: ] | - | ya nyumba' |
| [p$^{h}$a:] | - | mnyama |
| [cuŋgu] | - | cha kupikia |
| [c$^{h}$uŋgu] | - | mdudu |

Katika kuandika sheria ya kuonyesha kuwa /β/ inakuwa [b], tutasema:

$$\begin{bmatrix} + \text{konsonanti} \\ - \text{vokali} \\ + \text{mbele} \\ + \text{mfululizo} \end{bmatrix} \longrightarrow [-\text{mfululizo}] \; / \; [+\text{ nasali}] _____ .$$

Sauti nyingine ambayo hubadilika ni [š] kuwa [ʃ̌]. Mifano ni kama vile:

| Umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /n + šiarɛ/ | ⟶ | [$^{h}$ʃ̌iarɛ] | nizae' |
| /n + šɔkiɛ/ | ⟶ | [ʃ̌ɔkiɛ] | nirudishe |
| /n + šibɛ/ | ⟶ | [ʃ̌ibɛ] | nilime' |
| /n + šukɛ/ | ⟶ | [ʃ̌ukɛ] | nisengenye' |
| /n + šejiɛ/ | ⟶ | [ʃ̌ɛjiɛ] | nibadilishe' |
| /n + šanorɛ/ | ⟶ | [ʃ̌anorɛ] | nichane' |
| /n + šɛrɛ/ | ⟶ | [ʃ̌ɛrɛ] | nizuru' |
| /n + šɔrɛ/ | ⟶ | [ʃ̌ɔrɛ] | nichore' |
| /n + šariɛ/ | ⟶ | [ʃ̌ariɛ] | nitafute' |
| /n + širɛ/ | ⟶ | [ʃ̌irɛ] | nikesi |
| /n + šidɛ/ | ⟶ | [ʃ̌idɛ] | nishinde |
| /n + šaŋgɛ / | ⟶ | [ʃ̌aŋgɛ] | niranda-rande' |
| /n + šuriɛ/ | ⟶ | [ʃ̌uriɛ] | niniginize' |
| /n + šuɛ/ | ⟶ | [ʃ̌uɛ] | nijute' |

Sheria ya kifonolojia itakuwa:

$$\begin{bmatrix} +\text{konsonanti} \\ -\text{vokali} \\ +\text{mfululizo} \\ +\text{korono} \end{bmatrix} \rightarrow [-\text{mfululizo}] \;/\; __ \left\{ \begin{matrix} \text{V} \\ \begin{bmatrix} +\text{juu} \\ +\text{mbele} \end{bmatrix} \\ \text{V} \\ \begin{bmatrix} +\text{juu} \\ -\text{mbele} \end{bmatrix} \\ \text{V} \\ \begin{bmatrix} -\text{juu} \\ -\text{chini} \end{bmatrix} \\ \text{V} \\ \begin{bmatrix} +\text{mbele} \\ -\text{juu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix} \\ \text{V} \\ \begin{bmatrix} +\text{chini} \end{bmatrix} \end{matrix} \right\}$$

Mfano pekee wa /j/ kuwa [š] ni:

| umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /mo + ija/ | ⟶ | [mo:iši] | \`mwizi' |

Mfano huu unaelekea kulingana na ule wa Kiswahili sanifu ambapo:

| umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /mu + ibi/ | ⟶ | [mwizi] | \`mwizi' |

Kufikia hapo, tunaweza kujumlisha mifanyiko ya kisauti ambayo inahusu kukazana kwa sauti, katika Kikikuyu sanifu, na Kikikuyu cha Kabete, na pengine kulinganishwa na lugha nyingineo.

Jumla ya kukazana ni:

$$\begin{bmatrix} \text{r} \\ \beta \\ \check{\text{s}} \\ \text{j} \end{bmatrix} \rightarrow \begin{bmatrix} \text{d} \\ \text{b} \\ \check{\text{j}} \\ \check{\text{s}} \end{bmatrix} \;/\; __ [+\text{nasali}]$$

Kwa kiasi wastani, jumla ya kukazana kwa sauti katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete inaelekea kulingana na halia ile, katika Kitharaka. Katika lugha hii tunapata:

$$\begin{bmatrix} \text{r} \\ \beta \\ \text{j} \\ \gamma \end{bmatrix} \rightarrow \begin{bmatrix} \text{d} \\ \text{b} \\ \check{\text{j}} \\ \text{g} \end{bmatrix}$$

8.

Mfano huu ni kwa mujibu wa Mberia (1981:55)

Sheria ya kifonolojia ambayo inaonyesha /j/ kuwa [š] katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete ni:

$$\begin{bmatrix} +\text{ vokali} \\ +\text{ konsonanti} \end{bmatrix} \rightarrow [-\text{vokali}] \; / \quad V - V.$$

## 3.4.0 HITIMISHO

Katika sura hii tulikuwa na lengo-pacha. Moja, ni kudhihirisha mifanyiko ya kisauti katika Kikikuyu sanifu ambacho Karega (1977) na Mukuriah (1987) wamekipa lakabu ya lahaja ya Kusini.

Pamoja na hayo, tumetaka kuonyesha kuwa; hicho ambacho wazungumzaji - wazaliwa wamekiita Kikikuyu cha Kabete, kwa vipimo vya kifonolojia, hakikujitokeza kuwa tofauti, hata kidogo, na Kikikuyu ambacho kinatumiwa kwa shughuli rasmi kama vile utangazaji na uandishi.

Sababu yetu ya kutumia data kutoka eneo la Kabete ni kuwa; lugha kimatendo, ni tofauti na data ya maandishi.

Tunakubaliana na Arlotto (1972) ambaye anasizitiza umuhimu wa kukusanya data, katika uasilia wake.

Kwa sababu hiyo, tumelinganisha pamoja, data isiyo- tofauti. Moja toka umilisi wa lugha, kwa mujibu wa wazungumzaji - wazaliwa; nyingine kutoka lugha ambayo imesanifishwa kwa sababu za kijamii.

Kama anavyosema Hooper (1976:3):

> "... lengo la utafiti - elezi wa lugha ni kuvyaza sarufi ya lugha. Sarufi hiyo ni wakilisho la ujuzi ambao mzungumzaji - mzaliwa anao ..."[8]

Akimalizia maelezo haya anasema:

> "Ujuzi huu unaitwa umilisi"[9]

TANBIHI

1. S.A. Schane, (1973). "Natural Rules in Phonology" katika Robert P. Stockwell na Ronald K.S. Macaulay (eds) Linguistic change and Generative Theory. Bloomington. Indiana University Press. 208.

2. L.M. Hyman, (1975): Phonology : Theory and Analysis. New York: Holt, Rhinehart and Winston. 173.

3. ————, (opp cit) 163.

4. ————, (opp cit) 164

5. S.A. Schane, (opp cit) 207.

6. J.B. Hooper, (1976): An Introduction to Natural Generative Phonology. New York. Academic Press. 201.

7. ————, (opp cit). 201

8. Kithaka wa Mberia, (1981): The Consonants of Kitharaka. M.A. Thesis. University of Nairobi. 55

9. J.B. Hooper, (opp cit). 3.

## 4.0.0. SURA YA NNE. ULINGANISHI

## UTANGULIZI

Katika sura hii, tunadhamiria kulinganisha halia za kisauti katika Kiswahili sanifu na Kikikuyu sanifu.

Kwa upande mwingine, tungependa kutilia nguvu kauli kwamba, Kikikuyu cha Kabete, katika kiwango cha fonolojia, ni sawa na Kikikuyu sanifu.

Ilidhihirika kuwa lahaja hizi mbili hazina tofauti, katika viwango vya sauti, au fonetiki, na mofolojia, katika 1.0.0.

Kama tulivyofanya katika sura zile mbili, tutajadilia ulinganishi huu chini ya mada zile za mpangilio wa sheria za kifonolojia kwa mujibu wa Schane (1973).

Mada hizi hi sheria za muundo wa silabi unaopendekezwa; sheria za uwiano, sheria za kudhoofika kwa sauti, na sheria za kukazana kwa sauti.

### 4.1.0 SHERIA ZA MUUNDO WA SILABI UNAOPENDEKEZWA

Katika Kiswahili sanifu, halia za kuundwa kwa nusu-vokali, ukakaaishaji na kudondoshwa vokali zinadhihirika katika jumla ya sheria za muundo wa silabi unaopendekezwa.

Halia hizi zinajitokeza katika Kikikuyu sanifu pamoja na Kikikuyu cha Kabete. Hii ni kauli ambayo itaendelea kuthibitika, kila tutakaporejelea mabadiliko yenyewe.

### 4.1.1 KUUNDWA KWA NUSU-VOKALI

Katika Kiswahili sanifu, nusu-vokali inaelekea kuundwa katika mazingira enezi zaidi kuliko Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete.

Kiswahili sanifu kimethibiti kuundwa kwa nusu-vokali katika ngeli ya 1. {mu -} kama vile:

| Umbo ndani | | umbo nje | maana |
|---|---|---|---|
| /mu + izi/ | ⟶ | [mwizi] | 'mwizi' |
| /mu + ɛnzi/ | ⟶ | [mwɛnzi] | 'mwenzi' |

Pamoja na ngeli ya 1, zipo ngeli nyingine ambazo zinadhihirisha halia hii. Ni kama vile 3, 11, 15, 17, 18 na viambishi vya umilikaji.

Mifano ni kama vile:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /mu + aka / | ⟶ | [mwaka] | 'mwaka' |
| /u + ɛmbɛ/ | ⟶ | [wɛmbɛ] | 'wembe' |
| /ku + imba / | ⟶ | [kwimba] | 'kwimba' |
| /ku + iŋgi / | ⟶ | [kwiŋgi] | 'kwingi' |
| /mu + ɛmbamba/ | ⟶ | [mwɛmbamba] | 'mwembamba' |

Ngeli ya 8 pia inaonyesha kuundwa kwa nusu-vokali. Mifano ni:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /vi + akula / | ⟶ | [vyakula] | 'vyakula' |
| /vi + ɔmbɔ / | ⟶ | [vjɔmbɔ] | 'vyombo' |

Viambishi vya umilikaji vinavyoonyesha kuundwa kwa nusu-vokali ni kama vile:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /i + angu/ | ⟶ | [jaŋgu] | 'yangu' |
| /i + akɔ/ | ⟶ | [jakɔ] | 'yako' |
| /vi + ɛtu / | ⟶ | [vjɛtu] | 'vyetu' |
| /vi + ɛnu / | ⟶ | [vjɛnu] | 'vyenu' |

Halia hii si enezi vile, katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete. Katika lugha hii, nusu-vokali inaelekea kuundwa katika ngeli za 1, 3, na 15, na katika viambishi vya umilikaji kama vile {ro -}, {o-} na {e-}. Mifano ni kama vile:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /mo + ana / | ⟶ | [mwana] | 'mtoto' |
| /mo + isi / | ⟶ | [mwoiʃi] | 'mwizi' |
| / mo +ɛri] / | ⟶ | [ mwɛri ] | 'mwezi' |
| / me +ɛri / | ⟶ | [ mjɛri ] | 'miezi' |
| /ro + akwa / | ⟶ | [ jakwa ] | 'yangu' |
| /e + a+ɔ / | ⟶ | [ jaɔ ] | 'yao' |
| /e + akwa/ | ⟶ | [ jakwa ] | 'yangu' |

Mazingira ya 1, 3, 15 na viambishi vya umilikaji yanalingana na yale ya Kiswahili sanifu, isipokuwa Kiswahili sanifu kinaundia nusu-vokali katika mazingira mapana zaidi.

### 4.1.2 KUDONDOSHWA KWA VOKALI

Kwa mara ya pili, halia inaonekana kuenea zaidi katika Kiswahili sanifu kuliko Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete.

Halia yenyewe ni kudondoshwa kwa vokali ambayo inaelekea kuundwa katika ngeli za 2, 3, 6, 7, na 16. Mifano ni kama:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /mu + gawɛ/ | ⟶ | [ m̩gawɛ ] | 'mgawe' |
| /mu + hindi/ | ⟶ | [ m̩hindi ] | 'mhindi' |
| /wa + ɛnzi/ | ⟶ | [ wɛnzi ] | 'wenzi' |
| /ji + ambɔ/ | ⟶ | [ ǰambɔ ] | 'jambo' |
| /pa + iŋginɛ/ | ⟶ | [ peŋginɛ ] | 'pengine' |

Pronomino ya nafsi ya pili wingi, {mu -} pia inaonyesha kudondoshwa kwa vokali.

Mazingira mengineyo ambayo yanaelekea kusheheni fenomena hii ni mofimu ya kukanusha, {ha -}

Tukitoa mifano michache tunapata:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ha + ku+ɛnda/ | ⟶ | [ hakwɛnda ] | 'hakwenda' |
| /ha + ku+iŋgia/ | ⟶ | [ hakwiŋgia ] | 'hakuingia' |

Vile vile, vipo vionyeshi ambavyo vinadhihirisha kupotea kwa vokali. Ni kama vile:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /hu + ju+ɔ/ | ⟶ | [ hʊjɔ ] | 'huyo' |
| /ha + wa+ɔ/ | ⟶ | [ haɔ ] | 'hao' |
| /hu + ju+ɔ/ | ⟶ | [ huɔ ] | 'huo' |
| /hi + li+nɔ/ | ⟶ | [ hilɔ ] | 'hilo' |
| /ha + ja+ɔ/ | ⟶ | [ haja ] | 'haya' |

how about ½ vokali /w

Kama tulivyotaja tayari hapo juu, hakuna mifano yo-yote ya kudondoshwa kwa konsonanti katika Kiswahili sanifu hata kama ipo katika lahaja nyingine za Kiswahili kama vile Kivumba na Chi - chifundi.

Kwa hivyo tunayo sababu ya kusema kuwa Kikikuyu sanifu, na Kikikuyu cha Kabete kimejipekeesha na Kiswahili sanifu kwa mujibu huu.

### 4.1.4 UKAKAAISHAJI

Mfanyiko huu umeelekea kujitokeza katika lugha zote mbili. Kiswahili sanifu kwa upande mmoja na Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete; kwa upande mwingine.

Kiswahili sanifu kimedhihirisha halia hii katika ngeli ya 7, na viambishi vya umilikaji kama {ki-} na vionyeshi kama vile hicho'.

Mifano ya ukakaaishaji katika ngeli ya 7, na viambishi vya umilikaji ni kama vile:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ki + ɔmbɔ/ | ⟶ | [ čɔmbɔ ] | 'chombo' |
| /ki + ɛtɛzɔ/ | ⟶ | [ čɛtɛzɔ ] | 'chetezo' |
| /ki + ura/ | ⟶ | [ čura ] | 'chura' |
| /ki + andalua/ | ⟶ | [ čandalua ] | 'chandalua' |
| /ki + akɔ/ | ⟶ | [ čakɔ ] | 'chako' |
| /ki + aɔ/ | ⟶ | [ čaɔ ] | 'chao' |

Kiswahili sanifu kinathibiti mazingira mapana zaidi, kwa kuwa ukakaaishaji unapatikana katika ngeli moja, mofimu za umilikaji na vionyeshi.

Licha ya Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete kuonyesha ukakaaishaji katika mazingira ya nafsi ya kwanza pekee, mazingira haya yanaelekea kuzaa zaidi, kuliko yale ya Kiswahili sanifu. Mifano ni kama vile:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /n + ariɛ/ | ⟶ | [ $^{n}$ǰariɛ ] | 'nizungumze' |
| /n + ənererɛ/ | ⟶ | [ ɲanererɛ ] | 'nipase sauti' |
| /n + ɛdɛ/ | ⟶ | [ ɲɛ$^{n}$dɛ ] | 'nipende' |
| /n + $^{n}$jɛ/ | ⟶ | [ ɲɛ$^{n}$ǰɛ ] | 'ninyoe' |
| /n + imɛ/ | ⟶ | [ ɲimɛ ] | 'ninyime' |
| /n + ɔnɛ/ | ⟶ | [ ɲɔnɛ ] | 'nione' |

| | | | |
|---|---|---|---|
| /hi + +zi+ɔ / | ⟶ | [ hizi ] | 'hizi' |
| /hu + +ku+ɔ | ⟶ | [ hukɔ ] | 'huko' |
| /ha + +pa+ɔ / | ⟶ | [ hapɔ ] | 'hako' |
| /hu + +mu+ɔ / | ⟶ | [ humɔ ] | 'humo' |

Halia hii hainonekani kuenea vile katika mazingira mapana vile, katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete.

Inathibitika katika mazingira ambapo pronomino ya nafsi ya kwanza {a-} na ya nafsi ya pili wingi, {ma-}, pekee. Katika Kiswahili sanifu, fenomena hii ni enezi zaidi, kwani ikienea katika ngeli za 2, 3, 6, 7, na 16; pamoja na pronomino, na mofimu ya kukanusha.

Mifano ya vokali kudondoshwa katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete ni:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /a +ma+ɔɛrɛ / | ⟶ | [ amɔɛrɛ ] | 'awachukulie' |
| /a +ma+etɛ/ | ⟶ | [ amɛtɛ ] | 'awaite' |
| /ma +ma+erɛ / | ⟶ | [ mamɛrɛ ] | 'wawaambie' |

4.1.3 KUDONDOSHWA KWA KONSONANTI

Halia hii zikuthi katika Kiswahili sanifu. Imejitokeza katika Kikikuyu sanifu, na Kikikuyu cha Kabete.

Konsonanti ambazo zimeelekea kudondoshwa ni [n] na [r]. Mazingira ambayo yamethibiti mfanyiko ni kabla ya mofimu ya nafsi ya kwanza umoja, {n-}.

Mifano ambayo tumeitoa ni kama vile:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /n +nuŋgɛ / | ⟶ | [ nuŋgɛ ] | 'ninuke' |
| /n +ɲɔtɛ / | ⟶ | [ ɲɔtɛ ] | 'nione kiu' |
| /n +makiɛ / | ⟶ | [ makiɛ ] | 'nishtue' |
| /n +remɛ/ | ⟶ | [ nɛmɛ ] | 'nilime' |
| /n +riŋgɛ/ | ⟶ | [ niŋgɛ ] | 'nigonge' |
| /n +romɛ/ | ⟶ | [ nomɛ ] | 'niume' |

| | | | |
|---|---|---|---|
| /n + ɑmɛ/ | ⟶ | [ ɲɑmɛ ] | 'nikauke' |
| /n + umɛ/ | ⟶ | [ ɲumɛ ] | 'nitoke' |

Halia hii inajitokeza kabla ya mashina ya vitenzi ambayo yanaanza kwa vokali:

$$\left\{\begin{bmatrix} a \\ e \\ i \\ ɔ \\ u \end{bmatrix}\right\}$$

4.2.0 SHERIA ZA UWIANO

Chini ya jumla ya sheria hizi tunanuia kulinganisha mifanyiko kama kuathiriwa kwa nasali kuhusu mahali pa kutamkia sifa ya ughuna, isoghuna na uwiano wa vokali.

4.2.1 KUATHIRIWA KWA NASALI KUHUSU MAHALI PA KUTAMKIA

Tofauti ambayo imejitokeza kwa uwazi kabisa kuhusu halia hii, kati ya Kiswahili sanifu kwa upande mmoja, na Kikikuyu sanifu, pamoja na Kikikuyu cha Kabete kwa upande mwingine ni kuwa kuathirika kwa nasali katika Kiswahili sanifu ni halia ya kofonolojia ilhali halia hiyo ni ya kimofofonolojia, katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete vile vile.

Katika Kiswahili sanifu, nasali inaathirika kuhusu mahali pa kutamkia, kote katika ngeli ya tisa. Mifano ni kama vile:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /n + bɛgu / | ⟶ | [ mbegu ] | 'mbegu' |
| /n + vua / | ⟶ | [ ɱvua ] | 'mvua' |
| /n + dɔgo / | ⟶ | [ ndɔgɔ ] | 'ndogo' |
| /n + ǰia / | ⟶ | [ ɲǰia ] | 'njia' |
| /n + gumu / | ⟶ | [ ŋgumu ] | 'ngumu' |
| /n + ti / | ⟶ | [ nči ] | 'nchi' |
| /n + gwɛ / | ⟶ | [ ŋgwɛ ] | 'ngwe' |

Tofauti iliyopo ni kuwa katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete; pamoja na kuathirikwa katika nomino fulani katika ngeli ya tisa, nasali inaathiriwa pia, katika mazingira mengineyo. Mazingira yenyewe ni kiambishi cha pronomino ya nafsi ya kwanza umoja {n-} kinapotangulia mashina mbalimbali ya vitenzi. Jumla ya mifano ni: .

| | | | |
|---|---|---|---|
| /n + ama/ | ⟶ | [ ɲama ] | 'nyama' |
| /n + gɔdu/ | ⟶ | [ ŋɔdu ] | 'kondoo' |
| /n + gui/ | ⟶ | [ ŋgui ] | 'mbwa' |
| /n + ɔɛ/ | ⟶ | [ ɲǰɔɛ ] | 'nichukue' |
| /n + kerɛ/ | ⟶ | [ ŋgerɛ ] | 'nivuke' |
| /n + kɛrɛ/ | ⟶ | [ ŋgɛrɛ ] | 'nikatekate' |
| /n + ɣiɛ/ | ⟶ | [ ŋgiɛ ] | 'nisumbue' |
| /n + gaɛ/ | ⟶ | [ ŋgaɛ ] | 'nigawe' |
| /n + ɣarorɛ/ | ⟶ | [ ŋgarorɛ ] | 'nigeuze' |

## 4.2.2 SIFA YA UGHUNA

Kama ilivyo halia ya kudondoshwa kwa konsonanti, sifa au halia ya sauti fulani kupata sifa ya ughuna imejitokeza katika Kikikuyu sanifu, pamoja na Kikikuyu cha Kabete.

Fenomena hiyo haikudhihirika katika Kiswahili sanifu.

Katika Kikikuyu, mfanyiko huu unathibitika katika pronomino ya nafsi ya kwanza umoja {n-} inapotangulia mashina ya vitenzi mbalimbali, na ngeli ya 14.

Mifano ni kama vile:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /n + kimɛ/ | ⟶ | [ ŋgimɛ ] | 'niponde' |
| /n + kɔmɛ/ | ⟶ | [ ŋgɔmɛ ] | 'nilale' |
| /n + kirɛ/ | ⟶ | [ ŋgirɛ ] | 'ninyamaze' |
| /n + kuɲɛ/ | ⟶ | [ ŋguɲɛ ] | 'nichune' |
| /n + kedɛ/ | ⟶ | [ ŋgedɛ ] | 'nisuke' |
| /n + twarɛ/ | ⟶ | [ $^{n}$dwarɛ ] | 'niugue' |
| /n + terɛ/ | ⟶ | [ $^{n}$derɛ ] | 'nikose kuhudhuria' |
| /n + to:rɛ/ | ⟶ | [ $^{n}$dɔrɛ ] | 'niishi milele' |

| | | | |
|---|---|---|---|
| /n + tore/ | ⟶ | [ ⁿdorɛ ] | 'nitoboe shimo' |
| /ko + +e+tɛma/ | ⟶ | [ gwetɛma ] | 'kujikata' |
| /ko + +e+šɔkia/ | ⟶ | [ gwešɔkia ] | 'kujinung'unikia' |
| /ko + +e+ɣokia/ | ⟶ | [ gweɣokia ] | 'kujiharibu' |

## 4.2.3 SIFA: ISO-GHUNA

Vile vile, hali ya sauti fulani kupoteza ughuna wake katika umbo la nje, ilhali sifa ya ughuna ilikuwemo katika umbo ndani, inajitokeza katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete tu, wala haielekei kujidhihirisha katika Kiswahili sanifu.

Mifano ya kupotea kwa ughuna inapatikana katika ngeli ya 12, na mofimu inayoleta dhana ya ukubwa {ke-}, inapotangulia majina mbalimbali katika lugha ya Kikikuyu.

Mifano ni:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ka + ɴ +kari/ | ⟶ | [ gakari ] | 'kijigari' |
| /ka + ɴ +kwarɛ/ | ⟶ | [ gakwarɛ ] | 'kijikware' |
| /ka + ɴ +kɔma/ | ⟶ | [ gakɔma ] | 'kijishetani' |

Kabla hatujaendelea na mifano, tungependa kutaja kuwa, ni kama tulivyoeleza katika 3.2.3, kwamba sauti zinazopoteza ughuna, si zile za mwanzo wa nomino zile, bali mofimu ya pili kutoka mwanzo wa nomino, fonimu za mwanzo za ngeli.

Mifano iliyobakia ni:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ka + ɴ +tuma/ | ⟶ | [ getuma ] | 'giza totoro' |
| /ka + ɴ +tɛɣɛ/ | ⟶ | [ getɛɣɛ ] | 'jidege |
| /ka + ɴ +tutu/ | ⟶ | [ getutu ] | 'jitekenya' |

## 4.2.4 UWIANO WA VOKALI

Kuhusu fenomena hii, Kiswahili sanifu na Kikikuyu sanifu, pamoja na Kikikuyu cha Kabete zinafananisha mazingira, ya kuathiriwa kwa vokali kwa upande wake.

Katika Kiswahili sanifu, vokali ambayo ipo katika mzizi wa kitenzi inaathiri vokali iliyopo katika mofimu ya kunyambua kitenzi.

Lakini lahaja zile za Kikikuyu zinathibiti vokali kuathiriana, katika mazingira ya kunyumbua vitenzi, na kuundwa kwa nomino pia.

Tutaanza kwa mifano ya athari hii ya vokali, kwanza katika Kiswahili sanifu. Ni kama vile:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ib+i+an+a/ | ⟶ | [ ibiana ] | 'ibiana' |
| /ɛnd+ +a/ | ⟶ | [ ɛndɛa ] | 'endea' |
| /kat+ik+a/ | ⟶ | [ katika ] | 'katika' |
| /sɔm+ɛk+a/ | ⟶ | [ sɔmɛka ] | 'someka' |
| /sɔm+an+a/ | ⟶ | [ somana ] | 'somana' |
| /um+i+an+a/ | ⟶ | [ umiana ] | 'umiana' |
| /čɛk+ɛw+a/ | ⟶ | [ čɛkɛwa ] | 'chekewa' |
| /čɔm+ɔk+a | ⟶ | [ čɔmɔka ] | 'chomeka' |
| /fuŋg+am+a/ | ⟶ | [ fuŋgama ] | 'fungama' |

Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete, katika mazingira ya kunyambua vitenzi zina:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ug+ura/ | ⟶ | [ ugera ] | 'sɛmea' |
| /roŋg+vra/ | ⟶ | [ roŋgera ] | 'nyoshea' |
| /kɛn+vra | ⟶ | [ kɛnɛra ] | 'furahia' |
| /rɔg+vra/ | ⟶ | [ rɔgɛra ] | 'rogea' |

V. inasimamia vokali.

Kuhusu kuathiriana kwa vokali katika uundaji wa nomino kutokana na vitenzi tunapata mifano katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete. Ni kama vile:

| kitenzi | | Nomino | Nomino |
|---|---|---|---|
| /ko + iɣa/ | ⟶ | [ moiɣerɛ ] | 'namna ya kuweka' |
| /ko + ɣoria/ | ⟶ | [ moɣɔrɛriɛ ] | 'namna ya kuchokoza' |
| /ko + ɔha/ | ⟶ | [ keɔhɔ ] | 'kifungo' |
| /ko + taŋgɔ / | ⟶ | [ getaŋgɔ ] | 'usumbufu' |
| /ko + e+era / | ⟶ | [ mweierɔ ] | 'hiari' |

| KITENZI | | NOMINO | NOMINO |
|---|---|---|---|
| /ko + oma / | ⟶ | [ o:mo ] | 'ugumu' |
| /ko + ira / | ⟶ | [ oiro ] | 'weusi' |

Vile tunavyoweza kusema, kuhusu halia hii, ni kuwa, katika lugha zote zile; Kiswahili sanifu, Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete, mazingira ya unyambuaji wa vitenzi yanaelekea kunawiri.

Tofauti iliyopo ni kuwa Kikikuyu kinaeneza fenomena hiyo katika mazingira mengineyo; uundaji wa nomino.

Tofauti nyingineyo ni kuwa Kikikuyu kinathibiti mifano ya uwiano kamili ya sifa { ± } [mbele], pamoja na sifa ya [urefu]. Uwiano kamili haujitokezi katika Kiswahili sanifu, ila nusu-uwiano.

Mifano ile ya uwiano kamili katika Kikikuyu sanifu, na Kikikuyu cha Kabete ni:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ko + ɔrɔr+ɔa / | ⟶ | [ wɔrɔrɔ ] | 'ulainifu' |
| /ko + oma/ | ⟶ | [ o:mo ] | 'ugumu' |

## 4.2.5 MVUTANO WA VOKALI

Mvutano wa vokali ni fenomena ambayo inahusu vokali mbili zenye urefu tofauti kuathiriana, ili kiwango cha urefu kiwe kingine kabisa, kisicho cha zo-zote kati ya vokali asili zinazohusika.

Mchoro wetu katika sehemu ya 2.2.1 unathibitisha dai hili kwa uwazi zaidi.

Halia hii imejitokeza katika Kiswahili sanifu katika ngeli za 2, 6 na 16; bila kujithibiti katika, au Kikikuyu sanifu ama Kikikuyu cha Kabete.

Kwa hivyo Kiswahili sanifu kimejipekeesha, tokana na Kikikuyu, kwa halia hii.

Mifano ni kama vile:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /wa + ɛzi/ | ⟶ | [ wɛzi ] | 'wezi' |
| /wa + ɛnzi: / | ⟶ | [ wɛnzi: ] | 'wenzi' |
| /ma + ikɔ/ | ⟶ | [ mɛkɔ ] | 'meko' |
| /ma + inɔ/ | ⟶ | [ mɛnɔ ] | 'meno' |
| /pa + iŋgi:/ | ⟶ | [ pɛŋgi: ] | 'pengi' |

| | | | |
|---|---|---|---|
| /pa + 'iŋgine/ | ⟶ | [ pɛŋginɛ ] | 'pengine' |

## 4.3.0 KUDHOOFIKA KWA SAUTI

Kudhoofika kwa sauti kumejitokeza katika Kiswahili sanifu pekee kwa mujibu wa ulinganishi wetu, wala hakukujithibiti katika, au Kikikuyu sanifu ama Kikikuyu cha Kabete.

Kabla ya kuingilia mifano, tunaona ikiwa muhimu kuonyesha jumla ya mabadiliko haya, katika Kiswahili sanifu. Jumla ya mabadiliko ya kudhoofika kwa sauti ni:

$$\begin{bmatrix} k \\ \check{j} \\ d \\ j \\ g \\ k \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} \check{s} \\ z \\ z \\ \check{s} \\ \check{j} \\ f \end{bmatrix}$$

Tukithibitisha kwa mifano, tutapata:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /mu + ǰɛŋgi/ | ⟶ | [ m̩ǰɛnzi ] | 'mjenzi' |
| /mu + fuati/ | ⟶ | [ m̩fuasi ] | 'mfuati' |
| /mu + čɛki/ | ⟶ | [ m̩čɛši ] | 'mcheshi' |
| /mu + piki/ | ⟶ | [ m̩piši ] | 'mpishi' |
| /mu + pɛndi/ | ⟶ | [ m̩pɛnzi ] | 'mpenzi' |
| /cek + +j+a/ | ⟶ | [ čɛša ] | 'chesha' |
| pit + +j+a/ | ⟶ | [ piša ] | 'pisha' |
| /mu + s mtagi/ | ⟶ | [ m̩sɔmaǰi ] | 'msomaji' |
| /mu + fug+aǰi/ | ⟶ | [ m̩fugaǰi ] | 'mfugaji' |

## 4.4.0 KUKAZANA KWA SAUTI

Fenomena hii haikuelekea kunawiri katika Kiswahili sanifu, kama ilivyoelekea kuwa katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete.

Sauti zinazokazana katika Kiswahili sanifu ni:

$$\begin{bmatrix} l \\ l \\ l \\ r \\ w \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} z \\ v \\ d \\ d \\ b \end{bmatrix}$$

Mifano ya kukazana kwa sauti ni kama vile:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /mu + kal+i/ | → | [ m̩kazi ] | 'mkazi' |
| /mu + lɛl+i/ | → | [ m̩lezi ] | 'mlei' |
| /mu + zal+i/ | → | [ m̩zazi ] | 'malezi' |
| /u +tulil+u/ | → | [ utulivu ] | 'utulivu' |
| /u +ɔKɔl+u/ | → | [ wɔkɔvu ] | 'wokovu' |
| /n + limi/ | → | [ ndimi ] | 'ndimi' |
| /n + rɛfu/ | → | [ ndɛfu ] | 'ndefu' |
| /n + wili/ | → | [ mbili ] | 'mbili' |

/l/ hii haipo tena katika mashina ya nomino, hivi leo.
Jumla ya kukazana kwa sauti katika Kikikuyu sanifu cha Kabete-ni:

$$\begin{bmatrix} r \\ \beta \\ \check{s} \end{bmatrix} \longrightarrow \begin{bmatrix} d \\ b \\ \check{j} \end{bmatrix}$$

Mifano ni kama:

| | | | |
|---|---|---|---|
| /n + rugɛ/ | → | [ $^{n}$dugɛ ] | 'nipike' |
| /n + rerɛ/ | → | [ $^{n}$derɛ ] | 'nilie' |
| /n + rɔrɛ/ | → | [ $^{n}$dɔrɛ ] | 'niangalie' |
| /n + rašiɛ/ | → | [ $^{n}$dašiɛ ] | 'nitoe mahari' |
| /n + roɛ/ | → | [ $^{n}$doɛ ] | 'nipigane' |
| /n + βerɛ/ | → | [ $^{h}$bɑrɛ ] | 'nilainishe supu' |
| /n + βutɛ/ | → | [ $^{h}$butɛ ] | 'nitoe manyoya' |
| /n + šiarɛ/ | → | [ $^{n}$ǰiarɛ ] | 'nizae' |
| /n + sɔkiɛ/ | → | [ $^{n}$ǰɔkiɛ ] | 'nirudishe' |

| | | | |
|---|---|---|---|
| / n+šukɛ / | ⟶ | [ $^n$ǰukɛ ] | 'nisengenye' |
| / n+sɛǰiɛ / | ⟶ | [ $^n$ǰɛǰiɛ ] | 'nibadilishe' |
| / n+šanorɛ / | ⟶ | [ $^n$ǰanorɛ ] | 'nichane' |
| / n+šɛrɛrɛ / | ⟶ | [ $^n$ǰɛrɛrɛ ] | 'nitembelee' |
| / n+šɔrɛ / | ⟶ | [ $^n$ǰɔrɛ ] | 'nichore' |
| / n+šariɛ / | ⟶ | [ $^n$ǰariɛ ] | 'nitafute' |
| / n+širɛ / | ⟶ | [ $^n$ǰi:rɛ ] | 'nikesi' |
| / n+šidɛ / | ⟶ | [ $^n$ǰi:dɛ ] | 'nishinde' |
| / n+saŋgɛ / | ⟶ | [ $^n$ǰaŋgɛ ] | 'niranda-rande' |
| / n+šuriɛ / | ⟶ | [ $^n$ǰuriɛ ] | 'ŋining'inize' |

Licha ya kuwa Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete kinaonyesha kukazana kwa sauti kabla ya mofimu ya pronomino ya nafsi ya kwanza umoja pekee {n-}, mifano inaelekea kuwa marudufu.

## 4.5.0 HITIMISHO

Tungependa kumulikia aina ya ulinganifu, ambao umejitokeza katika sura hii, kati ya Kiswahili sanifu na Kikikuyu sanifu, ambacho kimejitokeza kufanana na Kikikuyu cha Kabete, katika kiwango cha fonolojia.

Nusu-vokali ilielekea kuundwa katika mazingira mapana zaidi katika Kiswahili sanifu kuliko ilivyo katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete.

Katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete, nusu vokali imeundwa katika mazingira sawa.

Kwa njia ile ile, kudondoshwa kwa vokali kunaonekana kuenea zaidi katika Kiswahili sanifu kuliko katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete.

Vokali inadondoshwa katika mazingira yale yale, katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete kwa upande wake, na Kiswahili sanifu kwa upande mwingine ni kudondoshwa kwa konsonanti.

Mfanyiko huu haupo, katika Kiswahili sanifu, hata kama upo, katika lahaja nyinginezo za Kiswahili kama vile Chi-chifundi na Kivumba.

Ukakaaishaji ndiyo fenomena pekee ambayo inaelekea kuenea karibu sawa katika Kiswahili sanifu na Kikikuyu sanifu, pamoja na Kikikuyu cha

Kabete. Kiswahili sanifu kinayo mazingira mengi zaidi, lakini mazingira hayo hayakuthibiti mifano mingi.

Kikikuyu cha Kabete na Kikikuyu sanifu kwa upande mwingine hazikuwa na mazingira mengine isipokuwa kabla ya pronomino ya nafsi ya kwanza umoja {n-}, lakini mazingira hayo yana mifano mingi. Ndiyo sababu yetu ya kusema kuwa halia imeenea kwa njia karibu sawa.

Kuhusu kuathirika kwa nasali kuhusu mahali pa kutamkia, inabainika kuwa mfanyiko huu ni wa kifonolojia katika Kiswahili sanifu. Msingi wake ni wa sifa ya kifonetiki tu.

Lakini katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete kuathirika kwa nasali ni halia ya kimofofonolojia. Kwa maana ya kuwa kinachochochea mfanyiko huu, sio sifa ya msingi wa kifonetiki tu, bali pia mazingira ya kimofolojia.

Athari za sauti fulani kupata sifa ya ughuna, ambao kupoteza sifa ya ughuna ni jambo ambalo linajitokeza katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete pekee. Athari hii haijitokezi kamwe katika Kiswahili sanifu.

Mvutano wa vokali nao unajitokeza katika Kiswahili sanifu pekee. Haushuhudiwi katika, ama Kikikuyu sanifu, au Kikikuyu cha Kabete.

Tofauti nyingine ambayo inajitokeza kati ya Kiswahili sanifu na kwa upande wa pili Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete ni kuhusu uwiano wa vokali.

Uwiano huu unajitokeza katika mazingira ya kuunda nomino kutokana na vitenzi, katika Kikikuyu sanifu, pamoja na Kikikuyu cha Kabete. Vokali haielekei kuathiriana katika mazingira haya, katika Kiswahili sanifu.

Ijapokuwa, katika Kiswahili sanifu, na vile vile Kikikuyu cha Kabete, pamoja na Kikikuyu sanifu katika kunyambua vitenzi, vokali iliyopo katika mzizi wa kitenzi, imeelekea kuiathiri vokali iliyopo katika mofimu ya mnyambuliko.

Kudhoofika kwa sauti ndiyo fenomena nyingine ambayo imejitokeza katika Kiswahili sanifu, bila kujitokeza katika Kikikuyu sanifu, au Kikikuyu cha Kabete.

Halia ya mwisho, ambayo ni kukazana kwa sauti, imethibitika kote kote, pia. Lakini imeelekea kuenea karibu sawa katika lahaja zote, yani Kiswahili sanifu, Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete.

Katika halia zote za kisauti zile zilizothibitika katika Kikikuyu sanifu zimethibitia, vile vile, katika Kikikuyu cha Kabete, na katika mazingira sawa kabisa.

## 5.0.0 SURA YA TANO

Mwanzoni mwa kazi hii, tulisema kuwa nia yetu ni kufanya utafiti wa kiwakati.

Hivi ni kama kusema kuwa historia haikupewa nafasi katika upeo wetu.

Sababu mojawapo ni kuwa hali nyingi za kisauti ambazo tumezishughulikia zinaelekea kuimarisha misingi yake katika nadharia yetu, na maelezo ya kiwakati, kuliko kimapisi.

Hatuoni sababu yenye mantiki, kwa hivyo, ya kulazimisha historia katika maelezo yetu ilhali haiafiki, kote kote.

Tatu ni kuwa wakati nao hauturuhusu. Kwa sababu hiyo, kile ambacho tutakieleza, katika sura hii, ni uasilia wa fenomena za kisauti, ambazo zimejitokeza katika Kiswahili sanifu, Kikikuyu sanifu ambacho kina mzungumzaji - mzaliwa; Kikikuyu cha Kabete.

Lakini kabla hatujafanya hivyo, tungependa kueleza kwa ufupi, dhana ya uasilia, kama inavyofasiliwa miongoni mwa wana-isimu, na jukumu la nadharia asilia zalishi, ambayo ndiyo mhimili wa nadharia ambayo tumeitumia: fonolojia asilia zalishi.

### 5.1.0 JUKUMU LA FONOLOJIA ASILIA ZALISHI

Kama tulivyoeleza katika 2.0.0, lengo la nadharia zalishi, kwa mujibu wa Hooper (1976:3) ni kuandika sarufi. Kama anavyosema, jukumu la nadharia zalishi ni kuandika sarufi inayowakilisha umilisi wa mzungumzaji - mzaliwa, ambao unamwezesha kuelewa idadi iso-ukomo ya sentensi, katika lugha yake.

Katika kutekeleza jukumu hilo, sarufi tunayoiandika inawakilisha umilisi huu. Wanatuonya; Chomsky (1964) na Chomsky na Halle (1968) kuhusu kutotegemeka kwa utendaji.

Kwa hivyo, lengo la sarufi zalishi ni umilisi, wala sio utendaji wa lugha.

Ikiwa tutaendeleza wazo hili kwa kumnukuu Hooper (1976:3) anaelekea kusema;

> "Katika sarufi zalishi, umilisi wa kiismu unaweza kuwakilishwa katika mfumo wa sheria ambazo zinaonyesha uhusiano wa sauti na maana ambao unatumiwa katika lugha. Sarufi, basi, inastahili kufasili seti ya sheria ambazo ziko katika ilhamu ya

mzungumzaji, ambazo amezijua, na ambazo
zinamwezesha kutumia lugha yake"[1]

Kwa sababu hiyo, lengo moja la sura hii ni kuonyesha mfumo wa kaida au sheria zilizoko katika jumla ya halia za kifonolojia,katika Kiswahili sanifu; Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete.

Katika kutekeleza haya Hooper (1976:133) anaeleza:

"Nadharia yenyewe ni lazima ionyeshe, hasa, seti ya
Sheria ambazo zina msingi wake katika mazingira ya
kifonetiki katika lugha yo-yote."[2]

Lakini jukumu hili halikosi kukabiliwa na matatizo, kama ilivyo kawaida ya nadharia nyingi, ifikapo kuzionyesha kiutekelezi.

Chambilecho Hooper (1976:133):

"Seti hiyo inaweza kuwa kubwa, lakini, bila shaka ina
ukomo, kwani ikijulikana kuwa baadhi ya halia zile
aghalabu; mathalani hutekelezwa, tena na tena, kutoka
lugha moja hadi lugha nyingine."[3]

Kwa hivyo si jambo la ajabu kupata mifanyiko ya kisauti ikishabihiana toka lugha moja hadi nyingine.

Ikiwa sura hii ina lengo - pacha; lengo la pili, katika sura hii, ni kuonyesha uasilia wa halia zote za kisauti ambazo zimethibitika katika Kiswahili sanifu, Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete .

Tunasema kwa pamoja kwa sababu tulilinganisha mabadiliko yale, katika sura ya nne, na kwa hivyo hatuoni sababu ya kuirejelea mifanyiko ile, kiulinganishi.

Halia zilizojitokeza katika lugha ambazo tumezitafitia ni aina mbili.

(i) Zile ambazo zina maelezo yake katika misingi ya kifonetiki, au sifa za kifonolojia pekee.

(ii) Zile ambazo zina maelezo yake katika misingi mingineyo, kama vile mipaka ya maneno, mipaka ya mofimu ambayo ina misingi yake katika sintaksia au semantiki.

Kategoria hizi za kimofolojia, kisintaksia, na Kisemantiki hazihusishiki, kwa njia ya moja kwa moja, na sifa za kifonetiki.

Kwa kurejelea sheria (i) na (ii) tunatarajia kuwa nadharia yetu itaweza kutoa maelezo kamili, kuhusu sheria hizo.

Anayo ya kusema, Hooper (1976:102) kuhusu aina hizi mbili za sheria. Anasema:

> "Ninavyoona mimi, ni kwamba mabadiliko ya kisauti kila mara huchochewa na sababu za kifonetiki na kwa hivyo, pia; katika mazingira ya kifonetiki."[4]

Anaeleza vile sheria za kimofofonolojia, nazo, huibuka katika lugha. Anaeleza, tena; Hooper (1976:102):

> "Zinajaribu (sheria za kifonolojia, ) kutekelezwa kwa ruwaza au mpango maalum, katika lugha zote. Lakini, kati yasheriakuingia katika lugha, na kuimarishwa kwake, mambo mengi yanaweza kutokea ambayo yanaweza kuathiri au kuzuia matokeo ya badiliko la sauti kuwa la kote kote. Na hapo mazingira yasioonyesha kuathiriwa na halia ile; yanajitokeza. Kwa hivyo, kuweko kwa mazingira yasoathiriwa; na athari za kimofosintaksia kunaweza kuelezwa kama matokeo yanayojitokeza katika harakati ya kutelekeza mabadiliko ya Kisauti."[5]

(mabano ni yetu).

## 5.1.1 DHANA YA UASILIA

Inakuwa vigumu kueleza uasilia wa mabadiliko ya kifonolojia bila kutoa fasili ya dhana ya uasilia, kama alivyoieleza Hooper (1976), katika mjadala wake kuhusu uasilia.

Dhana ya uasilia, katika isimu ina mizizi yake mbali kama kwa Wanashule wa Prague kama vile Trubetzkoy.

Na kama wanaisimu walivyoendelea kuchangia dhana hiyo, ndivyo ilivyoendelezwa.

Roman Jakobson aliiendeleza hatua moja mbele, akitegemea kwa kiasi, mchango wa Trubetzkoy, kuhusu uasilia, sambamba na fonetiki.

Katika sifa -bainishi zile za R. Jakobson, dhana ya uasilia kuambatanishwa na sifa za kifonetiki haikufichika.

Nao Chomsky na Halle, katika michango yao mbalimbali, wakaikuza dhana ya uasilia katika fonolojia. Kwao pia, sifa za kifonetiki zilikuwa nguzo dhabiti, katika kuumithilisha uasilia.

Schane (1973) na ambaye Hooper anamnukuu kama mhimili wa msingi wa dhana yake ya uasilia, alijadilia uasilia katika fonolojia.

Hooper (1976:133) anasema kuwa uasilia, katika nadharia yake, una misingi yake katika dhana asili ya uasilia ya Stampe (1969, 1973, a, b); Jakobson (1941 [1968]) na kwa kiasi kikubwa, Schane (1972) ambaye katika (1973) pia ameshiriki katika kutatua utata mwingi uliozunguka dhana ya uasilia.

Hooper (1976:133) anadokeza:

> "Nadharia za uasilia wa sheria zimepata tatizo la aina moja, la kimsingi: ukosefu wa fasili yenye mantiki, kuhusu kile kinachomaanishwa na "uasilia." "[6]

Katika (1976:131) yeye anakiri kwamba dhana yake, ya "uasilia" ni maendeleo ya michango ya wanaisimu, ambao tuliwataja.

Anaelekea kukubaliana na Schane, (1973), kuhusu "uasilia", anaposema:

> "Huku akikabiliwa na mfanyiko, hususan wa kifonolojia, mwana-fonolojia atauita asilia, ikiwa unaweza kuelekeza bayana, kwa maelezo ya misingi ya kifonetiki, kama, kwa mfano kuathiriana kwa sauti kuhusu mahali pa kutamkia kati ya sauti zilizopakana; au mfanyiko utaitwa asilia, ikiwa umepatikana katika lugha kadha, hata kama kichocheo cha kifonetiki hakijulikani"[7]

Dhana hizi mbili ndizo zitakazokuwa vigezo vyetu, katika mizani ya uasilia, ya kupimia halia za kisauti ambazo zimejitokeza katika lahaja zile tulizolinganisha.

## 5.2.0 HALIA ZA KISAUTI

Katika Kiswahili sanifu, mabadiliko ya kisauti ambayo yalijitokeza ni:

(i) Kuundwa kwa nusu-vokali.

(ii) Ukakaaishaji

(iii) Kudondoshwa kwa vokali.

(iv) Mvutano wa vokali.

(v) Mkubaliano wa vokali.

(vi) Kuathiriwa kwa nasali kuhusu mahali pa kutamkia.

(vii) Kudhoofika kwa sauti.
(viii) Kukazana kwa sauti.

5.2.1

Halia za Kifonolojia ambazo zinajitokeza katika Kikikuyu sanifu, nazo ndizo:

(i) Kuundwa kwa nusu-vokali
(ii) Ukakaaishaji.
(iii) Kudondoshwa kwa vokali.
(iv) Kudondoshwa kwa konsonanti zikiwa:
  (a) Nasali
  (b) Vilainisho
(v) Kuathiriwa kwa nasali kuhusu mahali pa kutamkia.
(vi) Sifa ya kupata ughuna.
(vii) Sheria ya Dahl
(viii) Mkubaliano wa vokali.
(ix) Kukazana kwa sauti.

Kikikuyu cha Kabete kimethibiti halia - pacha na Kikikuyu sanifu. Ni zizi hizi:

(i) Kuundwa kwa nusu vokali.
(ii) Ukakaaishaji
(iii) Kudondoshwa kwa vokali
(iv) Kudondoshwa kwa konsonanti.
  (a) Nasali
  (b) Vilainisho
(v) Kuathiriwa kwa nasali kuhusu mahali pa kutamkia.
(vi) Sifa ya kupata ughuna.
(vii) Mkubaliano wa vokali
(viii) Kukazana kwa sauti

Almuradi tutaeleza uasilia wa halia zote za kisauti, kwa pamoja.

Vile tunavyojaribu kusema ni kuwa, kwani mifanyiko ikiwa na uasilia ule ule, iwe ni katika Kiswahili sanifu, au Kikikuyu sanifu, ama Kikikuyu cha

Kabete; hatutaorodhesha kwa orodha tatu,moja ya kila lahaja, bali tutaieleza kwa pamoja, na uasilia wake.

Pia tutaeleza ikiwa sheria yenyewe imejitokeza kama sheria ya kifonolojia, au kimofofonojia, kulingana na lahaja ambayo inapatikana.

Kwa hivyo, tukirejelea Kiswahili sanifu; Kikikuyu sanifu; na Kikikuyu cha Kabete, halia zinazojitokeza, na ambazo tunaelekea kuzishughulikia ni:

(i) Kuundwa kwa nusu-vokali.
(ii) Ukakaaishaji.
(iii) Kudondoshwa kwa vokali.
(iv) Kudondoshwa kwa konsonanti.
(v) Kuathiriwa kwa nasali kuhusu mahali pa kutamkia.
(vi) Mvutano wa vokali.
(vii) Mkubaliano wa vokali.
(viii) Kupata ughuna
(ix) Kupotea ughuna
(x) Kudhoofika kwa sauti.
(xi) Kukazana kwa sauti.

Lakini zamu hii, tutayapanga mabadiliko yale, kwa; konsonanti kwa upande mmoja na vokali, kwa upande mwingine.

## 5.2.0 MABADILIKO YANAYOHUSU KONSONANTI

Chini ya sehemu hii tutateleza halia zinazohusu konsonanti, au katika maumbo ya ndani, ama ya nje.

Mabadiliko haya na:

(i) Ukakaaishaji.
(ii) Kudondoshwa kwa konsonanti.
(iii) Kuathiriwa kwa nasali kuhusu mahali pa kutamkia.
(iv) Sifa ya ughuna.
(v) Sifa: Kusoghuna.
(vi) Kudhoofika kwa sauti.
(vii) Kukazana kwa sauti.

## 5.2.1 UKAKAAISHAJI

Halia hii imejitokeza katika Kiswahili sanifu, Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete.

Mfanyiko huu umejitokeza kama mfanyiko wa kifonolojia, katika lahaja tatu zile.

Kichocheo chake ni sifa ya vokali ya [+ juu] kutangulia konsonanti, na kisha kufuatiwa na vokali nyingine, katika Kiswahili sanifu.

Lakini katika Kikikuyu, ukakaaishaji unajitokeza kabla ya vokali nyinginezo, kama vile [a], [ɛ], na [ị].

Hata hivyo, mazingira yale, ambayo ni kabla ya kiambishi cha pronomino ya nafsi ya kwanza umoja {n-} yanawezekana iwe mofimu ile ipo wakati ilikuwa {ni-}, au [n̩ ].

Bakari (1982) anatoa pendekezo kama lile ambapo neno kama vile [ čiazi ], katika Chijomvu linatokana na:

K→Kʸ→ Č / – [i]

Au neno [nama] katika Kitikuu.

Linakuwa si /N + ama/→ [n̪ama], kwani hatuoni sifa yenye uasilia, ya kufanya /N/ iwe [n̪], kwa mora moja ile.

Ila inakuwa: Bakari (1982)

* /Ni + ama/ → /nʸ+ama/→ /ɲama/ ⟶ [n̪ama]

Kwa hivyo, pendekezo ni kuwa mifano kama vile:

| Umbo ndani | | umbo nje | othografia | |
|---|---|---|---|---|
| /n + aɲorɛ / | ⟶ | [ɲanorɛ ] | 'nianue' | |
| /n + ɛ̃ǰ ɛ / | ⟶ | [ ɲ ɛ̃ǰ ɛ ] | 'ninyoe ' | |
| Inatokana na: | | | | |
| */ni + anorɛ/ | ⟶ | /nʸ+ anorɛ/ | ⟶ [ɲanorɛ ] | 'nianue' |
| */ni +ɛǰɛ/ | ⟶ | /nʸ+ɛǰɛ/ | ⟶ [ ɲɛⁿǰɛ ] | ninyoe |

## 5.3.2 KUDONDOSHWA KWA KONSONANTI

Katika isimu, dhana ya kudondoshwa kwa konsonanti inaambatanishwa na kuunda muundo sahili zaidi, wa silabi.

Halia hii inajitokeza katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete kama mfanyiko wa kimofofonolojia.

Sifa ambayo inachochea; kudondoshwa huku ni kupakana kwa sauti mbili, ambazo zote ni [-silabi], kama kwa mfano katika /n+riŋgɛ/ ambalo lina maana ya nipige'.

Tukizingatia sifa bainishi, tutapata kwamba muundo wa silabi ni:

[-silabi] [-silabi] [+silabi] [-silabi] [-silabi] [+silabi]

Muundo wa silabi katika mfano huu ni kkvkkv. Konsonanti ile inapododoshwa, tunapata KVKKV.

Kwa hivyo kichocheo cha kifonetiki katika konsonanti kupotea, ni sifa [- silabi].

## 5.3.3 KUATHIRIWA KWA NASALI KUHUSU MAHALI PA KUTAMKIA

Katika Kiswahili sanifu, sheria hii inajitokeza kama sheria ya kifonolojia, kwani inatekelezwa kote kote katika ngeli ya 9.

Katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete mfanyiko huu ni wa kimofofonolojia.

Tunasema hivyo kwa sababu unatekelezwa katika vitomeo vinginevyo katika ngeli ya tisa, wala si vyote, kama tulivyoeleza katika 3.2.1.

Hata hivyo, kichocheo cha kifonetiki ni [$\alpha$ mahali].

Tunasema hivyo kwa sababu nasali ile inakubaliana, unyounyo, na sifa ya mahali pa kutamkia, yo-yote ile, ya konsonanti inayoifuatia.

## 5.3.4 KUPATA KWA UGHUNA:

Halia hii ilijitokeza katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete kama mfanyiko wa kimofofonolojia.

Tunasema hivyo kwa kuwa halia hiyo haikutekelezwa katika mazingira yote, ila ni kitomeo fulani, katika pronomino ya nafsi ya kwanza umoja {n-} kutangulia shina la kitenzi linaloanzwa kwa sauti za mtuo, /K/ na /t/.

Sifa inayochochea mfanyiko huu ni kuwa nasali ni sauti ambayo ina sifa ya ughuna. Kwa hivyo, inapotangulia sauti kama [k] au [t] ambazo ni [- ghuna], sifa ile ya [+ ghuna] inaathiriwa kwa sauti hizi.

## 5.3.5 SHERIA YA DAHL

Katika mabadiliko haya, /k/ imebadilika na kuwa [ɣ], katika faridi nyinginezo, za ngeli ya 12, katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete.

Sheria hii imedhihirika kuwa ya kimofofonolojia.

Tukizingatia mifano kama vile:

/ka + N + kari/ ⟶ /ka # gari/ ⟶ [ɣakari] 'kijigari'
/ka + N + kema/ ⟶ /ka # gema/ ⟶ [ɣakɛma] 'kijinyani'
/ka + N + kware/ ⟶ /ka # gwarɛ/ ⟶ [ɣakwarɛ] 'kijikware'
./ka + N + to:ɣa/ ⟶ /ka # ndoiɣa/ ⟶ [ɣato:ɣa] 'ki jitwiga'

Karega (1977:154} anaeleza kuhusu halia hii, ambayo ni sheria ya Dahl:

> "Sheria ya Dahl ni sheria ya kupata kwa ughuna ambayo inapatikana katika lugha nyingi za Kibantu".[9]

Huu ni mfano wa athari kwa mbali. Tutaiita halia asilia, kwa sababu ya kupatikana katika lugha nyingi (za Kibantu); na kuwa nasali inaathiri kutoka mbali.

## 5.3.6 KUKAZANA KWA SAUTI

Kulingana na Hooper (1976:206); Ruwaza ya kukazana kwa sauti ni kama vile:

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
|---|---|---|---|---|---|
| [nusu - vokali] | [vilainisho] | [nasali] | [+ mfululizo, + sauti] | [+ mfululizo, - sauti] | [+ mtuo, - sauti] ⟶ |

Ikiwa sauti zinapanda po-pote kutoka 1, kuelekea 6 sauti hizo zinasemekana kuwa zimekazana.

Halia hii inajitokeza katika Kiswahili sanifu kama sheria ya kimofofonolojia katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete.

Kwa mujibu wa mifano ya:

(i) [l] → [z]
(ii) [l] → [v]
(iii) [l] → [d]
(iv) [r] → [d]
(v) [w] → [b]

Sifa ambayo inaelekea kubadilika, ni [+vokali] kuwa [-vokali], katika mifano yote ile.

Tunasema hivyo kwa sababu, tukizingatia sifa za vikundi asilia, tunapata.

(i) $$\begin{bmatrix} + \text{konsonanti} \\ + \text{vokali} \end{bmatrix} \rightarrow \begin{bmatrix} \alpha\ \text{konsonanti} \\ - \text{vokali} \end{bmatrix}$$

(ii) $$\begin{bmatrix} + \text{konsonanti} \\ + \text{vokali} \end{bmatrix} \rightarrow \begin{bmatrix} \alpha\ \text{konsonanti} \\ - \text{vokali} \end{bmatrix}$$

(iii) $$\begin{bmatrix} + \text{konsonanti} \\ + \text{vokali} \end{bmatrix} \rightarrow \begin{bmatrix} \alpha\ \text{konsonanti} \\ - \text{vokali} \end{bmatrix}$$

(iv) $$\begin{bmatrix} + \text{konsonanti} \\ + \text{vokali} \end{bmatrix} \rightarrow \begin{bmatrix} \alpha\ \text{konsonanti} \\ - \text{vokali} \end{bmatrix}$$

(v) $$\begin{bmatrix} - \text{konsonanti} \\ - \text{vokali} \end{bmatrix} \rightarrow \begin{bmatrix} + \text{konsonanti} \\ \alpha\ \text{vokali} \end{bmatrix}$$

Kutoka (i) hadi (iv), sifa inayopotea ni ya kuwa [+ mfululizo]. Kwa hivyo, [+ mfululizo] → [- mfululizo]

Katika (v) [Konsonanti] inakuwa [+ konsonanti]. Kwa hivyo vichocheo vya kifonetiki vya kukazana kwa sauti ni sifa za [mfululizo], na [konsonanti]

## 5.3.7 KUDHOOFIKA KWA SAUTI

Katika mchoro wetu:

1 2 3 4 5 6

← usu - vokali] [vilainisho] [nasali] $\begin{bmatrix} + \text{mfululizo} \\ + \text{sauti} \end{bmatrix}$ $\begin{bmatrix} + \text{mfululizo} \\ - \text{sauti} \end{bmatrix}$ $\begin{bmatrix} + \text{mtuo} \\ - \text{sauti} \end{bmatrix}$

Kuelekea upande wa mshale ; ikiwa sauti zimeteremka kati ya 6, kuelekea 1, sauti hizo zitasemekana kuwa zimedhoofika.

Halia hii inajitokeza katika Kiswahili sanifu kama mfanyiko wa kimofofonolojia.

Tukizingatia sauti ambazo zinabadilika:

(i) [k] → [š]
(ii) [ǰ] → [z]
(iii) [d] → [z]
(iv) [g] → [ǰ]
(v) [k] → [ʃ]

Kwa mujibu wa sifa - bainishi tunapata;

(i) [- mfululizo] → [+ mfululizo]
(ii) [- mfululizo] → [+ mfululizo]
(iii) [- mfululizo] → [+ mfululizo]
(iv) [- mfululizo] → [+ mfululizo]

Sifa inayochochea kudhoofika, katika Kiswahili sanifu ni sifa ya [mfululizo].

## 5.4.0 MABADILIKO YANAYOHUSU VOKALI

Katika sehemu hii, tutaeleza uasilia wa mabadiliko yale yanayohusu vokali, kama vile:

5.4.1: Kuundwa kwa nusu-vokali
5.4.2: Kudondoshwa kwa vokali.
5.4.3: Mvutano wa vokali.
5.4.4: Mkubaliano wa vokali.

## 5.4.1 KUUNDWA KWA NUSU VOKALI

Mfanyiko huu umejitokeza kama halia ya kifonolojia katika Kiswahili sanifu, lakini; kama ya kimofofonolojia, katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete.

Tunasema vile kwa sababu; katika Kiswahili sanifu, kila mara ambapo vokali;

[u] + [a] → [w]
[u] + [ɛ] → [w]
[u] + [i] → [w]
[i] + [a] → [j]
[i] + [ɔ] → [j]
[i] + [ɛ] → [j]

Zinafuatana nusu-vokali za [w] na [j] zinaundwa, katika mazingira yake.

Katika Kikikuyu sanifu, na Kikikuyu cha Kabete, sio mazingira yote ya:

[o] + [a]
[o] + [i]
[o] + [ɛ]

yanazipa nusu-vokali kuundwa. Mifano ya isikoundwa ni kama vile:

/mo + ini/ → [moini] → mwimbaji

Kichocheo cha kuundwa kwa nusu-vokali ni sifa ya [usilabi].

Zinapofuatana sauti mbili au vokali mbili, ambazo ni [+silabi] [+ silabi] au VV sauti moja ambayo ni [+silabi] inapoteza usilabi wake, ili kusahilisha muundo wa silabi.

### 5.4.2 KUDONDOSHWA KWA VOKALI

Halia hii imejitokeza katika Kiswahili sanifu, kama halia ya kimofofonolojia.

Sifa ya kifonetiki inayochochea mabadiliko haya ni sifa ya [u silabi].

Katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete, mfanyiko huu ni wa kimofofonolojia.

Sifa ya [usilabi] inasemekana kuchochea mfanyiko huu, kwani pawapo na mfuatano wa vokali mbili, kama ilivyo katika data yetu ya Kikikuyu, pana msongamano wa sifa; [+ silabi], [+ silabi].

Kwa hivyo, mojawapo wa vokali hizi mbili inadondoshwa, ili kusahilisha muundo ule wa silabi, ambao; unaopendekezwa ni:[-silabi], [+ silabi], [- silabi], [+ silabi].

Katika Kiswahili sanifu, vokali inadondoshwa hata kabla ya nasali, kama katika /mu + gawɛ/ ⟶ /mgawɛ/ ⟶[m̩gawɛ], au /a + mu + hɔŋgɛ/ ⟶ [am̩hɔŋgɛ], kwa kichocheo chicho hicho, [usilabi] kwani hata vokali inapopotea, sifa ya [usilabi] inabebwa na nasali.

## 5.4.3 MVUTANO WA VOKALI

Halia hii imejitokeza katika Kiswahili sanifu, kama halia ya kifonolojia.

Vokali za [a] na [i] zinapopakana katika ngeli za 2, 6 na 16; na vokali za [a] na [ɛ], zinaelekea kuathiriana, kuhusu sifa ya [urefu].

Kwa hivyo:

(i) [a]+[i] ⟶ [ɛ]

(ii) [a]+[ɛ] ⟶ [ɛ]

Kwa hivyo uasilia wa mfanyiko wa mvutano wa vokali ni sifa [d urefu].

Tunasema [d] kwa sababu, katika (i)

$$[+\text{ chini}] + \begin{bmatrix} +\text{ juu} \\ +\text{ mbele} \end{bmatrix} \rightarrow \begin{bmatrix} -\text{ juu} \\ -\text{chini} \end{bmatrix}$$

na katika (ii)

$$[+\text{ chini}] + \begin{bmatrix} +\text{ juu} \\ -\text{chini} \end{bmatrix} \rightarrow \begin{bmatrix} \alpha\text{ juu} \\ \alpha\text{ chini} \end{bmatrix}$$

## 5.4.4 MKUBALIANO WA VOKALI

Mfanyiko huu umedhihirika katika Kiswahili sanifu, Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete.

Halia hii ni ya kimofofonolojia, kwani ikitekelezwa katika mazingira tofuati tofauti, katika lahaja tulizozishughulikia.

Hatuwezi kuiita halia ya kifonolojia, katika usafi wake, kwa kuwa sifa ya kuathiri ni au urefu, au umbele na kila moja ikitekelezwa kwa namna yake.

Uasilia ambao tunaweza kuambatanisha kama kichocheo cha halia hii ni sifa:

[α urefu], na sifa [α mbele] .

## 5.5.0 HITIMISHO

Katika sura hii, lengo letu lilikuwa kusitiri dai tulilolitoa katika sehemu ya 1.5.0, kwamba uasilia wa mabadiliko ya kisauti ambayo tumeyashughulikia yanaweza kuelezewa kwa tafswili, katika kiunzi cha nadharia yetu, fonolojia asilia zalishi.

Baada ya kujadilia jukumu la fonolojia asilia zalishi katika sehemu ya 5.1.0, tumeendeleza mjadala wa dhana ya uasilia kama alivyosema Hooper (1976).

Tumeendelea kuorodhesha aina ya sheria za Kifonolojia ambazo zipo katika Kiwahili sanifu, Kikikuyu sanifu, na kisha Kikikuyu cha Kabete.

Tumefanya hivyo, kwani Hooper (1976:3) anatueleza kuwa hilo ni jukumu moja kati ya majukumu ya nadharia asilia zalishi.

Anatukumbusha kwamba tunapoonyesha seti ya sheria ambazo zipo katika ilhamu ya mzungumzaji - mzaliwa, huwa tunaandika sarufi ya lugha ile.

Kwa kurejelea jambo hili, katika utafiti wetu tunaweza kusema kuwa nia yetu imekuwa kuchangia katika kuandika sarufi ya Kiswahili sanifu, Kikikuyu sanifu, na Kikikuyu cha Kabete, katika kiwango cha fonolojia.

Jambo ambalo tunakiri, pamoja na Hooper (1976:xii) ni kwamba nadharia ya fonolojia asilia zalishi ina matatizo yake, kiutekelezi, kama zilivyo nadharia nyinginezo za isimu.

Kile ambacho tunaweza kusema ni kuwa imetumulikia mwangaza katika hali ya kueleza uasilia, na mabadiliko ya kisauti katika Kiswahili sanifu, Kikikuyu sanifu; na Kikikuyu cha Kabete.

Chambilecho Hooper (1976:xii):

> "Hakuna makubaliano ya aina moja miongoni mwa wanaisimu ambao wanaitumia nadharia dhabiti; na kwa hivyo kile ambacho kipo katika kitabu hiki ni fasili yangu ya nadharia asilia zalishi ambayo inatofautiana wastani na maoni mengineyo kuhusu nadharia hii. Yapo maswali

mengine ya kiuthibitishi, ambayo hayajajibiwa. Maswali haya yanazuka katika nyanja za mofolojia na uasilia wa sheria za kifonolojia. Hivi; msomaji atapata kiunzi kipya ambacho muundo wake umeundwa kwa kina cha kutosha kuweza kuwasilishwa kama nadharia yenye mantiki; na ambayo pia: inazusha maswali yanayotuelekeza katika rutuba ya kuelewa uasilia wa halia, katika lugha."[10]

TANBIHI

1. J.B. Hooper, (1976:3) An Introduction to Natural Generative Phonology. New York Academic Press. 3

2. ____________, (opp.cit). 133

3. ____________, (opp.cit). 133.

4. ____________, (opp.cit). 102

5. ____________, (opp.cit). 102

6. ____________, (opp.cit). 133

7. ____________, (opp.cit). 131

8. ____________, (opp.cit). xii

## SURA YA SITA

### UTANGULIZI

Utafiti huu ulidhamiria kulinganisha halia za kifonolojia katika lugha tatu za kibinadamu; Kiswahili sanifu kwa upande mmoja na Kikikuyu sanifu kwa upande wa pili.

Lakini tukaonelea kuwa tungeweza kuupa utafiti wetu uzito zaidi, pindi tungelinganisha fonolojia ya Kikikuyu sanifu sawia na fonolojia ya lahaja ya Kikikuyu ambayo inapewa kielezi cha kijamii.

Katika 1.0.0. , tulieleza tatizo la kufasili eneo la Kabete.

Tatizo hili lilizuka kutokana na ukweli kwamba wazungumzaji wazaliwa tofauti na kutoka maeneo tofauti wanatoa fasiri tofauti kuhusu eneo la Kabete; japo wanakiri kwamba lipo, na wapo Wakikuyu wa Kabete.

Pengine tungerejelea upya maoni ya watu wa Gichugu; moja katika lahaja ambazo alianisha Karega (1977) ili kuthibitisha utata wa kufasili eneo la Kabete.

Anasema, (1977 : 3)

"Watu wa Gichugu wanadai ya kuwa wanatofautiana sana kiismu, na kuwa mtu ye-yote anayezungumza lahaja iliyo kusini mwa Ndia, ni Mokabete"[1] .

Kwa "Wakabete" wenyewe, wanachukulia kuwa yule anayeweza kudai kuwa ni mzungumzaji - mzaliwa ni vizazi viwili ambavyo vimezaliwa katika eneo la Kabete, Kangemi, Gatina, Riruta, Ndumbu-ini, Uthiru Kinoo na hata Gitaru.

Kinoo na Gitaru zipo katika wilaya ya Kiambu, ilhali Kangemi Kabete, Uthiru, Gatina, Riruta na Ndumbuini zipo katika wilaya ya Nairobi.

Lakini, tena, kati yao, wapo wazungumzaji-wazaliwa ambao wanadai kuwa watu wa Gitaru sio "Wakabete".

Almuradi utata huu wa fasili ya kimaeneo umetupa kutumia neno Kabete kama istilahi, ambayo inasimamia mjadala ule, wa Kabete ni wapi.

Katika sehemu hiyo hiyo, 1.0.0., tuliorodhesha fonimu na vokali ambazo zinapatikana katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete, na kujitokeza na matokeo sawa.

Lengo letu lilikuwa kulinganisha, hatimaye, Kiswahili sanifu kwa upande wake, na kwa upande wa pili, lahaja sanifu ya Kikikuyu, na lahaja nyingineyo ambayo inajulikana, kijamii na wazungumzaji - wazaliwa wengine.

Katika sura ya pili tulionyesha mifanyiko ya kisauti ambayo inapatikana katika Kiswahili sanifu.

Katika sura ya tatu, tulionyesha halia za kifonolojia, ambazo zinapatikana katika Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete; ili tuweze kulinganisha lahaja hizi na

Kiswahili sanifu.

Matokeo yalikuwa kwamba, Kikikuyu sanifu hakikuonyesha kutofautiana hata kidogo na Kikikuyu cha Kabete.

Zote zikiwa chini ya lahaja ya kusini: Karega (1977); sasa katika viwango vitatu: kiwango cha sauti; kiwango cha mofolojia; na cha fonolojia, tuna sababu ya kusema kuwa, isipokuwa tofauti ya fasili na lakabu, Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha Kabete zimethibiti faridi sawa za kiismu, na kuwa tofauti ni taasubi ya lugha tu, ambapo kila mzungumzaji; hutaka ile anayoiita lugha yake, iwe ndiyo bora kuliko nyinginezo.

Almuradi, sura ya pili na tatu zimethibitisha haipothesia yetu ya kwanza, ambayo inaelekea kudai kuwa halia za kifonolojia zipo, katika kila mojawapo ya lahaja hizi.

Katika sehemu ya 1.5.0, tulidai pia kuwa upo ulinganifu wa aina fulani, kati ya mifanyiko ya kisauti inayopatikana katika; Kiswahili sanifu kwa upande wake, na; Kikikuyu sanifu pamoja na Kikikuyu cha Kabete kwa upande wa pili.

Kwa kulinganisha Kikikuyu sanifu na Kikikuyu cha kabete katika sura ya tatu, tulikuta kuwa haipo tofauti, hata moja, katika kiwango kile, kati ya lahaja hizi mbili.

Hata hivyo, na tukichukulia matokeo haya kuwa sawa; tulipolinganisha Kikikuyu sanifu, sasa na Kiswahili sanifu, tulipata kuwa zipo tofauti kadha, kati ya lugha hizi mbili.

Tutaeleza jambo hili kwa undani kidogo.

## ULINGANISHI.

Tukirejelea jumla ya mabadiliko ya kifonolojia, tunapata kuwa zipo halia ambazo zilijitokeza katika Kiswahili sanifu na Kikikuyu sanifu, ihali mifanyiko mingine inapatikana katika lahaja moja, au nyingine.

Halia ambazo zilidhihirika katika lahaja zote mbili ni kama vile:

(i) Kuundwa kwa nusu -vokali

(ii) Kudondoshwa kwa vokali (iii) Ukakaaishaji

(v) Kuathiriwa kwa nasali kuhusu mahali pa kutamkia

(v) Mkubaliano wa vokali

(vi) Kukazana kwa sauti.

Halia hizi ziliekea kupatikana katika Kikikuyu sanifu, bila kupatikana katika Kiswahili sanifu ndizo :

(i) Kudondoshwa kwa konsonanti

(ii) Sifa ya kupata ughuna

(iii) Sheria ya Dahl.

Nazo zile ambazo zimejitokeza katika Kiswahili sanifu bila kuwepo katika Kikikuyu sanifu ni mbili tu. Ndizo:

(i) Mvutano wa vokali

(ii) Kudhoofika kwa sauti.

Kati ya halia ambazo zinajitokeza katika lahaja zote mbili, bado zipo tofauti za kimazingira.

Kwa mfano, nusu - vokali inaundwa katika mazingira mapana zaidi, katika Kiswahili sanifu, kuliko inavyokuwa, katika Kikikuyu sanifu, na kudondoshwa kwa vokali; vile vile.

Mfanyiko ambao unaelekea kuenea katika mazingira karibu sawa, katika Kiswahili sanifu na Kikikuyu sanifu ni ukakaaishaji.

Hapa lahaja zote mbili zimekaribiana mizani. kuhusu kuathiriwa kwa nasali kuhusu mahali pa kutamkia Kikikuyu sanifu na Kiswahili sanifu.

Tofauti nyingineo kuhusu halia ambayo inapatikana katika lahaja zote mbili zile.

Katika Kiswahili sanifu mkubaliano wa vokali unapatikana katika vokali ya shina la kitenzi, na vokali iliyoko katika mofimu ya kunyambua kitenzi.

Katika Kikikuyu, sanifu, mifano ya mkubaliano wa vokali katika mazingira kama yale ni michache.

Lakini katika mazingira ya kuundia nomino kutoka vitenzi mifano ipo, chungu nzima.

Halia ya mwisho ambayo inathibitiika katika lahaja hizi mbili; Kiswahili sanifu na Kikikuyu sanifu ni kukazana kwa sauti.

Kwa mara ya pili tena, lahaja zote mbili zinaelekea kutoshana mizani. Halia hii inaenea katika mazingira, karibu ya upana sawa.

Kwa hivyo, hata vile zipo halia ambazo zimejitokeza katika lahaja moja wala si nyingine, lahaja zile hazikutofautiana kote kote.

Kwa mazingira; na halia ambazo tumeorodhesha katika sehemu hii ya 6.1.0; Kiswahili sanifu kimetofautiana na Kikikuyu sanifu. Lakini lahaja zile zimeelekea kuwa karibu pacha, kimaenezi, kuhusu ukakaaishaji; na kukazana kwa sauti.

## 6.2.0 HITIMISHO

Tulihitimisha mtaala wa halia za kifonolojia kwa kueleza uasilia wa mabadiliko yote yale, ya kisauti ambayo yajitokeza katika lahaja tulizozishughulikia Kiswahili sanifu; dhidi ya Kikikuyu sanifu pamoja na Kikikuyu cha Kabete.

Mizani yetu ya kupimia uasilia iliegemea maoni ya Hooper (1976: 131) ambaye

anaeleza uasilia kwa; misingi ya kifonetiki; au kupatikana kwa halia ya kisauti katika baadhi ya lugha za kibinadamu.

Ilivyojitokeza ni kwamba mifanyiko ya kifonolojia, katika Kiswahili sanifu, na Kikikuyu ilielekea kuthibitisha vichocheo vya kifonetiki.

Halia zile, kama ilivyo sifa bia, hazikutokea bilashi. Chambilecho Hooper (1976:4): "Lengo la mbali la isimu - nadharia ni kuunda nadharia ambayo udhabiti wake unatosha tu kufasili, kwa makini ithibati zote za lugha"[2]

6.2.1 PENDEKEZO

Kabla hatujapendekeza jambo lo-lote, katika utafiti wetu tunataka kurejelea umuhimu wa ithibati, au dhana ya usayansi katika utafiti wo-wote, na kwa muktadha huu, lugha.

Hooper (1976:xii) anaeleza sifa-thibitiki katika nadharia asilia.

Kwa sababu hiyo, tunatilia mkazo wazo la kuepusha masiala ya utafiti wa lugha na hisia - nafsia.

Pengine tungemrejelea Wardhaugh (1986:24) ili tuweze kubainisha pendekezo. Analenga ndipo anaposema:

" Wazungumzaji wengi wanaweza kuipa lugha wanayoizungumza lakabu. Mara kwa mara utakuta kuwa majina hayo yana aina ya ugeni, kwa wale ambao wanafanya utafiti kisayansi. Lakini inatupasa kukumbuka kuwa, lakabu azitoazo mwanadamu mara nyingi hazina usayansi wo-wote: kisifa".[3]

Lakini mjadala kuhusu jina, na sifa inayoambatanishwa na jina si wa karne hii. Ni mjadala ulioanza na kuendelezwa tangu siku za Aristotle.

Dineen (1967: 9) anasema kuhusu jambo hili:

"Hakuna uhusiano wa moja kwa moja, kati ya maumbile ya vitu au dhana ambazo lugha inajihusisha nayo na faridi za kiismu au ruwaza zake ambazo kwanza, vitu hivi, au dhana hizi zinaeleza".[4]

Sababu ya kurejelea haya ni kwa sababu ya majina kama "Sanifu" na "Kikabete".

Neno "Mokabete" linaambatanishwa, si sana na maeneo ya Kabete: kama sifa ya mzungumzaji - mzaliwa· "Mokabete".

Kwa mzungumzaji -mzaliwa mwinginewe, kama vile wa Murang'a, Nyeri hata Kiambu, Kabete ni eneo la Wakikuyu "walaghai", 'wasioaminika' na wazungumzaji - wengine.

Kwa sababu hiyo, mzungumzaji - mzaliwa mwinginewe anapokuita "Mokabete", si

fasili ya kijografia anaiyoitoa bali anakupiga kijembe.

Lakini tulipozingatia vigezo thibitiki; fonolojia asilia zalishi, tumekuta kuwa lahaja mbili sanifu, zimethibiti halia bia za kisauti; kama ilivyothibiti lahaja ambayo imesutwa siku nyingi; "Kikikuyu cha Kabete".

Ikiwa tunaweza kuzivua taasubi zetu za kinafsia, kuhusu lugha nyingi za kibinadamu, tunaweza kugundua mengi kuhusu lugha hizo.

Chomsky (1965) miongoni mwa mijadala yake anatueleza kuwa lugha ya kibinadam ni lugha ya kibinadam, na haipo; lugha bora kuliko nyingine.

Cha muhimu katika mikabala yetu kama wanaisimu, ni kile ambacho Bakari (1982:29) anamulikia, anaposema;

> "Kuonyesha ithibati ; au : jongo ; katika kiunzi - nadharia kumekuwa moja katika masiala yale muhimu, katika falsafa ya sayansi"[5] .

TANBIHI.

1. E. K. Karega, (1977): Sound change and classification of the of the Dialects of Southern Mt. Kenya. Ph.D Thesis. University of Nairobi. 3

2. J. B. Hooper, (1976) : An Introduction to Natural Generative Phonology. New York Academic Press. 4

3. R. Wardhaugh (1986) : An introduction to Sociolinguistics. Basil Blackwell Inc. Oxford. 24.

4. F. P. Dineen, (1967) : An Introduction to General Linguistics. Holt, Rinehart and Winston, Inc. 9.

5. M. Bakari, (1982) : The Morphohonology of the Kenyan Kiswahili Dialects. Ph. D Thesis. University of Nairobi. 5.

## MAREJELEO


Abdalla, A. (1976) : Sauti ya Dhiki. Oxford University Press. Nairobi.

Bakari, M. (1982): The Morphophonology of the Kenyan Swahili Dialects. Ph. D Thesis. University of Nairobi.

Bennet, P.R. (1969): A Comparative Study of four Thagicũ verbal stems: the inflectional systems of Kikuyu, Kamba, Embu and Mwimbi. Thesis: microfilm. University of London.

Chomsky, N. (1964) : Current issues in Linguistic Theory. Mouton & Co. N.V Publishers; The Hague.

Chomsky, N. (1965): Aspects of the Theory of Syntax. Cambridge, M.I.T Press.

Chomsky, N. & M. Halle (1968): The Sound Pattern of English. Harper & Row.

Dineen, F.P. (1967): An Introduction to General Linguistics. Holt, Rinehart and Winston, Inc.

Foley, J. (1977): Foundations of Theoretical Phonology. Cambridge University Press. Cambridge.

Ford, K. (1974): Tone and Intonation in Kikuyu. Xerox copy. University of Nairobi.

Hooper, J.B. (1976): An Introduction to Natural Generative Phonology. New York Academic Press.

Hyman, L.M. (1975): Phonology : Theory and Analysis. Holt, Rinehart and Winston, Inc.

Karega, E.K. (1977): Sound Change and Classification of the Dialects of Southern Mt. Kenya. Ph. D. Thesis. University of Nairobi.

Katz, J.J. & Fodor, J.A. (1964): Readings in the Philosophy of Language. Prentice - Hall Inc. Englewood Cliffs, New Jersey.

Kithaka wa Mberia, (1981): The Consonants of Kitharaka. M.A. Thesis. University of Nairobi.

Maganga, C. (1990): The Morphophonology of Standard Kiswahili, Kimakunduchi, Kitumbatu and Kipemba. Ph. D Thesis Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Maringah, E.I. (1987): A Comparative Analysis of verbal Extensions in Kimbeere & Kiswahili. M. A. Thesis. University of Nairobi.

Mukuriah, D.M (1987): Mpangilio wa Ngeli: Ulinganishi wa Ngeli za Kiswahili Sanifu na Kikikuyu cha Kiambu. M.A. Thesis . University of Nairobi.

Njage, J.W. (1982): The Acquisition of Kikuyu Phonology. M.A. Thesis. University of Nairobi.

Polome, E.C. (1967): Swahili Language Handbook. Center for Applied Linguistics. 1717 Massachusetts Avenue, New York, Washington D.C.


Schane, S.A. (1973): Generative Phonology. Prentice - Hall Inc. Englewood Cliffs. New Jersey.

Schane, S.A. (1973): "Natural Rules in Phonology". Katika R.P. Stockwell na Ronald K.S. Macaulay. (eds). Linguistic Change and Generative Theory. Bloomington. Indiana University Press.


Tuki, (1990): Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha . Chuo Kikuu cha Dar -es - Salaam.

Wardhaugh, R. (1986): An Introduction to Sociolinguistics. Basil Blackwell Ltd. 108 Cowley Road; Oxford. OX 4 IJF. U. K.


VOKALI ZA KISWAHILI SANIFU



VOKALI ZA KIKIKUYU SANIFU



VOKALI ZA KIKIKUYU CHA KABETE



KONSONANTI ZA KISWAHILI SANIFU

| | Midomo | Midomo & Meno | Meno | Ufizi | Kaakaa - Ngumu | Kaakaa - Laini | Kidaka - tonge | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mtuo | p b | | | t d | | k g | | |
| Mkwaruzo | | f v | θ ð | s z | | ɣ | h | |
| Mtuo - Mkwaruzo. | | | | š, č | ǰ | | | |
| Vilainisho | | | | l r | | | | |
| Nusu- vokali | | w | | | j | | | |
| Nasali | m | | | n | ɲ | ŋ | | |

## KONSONANTI ZA KIKIKUYU SANIFU

| | Midomo | Midomo & Meno | Meno | Ufizi | Kaakaa - Ngumu | Kaakaa - Laini | Kidaka - tonge | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mtuo | b | | | t<br>d | | k<br>g | | |
| Mkwaruzo | β | | ð | | | ɣ | h | |
| Mtuo - Mkwaruzo | | | | š | ǰ | | | |
| Vilainisho | | | | ŕ | | | | |
| Nusu - Vokali | | w | | | j | | | |
| Nasali | m | | | n | ɲ | ŋ | | |

## KONSONANTI ZA KIKIKUYU CHA KABETE

| | Midomo | Midomo & Meno | Meno | Ufizi | Kaakaa - Ngumu | Kaakaa - Laini | Kidaka - tonge | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mtuo | p<br>b | | | t<br>d | | k<br>g | | |
| Mkwaruzo | β | | | ð | | ɣ | h | |
| Mtuo - Mkwaruzo | | | | š | ǰ | | | |
| Vilainisho | | | | r | | | | |
| Nusu - vokali | | w | | | j | | | |
| Nasali | m | | | n | ɲ | ŋ | | |

+ Mpaka wa mofimu

# Mpaka wa neno

/ / Mabano ya kifonimu

[ ] Mabano ya kifonetiki.